ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Pili– Tarehe 16 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba hukusu Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Waziri Kivuli, naomba turudi kwenye orodha ya shughuli za leo kwenye sehemu ya Waziri Kivuli tufanye marekebisho kidogo, kumekuwa na *printing mistake* imeandikwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, tubadilishe iwe Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Nakushukuruni waheshimiwa wajumbe.

Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny: Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani pamoja na Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na mambo yanayohusiana nayo.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 14

Jeshi la Wananchi wa Tanzania (J.W.T.Z) Kutoa Huduma za Kijamii, Zanzibar

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Tunapenda kulipongeza Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, kwa kuadhimisha miaka 45 ya kuundwa kwakwe. Pongezi zetu zaidi zinalenga kwa Jeshi letu kutokana na utaratibu uliojiwekea wa kutoa huduma za kijamii kwa wananchi wetu wa Tanzania, katika kuadhimisha sherehe za kila mwaka.

(a) Mhe. Waziri kuna huduma yoyote ya kijamii iliyotolewa kwa wananchi wetu wa Zanzibar, wakati wa sherehe za miaka 45 ya kuanzishwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania?

(b) Je, kama ipo ni sehemu gani na imewanufaisha wananchi wangapi?

(c) Kwa kuwa wawakilishi ni sehemu kubwa ya jamii ya Zanzibar. Je, huoni kuwa ipo haja ya kushirikishwa ipasavyo katika utowaji wa huduma hizo ili wafahamu namna zinavyotolewa katika majimbo yao?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako nami naungana na Mheshimiwa mwakilishi kulipongeza Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, kwa kuadhimisha miaka 45 ya kuundwa kwake na hasa kutokana na utaratibu waliojiwekea wa kutoa huduma za kijamii kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, zipo huduma za kijamii zilizotolewa kwa Wananchi wetu wa Zanzibar wakati wa Sherehe za miaka 45 ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, pamoja na kufanya usafi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

b) Mhe. Spika kama nilivyojibu katika kifungu (a) cha swali hili kwamba usafi umefanywa na Brigedi ya Nyuki umewanufaisha wazanzibar na wageni wetu.

Maeneo yaliyofanyiwa usafi huo kwa Unguja ni pamoja na Hospitali ya Mnazi mmoja, bustani ya Jamhuri, Maruhubi miembe mingi, Kinazini, Uwanja wa ndege, Bustani ya Migombani, Hospitali ya Wazee Welezo, Hospitali ya Kivunge, Beit-el-Ras na Chuo Kikuu cha Ualimu Nkurumah. Kwa upande wa Pemba ni Hospitali ya Chake chake, Hospitali ya Wete na Hospitali ya Vitongoji.

c) Mhe. Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lipo tayari kushirikiana na Waheshimiwa wawakilishi, viongozi pamoja na wananchi wote kuendeleza usafi wa huduma nyengine za jamii katika maeneo yao.

Jeshi la Wananchi linatoa shukurani za dhati kwa Masheha na wananchi wa maeneo yaliyotajwa kwa kutoa mashirikiano ya hali na mali katika zoezi la usafi lililofanyika katika maeneo yao. Kwa vile zoezi hili litakuwa endelevu tunaahidi kutoa mialiko rasmi kwa wabunge na wawakilishi ili tupate ushirikiano wao.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nalipongeza Jeshi letu hili la Wananchi wa Tanzania kwa kutimiza miaka 45 ya kuanzishwa kwa jeshi letu hili.

Lakini nilipongeze jeshi letu hili pamoja na huduma za usafi zinazofanywa katika sehemu mbali mbali za nchi zetu mbili. Kwa kweli mwelekeo wao tumeona wanakwenda kwenye usafi wa mazingira na hili ni jambo zuri kabisa.

Isipokuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa upande wa Tanzania Bara kuna huduma maalum za afya ambazo hutolewa kwa wananchi wetu mbali mbali kwenye sehemu zao, au wanaweka vituo muhimu kwa ajili ya wananchi wale kupata huduma za afya bila ya malipo ambazo ni huduma nzuri kuliko taasisi nyengine zozote.

Je, Mhe. Waziri anao mpango gani kwa kupitia wizara yake pamoja na wizara inayohusika, ili kuhakikisha kwamba kwa kipindi kijacho Mwenyezi Mungu akitufikisha huduma kama ile ipatikane kwa wananchi wetu wa Zanzibar na hasa vijijini wafaidie nayo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, napokea pongezi kutoka kwa Mhe. Mwakilishi kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na

salamu hizi nitazipeleka kwa maandishi, ili na wao waone namna gani waheshimiwa wawakilishi wanavyojali ile huduma wanayoitoa kwa jamii.

Kuhusu suala la kuweka vituo vya afya, kama wanavyofanya kwa wenzetu kule Tanzania Bara. Mhe. Spika, nataka nimthibitishie Mhe. mwakilishi hata hapa Zanzibar Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatoa hizo huduma za afya katika makambi mbali mbali ambazo kuna hospitali.

Kwa mfano, Hospitali ya Bububu ambayo ni hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kweli ni kimbilio kwa wananchi wetu wengi wa Zanzibar, tena wengine wanapopata matatizo huwa wanakwenda huko pamoja na kuwepo kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, sifa za Hospitali ya Bububu zote hapa Zanzibar tunazijua kwa namna ambavyo wanavyofanyakazi vizuri, yaani sawa na ile Hospitali ya Lugalo Dar-es-Salaam.

Kwa hivyo, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wote kwa jumla, kwamba hospitali za wanajeshi zipo wazi na zinafanyakazi kwa kuwahudumia wananchi wote bila ya kuangalia kama huyu ni askari ama ni raia.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake, pia niwapongeze wanajeshi katika sherehe zao pamoja na kutoa huduma. Hivi sasa huduma wanayohitajia zaidi watu ni kuchangia damu kwenye Benki ya Damu. Je, Mhe. Waziri huduma hii anaifikiriaje kuwaambia ndugu zetu wanajeshi ambao ni wakakamavu tena wenye lishe ya kutosha, miongoni mwa sherehe zao wawe na mpango wa kuchangia damu katika benki hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika kutoa huduma za jamii halichagui maeneo ya kufanyia kazi. Kwa sababu mara nyingi huwa wanafanya shughuli mbali mbali kwa kushirikiana na wananchi. Isipokuwa hii siku ya kuadhimisha, yaani siku ya kuzaliwa kwa jeshi ndio kunakuwa na mpango maalum wa kufanya hiyo huduma.

Mhe. Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wao wamo kwenye orodha ya watu ambao wanachangia damu katika Benki yetu ya Damu. Kwa hivyo, kama tunavyowajua majeshi wanakula vizuri tena wanakuwa na afya nzuri, kwa kweli wanatoa damu nyingi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu na damu yao ipo kwenye Benki ya Damu na wananchi wetu wanaitumia.

Nam. 37

Vikundi vya Uzalishaji Chumvi – Pemba

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Katika Kisiwa cha Pemba kuna vikundi vya uzalishaji chumvi visivyopungua hamsini (50), ambavyo vimeundwa kuwawezesha wananchi kujiajiri na kujikimu na maisha. Pia kumeanzishwa Kitengo cha Utiaji wa Madini Joto (*Iodine*) katika chumvi inayozalishwa, ili isiwe na madhara kwa walaji.

(a) Serikali inatoa msukumo gani katika kuviendeleza vikundi hivi?

(b) Ni muda mrefu sasa chumvi huagizwa kutoka nje ya nchi yetu. Je, wizara imekwishafanya utafiti wa kujua mahitaji ya chumvi, ili tuweze kutumia chumvi inayozalishwa ndani ya nchi na kuepuka kuagiza chumvi kutoka nje?

(c) Wazalishaji wengi wa chumvi wanatumia utaalamu duni katika kuzalisha chumvi.Je, wizara ina mpango gani katika kuwaendeleza wazalishaji wa chumvi?

(d) Inaelezwa kwamba chumvi ikiwa haina madini joto huweza kuleta madhara kwa walaji, ni madhara gani hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu inatoa ushauri na elimu kwa vikundi vya uzalishaji wa chumvi, ili viwe imara na endelevu.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwa muda mrefu sasa chumvi huagizwa kutoka nje ya nchi yetu, lakini ni kiasi kidogo tu. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira tayari imekwishafanya utafiti wa kujua mahitaji ya chumvi, ambapo imebainika kuwa kwa kila mtu mmoja anatumia chumvi kwa wastani wa kilogramu 5 hadi 6, kwa maana hiyo tunakisia kwa Zanzibar nzima tunatumia kwa wastani tani 7000 hadi 8000 kwa mwaka kwa nchi nzima. Mhe. Spika, matumizi haya hayahusishi viwanda.

(c) Mhe. Spika, ni kweli wazalishaji wengi wa chumvi wanatumia utaalamu duni katika kuzalisha chumvi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya *AZASPO* na wataalamu wamekuwa wakitoa elimu za uzalishaji chumvi. Hivyo uzalishaji umeanza kuwa bora hivi sasa.

(d) Mhe. Spika, sio kweli kwamba chumvi ikiwa haina madini joto huweza kuleta madhara kwa walaji. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine kama Jumuiya ya *Association of Zanzibar Salt Procesing Organisation* (*AZASPO*) na *UNESCO*, wameweza kufundisha wakulima namna ya kuzalisha chumvi na kuweka *Iodine*, ili kupata mazao mengi na yenye viwango vinavyokubalika. Chumvi inayotengenezwa iwe na kiwango kinachokubalika.

Pia wazalishaji wanapatiwa mafunzo ya viwango ikiwa ni utaratibu wa Umoja wa Mataifa wa kutibu maradhi ya uvimbe wa koo unaoitwa (*Goitre*), ambapo imeonekana kutibika kwake kirahisi ni kuweka madini *Iodine* kwenye chumvi.

Mhe. Najma khalfan Juma: Mhe. Spika, swali langu ni dogo la nyongeza. Kwa kusaidiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, je kuna mpango wowote wa kuwajengea wazalishaji wa chumvi kiwanda ambacho kitatoa chumvi ya unga badala ya kununua nchi za nje na kuileta nchini?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Naomba nitoe taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba wazalishaji wa chumvi wa hapa Zanzibar tayari wameshafunga mitambo ya kusaga kwa ajili ya kuzalisha chumvi ya unga.

Kwa hivyo, jambo la msingi ni kwamba jitihada zitaendelea baina ya serikali na wao wenyewe kwa lengo la kufunga mitambo mingi zaidi, ili waweze kutoa chumvi nyingi zaidi ya unga na ifikie viwango vile ambavyo wanaweza kuuza nchini na nje *(Makofi)*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira wakati alipokuwa akijibu swali mama alisema, hakuna maradhi yoyote yanayoweza kupatikana kama chumvi tunayotumia itakuwa haina madini joto (*Iodine*).

Lakini *Iodine* ni madini ambayo ni muhimu kila binadamu apate kwenye chakula anachokula na kimazingira yanapatikana sana kwenye chumvi. Sasa kama kweli chumvi itakuwa haina haya madini joto ya kutosha kwa kiwango

kinachohitajika na wananchi wakatumia chumvi hii, basi yale maradhi ya *goitre* aliyoyataja yatatokea kwa jamii yetu?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba tena nitoe taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba, wazalishaji wa chumvi Pemba wanaweka *Iodine* katika chumvi wanayoizalisha, tena chumvi ile ni salama kutumika popote pale.

Nadhani kwenye Maonesho ya Asasi za Kiraia yaliyofanyika hapa walituonesha jinsi wanavyofanya na walitoa *hints* ambazo kama mtu anakuwa na wasi wasi basi anaweza kui-*test*. Kwa kweli wanaweka *Iodine* kwa kiwango kinachotakiwa na wanavyo vifaa vya kujaribia kama *Iodine* ile imefikia kiwango kinachotakiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, kuhusiana na suala la maradhi ambalo amelitaja kama itakuwa haina hiyo *Iodine*.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, chumvi ambayo haina *Iodine* upo uwezekano mkubwa wa kusababisha maradhi ya *goitre*. Lakini wazalishaji wetu wanaweka basi hilo litaepukika.

Nam. 5

Ugunduzi wa Mafuta Wakati wa Ukoloni

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Inafahamika wazi kwamba, Zanzibar imetawaliwa na Wakoloni mbali mbali kabla ya Mapinduzi Matukufu ya 1964.

(a) Kwa kuzingatia historia hiyo ya Ukoloni, wizara inamfahamu mtawala yupi aliyegundua nishati ya mafuta na gesi hapa Zanzibar?

(b) Kama imewahi kugundulika nishati hii, ni maeneo yepi na wakati upi wa historia ulishuhudia ugunduzi huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika mwambao wa Visiwa vya Unguja na Pemba ulianza mwaka 1952 mpaka 1964, ambapo Kampuni mbili

zilizokuwa na ubia, yaani *BP* na SHELL zilipewa ruhusa katika maeneo ya Unguja na Pemba. Baada ya utafiti wa kina kufanyika visima viwlii vilichimbwa, visima hivyo vilipewa majina ya Zanzibar – 1, Pemba -5. Visima vyote vilikuwa vikavu.

(a) Mhe. Spika, hakuna mtawala aliyegundua mafuta wala gesi enzi za Ukoloni.

(b) Hakuna eneo ambalo limegunduliwa mafuta katika Visiwa vya Unguja na Pemba, lakini tafiti za mtetemo na zile za akiolojia zinaonyesha uwezekano mkubwa wa kupatikana mafuta na gesi asilia ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe na Wajumbe wote wa baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar, kwa maamuzi yetu thabiti ya kutaka masuala yote ya utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia yatolewe kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Hivyo, mafuta na gesi asilia yatafutwe na kuchimbwa na yakionekana yawe kwa maslahi ya wazanzibar pekee *(Makofi)*.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeza Mhe. Waziri pamoja na wizara kwa jumla, kwa kuhakikisha kwamba msimamo wa serikali upo pale pale kwamba mafuta haya yatakapopatikana basi yawe kwa maslahi ya Wazanzibari. Mhe. Spika, naunga mkono hilo kwa asilimia mia moja na wala sina matatizo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pamoja na hayo yote nataka kuuliza swali moja. Katika kipindi kilichopita cha Baraza lako tukufu Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, kwa kauli njema tuliambiwa kwamba italetwa Sera ya mafuta katika kikao kinachofuata ambacho ndicho hiki kinachoendelea sasa. Lakini kwa bahati mbaya kwenye orodha wa shughuli zote sikuliona hili au sina habari nalo?

Je, Mhe. Spika, suala hili limefikia wapi, lipo au limeishia kwenye maelezo ili sisi wajumbe wako pamoja na wananchi wote wa Zanzibar tuweze kufaidika kwa taarifa hiyo nzuri, ambayo ni mwanzo wa kuhakikisha kwamba mafuta yamo mikononi mwetu? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwanza tunapokea pongezi zake kwa wizara. Pili ni sahihi kwamba wizara yangu katika utaratibu wa kikao chetu kilichopita, tuliahidi kuwa tutafanya kila jitihada

kuleta mbele ya Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar Sera ya Nishati ya Zanzibar, kwa ajili ya kujadiliwa kwa kina na hatiyame kupata baraka za Baraza hili la wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, lengo, dhamira na adhma ipo pale pale na sera hiyo italetwa kwenye Baraza hili tukufu *(Makofi)*.

Lakini kwanza nichukue nafasi hii adhimu, Mhe. Spika kupitia kwako kuwapongeza sana wajumbe wa baraza hili tukufu wa pande zote mbili. Kwa maana ndani ya historia ya visiwa vyetu hivi vya siasa za vyama vingi kwa mara ya mwanzo pande hizi mbili zilikaa kitako na kusaidia katika kuandaa sera hiyo ya Nishati ya Zanzibar bila ya kujali itikazi za kisiasa, lakini kuweka mbele maslahi ya Zanzibar na wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, hiyo ni dhahiri kwamba tunapotaka basi tunaweza kukaa kwa pamoja na kuweka mbele zaidi maslahi ya Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika utaratibu wa kuelekea kuileta sera hiyo hapa bahati mbaya vikao vinavyofuata baada ya pale ndio kidogo vilichelewesha. Lakini hatimaye wiki iliyopita wizara yangu imeweza kuwasilisha sera hiyo Baraza la Mapinduzi, mategemeo yetu ni kwamba itajadiliwa huko na hatimaye pengine kikao kinachofuata Mwenyezi Mungu akipenda tutaileta barazani *(Makofi)*.

Mhe. Haji Omar Kheir: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari katika hatua ya wataalam imeshaandaa sera na hivi sasa inasubiri kujadiliwa kwenye Baraza la Mapinduzi.

(a) Je, ni utaratibu gani wa Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi waliouweka au wanajiandaa vipi katika kuwapeleka vijana wetu kujifunza namna ya utekelezaji wa shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi asilia utakapokamilika?

(b) Wizara au serikali kwa jumla haioni kwamba kuna haja kwa kuwa jambo hili litaisaidia Zanzibar kiuchumi pamoja na maendeleo ya ustawi wa jamii kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa nini serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi haipeleki ujumbe wa kiserikali, kwa ajili ya kujifunza katika nchi ambazo zimeshafanya kazi hii ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia? *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, napenda kwa furaha kabisa kulijuilisha Baraza lako hili tukufu kwamba yale tuliyoagizwa na wajumbe wa baraza hili la kuwa *proactive*, kwa maana ya kuendelea na taratibu za kuiandaa nchi yetu katika suala zima hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta tunaendelea nalo.

Vile vile napenda kusema kwamba tulizungumza na wahisani wawili na mmoja kwa bahati nzuri sana wiki iliyopita ametuandikia barua rasmi ya kukubali kuwasomesha wazanzibari, ili tujiandae na sekta hii ya utafutaji wa uchimbaji wa mafuta *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa vile tulikubaliana labda niwakumbushe waheshimiwa wajumbe kwa zile fani ambazo tunayo dhamira ya kupeleka vijana wetu kama hivi ifuatavyo:-

1. Degree ya Mwanzo Uhandisi Mafuta na Gesi;
2. Degree ya Mwanzo Ukemia Mafuta na Gesi;
3. Degree ya Mwanzo Fizikia ya Mafuta na Gesi;
4. Degree ya Mwanzo Ukaguzi wa Mafuta na Gesi;
5. Degree ya Mwanzo Geologia kwa maana ya *BAC* Geology;
6. Degree ya Pili Uhandisi wa Matufa na Gesi;
7. Degree ya Pili ya Ukemia wa Mafuta na Gesi;
8. Degree ya Pili Geologia ya Mafuta na Gesi;
9. Degree ya Pili Uhandisi wa Maendeleo ya Nishati;
10. Degree ya Pili ya Utawala wa Rasilimali Watu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kuna mambo mawili ambayo yanaendana na shughuli hii. Kwanza tulikubaliana kwamba yoyote atayetusaidia hatutokuwa na masharti, yaani tusikubali masharti ya aina yoyote kama mtakumbuka hivyo ndivyo mlivyoagiza wajumbe wa baraza hili tukufu na ndivyo serikali ilivyoniagiza kusimamia. Kwa hivyo, huyo ambaye atakayetaka kutusaidia basi asiwe na masharti. Pili, pasiwe na mtu wa tatu kati.

Hivi sasa tayari tumeshapokea barua hiyo rasmi ya kutusaidia, lakini kwanza tunataka kujiridhisha kwamba, Je? ametufahamu vizuri na wala hakuna mitego kati. Pili, Je? hakuna mkono wa mtu wa tatu. Kwa hivyo, tukiridhika na hayo basi serikali pia imeniagiza nishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwachagua Wazanzibari hao baada ya kuandaa hadudi za rejea pamoja na viwango vinavyohitajika.

Vile vile kwa kuwa suala hili tumekubaliana, jambo hili tulifanye kwa uwazi na kushirikiana sote. Mhe. Spika, nawahakikishia wajumbe wa baraza lako hili tukufu kwamba barua yangu hiyo kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya

Amali na *copy* ataipata, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wa Kambi ya Upinzani, ili sote tuelewe nini kinachohitajika na kujihakikishia kwamba tunapata wazanzibari wenye sifa sio wazanzibari wanakotoka na pasiwe na maneno maneno kati. Haja yetu ni Wazanzibari wenye sifa ili waje waitumikie nchi yao, sio kujali anapotoka ilimradi awe na sifa.

Mhe. Spika, ujumbe wa kiserikali kwenda kujifunza tayari kazi hiyo Mheshimiwa inafanywa ,wameshakwenda baadhi ya viongozi wa wizara yangu katika nchi moja ya falme za Kiarabu, sitoitaja hii nchi , naomba tuendelee kuihifadhi. Pia wamekubali kuchukua wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda huko wakati wowote. Tunasubiri tumalize kazi na utaratibu wa kupitisha sera yetu ya nishati na hatimae tushirikiane na serikali kuona tutatumia utaratibu upi ili wajumbe watakaokuja kusimamia hatma ya nchi yetu kwenye suala hili na wao kupata angalau *orientation* ya shughuli hizi, mafunzo na kadhalika.

Pia napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu na Wazanzibari wote kwa jumla kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitogeuka ng'ombe kutilia ulimi puani. Msimamo juu ya suala hili la mafuta na gesi asilia umeshatoka wajibu wetu ni kuusimamia. Ninawaomba Wajumbe wa Baraza hili tukufu tuwe na umoja na mshikamano ili tuweze kulisimamia ipasavyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, ahsante kwa mara ya kwanza nataka niungane na Mhe. Waziri katika suala hili la mafuta na gesi jinsi namna ambavyo amejibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mwakilishi.

Mhe. Spika, wasi wasi wetu mkubwa katika mafunzo yote yanayotolewa kumekuwa na namna ya kuwapata watu wazalendo, wenye sifa lakini kwa kigezo fulani tu wakaekwa kando. Naomba Mheshimiwa aniambie katika mchakato ambao ameutaja wa kutafuta Wazanzibari wazalendo na wenye sifa na bila kujali upande anaotoka. Namuomba Mhe. Waziri anithibitishie ni vipi Baraza hili litaridhika na maamuzi ya mwisho yatakayofanywa kwa wale ambao wamekuwa ni wazalendo, Wazanzibari na wana sifa kwenda kufanya mafunzo hayo popote ambapo pataamuliwa.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nimemfahamu Mhe. Mwakilishi , naamini yeye ana niamini na kama unavyowaamini Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu juu ya utaratibu na dhamira yetu juu ya suala hili. Narejea tena kusema kwamba dhamira na lengo ni kulifanya kwa uwazi kama tunavyoendelea nalo hivi sasa na ndio maana nimewathibitishia kwamba wakati huo ukifika tukijiridhisha na huyu ambaye ameamua kutusaidia

tutamuarifu Mwenyekiti wa Kamati yetu. Tutakuarifu wewe Mhe. Spika, pia tutamuarifu na yeye ili aelewe kina nani wanahitajika, na wanahitajika kuwa na sifa zipi na tunategemea kwamba tutashirikiana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba tunapata Wazanzibari wenye sifa.

Hatutaki kuona tunachagua watu wapi wanapotoka, sisi haja yetu ni Mzanzibari ambaye atakuja kuitumikia nchi yake. Aidha iwe anatoka Pemba, anatoka Unguja na kama anatoka Unguja Chukwani haya, ilimradi awe Mzanzibari. Napenda kulithibitishia Baraza lako hili tukufu ikiwa Mzanzibari mimi ni muumini wa hilo lazima awe Mzanzibari anapotoka ni mtu majaaliwa ya Mwenyezi Mungu nchi hii ni yetu sote, Waunguja, Wapemba, Watumbatu na wengineo ni wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 30

Ujenzi wa Nyumba za Madaktari

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza**:-**

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kujenga nyumba za Madaktari katika maeneo mbali mbali katika Kisiwa cha Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapunguzia shida madaktari wetu kwenda na kurudi katika vituo vyao vya kazi lakini pia watapata kusaidia kutoa huduma masaa 24 pale mgonjwa anapotokea kwa wakati hasa vijijini.

(a) Je, Mhe. Waziri, nyumba hizi zilizojengwa katika maeneo mbali mbali za madaktari ni za familia ngapi?.

(b) Je, Mhe. Waziri, mradi wa ujenzi wa nyumba za madaktari umegharimiwa na serikali peke yake au pia na wadau wa maendeleo?.

(c) Ni lini nyumba hizo wataanza kukabidhiwa madaktari hao?.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vifungu vya (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inajenga nyumba 40 na kila nyumba itakuwa na familia mbili , nyumba hizo zitajengwa katika maeneo yafuatayo:-

Unguja:

1. Bambi
2. Kiboje
3. Ndijani kwa Baniani
4. Uzi
5. Uzini
6. Bumbwini
7. Donge
8. Kombeni
9. Matemwe
10. Mahonda
11. Kidoti
12. Kibuteni
13. Ukongoroni
14. Mfenesini
15. Kombeni
16. Bwejuu
17. Kitogani
18. Kizimbani
19. Tumbatu Jongowe

.

Pemba:

1. Bogoa
2. Fundo
3. Junguni Mtambwe
4. Kangagani
5. Kengeja
6. Kiuyu Mbuyuni Muwambe
7. Kiuyu Kipangani
8. Kisiwa panza
9. Konde
10. Mgelema
11. Ziwani
12. Makoongwe
13. Makongeni
14. Mtangani
15. Pujini
16. Shamiani
17. Tundauwa
18. Ukunjwi
19. Wambaa
20. Wingwi

b) Mhe. Spika, mradi wa ujenzi wa nyumba za madaktari umegharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia mkopo wa Benki ya maendeleo ya Afrika (*ADB*).

c) Mhe. Spika, nyumba hizo zitaanza kukabidhiwa madaktari baada ya kumalizika ujenzi kuanzia mwezi wa Agosti, 2010.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi nikauliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Kituo cha Afya Tunguu kuna mtu amejitolea amejenga nyumba ya daktari.

a) Kwa kuwa nyumba hiyo imekamilika miezi sita sasa,na hivi sasa imefungwa na Mkuu wa Mkoa ameshaiandikia Wizara ili watie *furniture* iweze kufunguliwa. Na hadi leo Wizara haijatia *furniture* hizo. Je, ni lini wizara itatia *furniture* ili nyumba hiyo iweze kutumika?

b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni kuchelewa kutumika kwa nyumba hiyo kwamba inachafuka?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, suala mama ni nyumba zilizojenga na *ADB* 40 na suala hili la nyongeza ni nyumba ya Tunguu iliyojengwa na mwananchi nyumba ya daktari, Mhe. Mkuu wa Mkoa yeye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali katika Mkoa wake inapaswa anifuate ili tujadili masuala haya matatu kwa pamoja ili tufanikishe nyumba hii kufunguliwa kwa pamoja mimi na yeye sio kuniletea barua tu. Afuatilie kwa sababu yeye mwenyewe ni Mhe. Mkuu wa Mkoa pia ni sehemu ya Serikali. Pia kuhusu hizo *furniture* ni kwamba tutashirikiana mimi na yeye na tutahakikisha kwamba nyumba hiyo haikaliwi na mashetani.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda nimuulize Mhe. Waziri kwamba ametueleza kuwa nyumba hizi zitakabidhiwa kwa madaktari mwezi wa nane.

a) Kwanza hizi zilizokwisha maliza zitakuwa na shughuli gani?

b) Ni kwamba kuna kitengo chochote katika Wizara ambacho kitakuwa na dhamana ya kuziangalia nyumba hizi wakati wote baada ya kukabidhiwa madaktari?

c) Je?, anatuhakikishia kwamba wale wanaohusika tu , ndio watakaopewa nyumba hizi, na siku moja haitaangukia miongoni mwa mtu mwengine ambaye hahusiki?.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni kwamba mkataba tuliokubaliana na mkandarasi ni kwamba azimalize nyumba zote 40 kwa Unguja 20 na Pemba 20 tukabidhiwe mwezi wa *August* , 2010. Zikimalizika hata kesho akitukabidhi tutazipokea. Hivyo ndivyo unavyosema mkataba wetu kama anataka kukaa nazo mpaka mwezi huo pia itabidi sisi kwa mujibu wa

mkataba huo tuongojee atukabidhi wakati huo. Lakini akitukabidhi kesho sisi tutazipokea.

Mhe. Spika, dhamana wa nyumba hizo ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ndio itapaswa kuziangalia nyumba hizi namna gani wazifanyie matengenezo na kuzisimamia kikamilifu.

Kuhusu wahusika watakaopewa ni madaktari na tutahakikisha kwamba nyumba hizo wanapewa madaktari, lengo la mradi huu ni kupunguza vifo vya mama na mtoto. Daktari anatakiwa akae pale pale ili mama mjamzito akija aweze kuhudumia pale pale na kuzalishwa. Hilo ndio lengo la mradi huo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi nikiwa shahidi katika ujenzi wa nyumba hizo nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii ni kweli nyumba hizo zimefika hatua nzuri za Unguja na Pemba ikiwemo ile ya Matemwe. Lakini Mheshimiwa, mimi hoja yangu ni kwamba kwa uzoefu madaktari bigwa huwa hawapendi kukaa vijijini hata uwajengee nyumba. Sasa nia ya serikali ni nzuri na nia ya mfadhili ni nzuri kwa sababu ya kupunguza vifo vya mama na watoto.

Je?, huu msimamo wa Serikali kwa madaktari ambao watakwenda kinyume na adhma ya Serikali watachukuliwa hatua gani ili kuonesha kwamba vile Serikali ilivyolenga kuweka madaktari.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kuhusu madaktari kwamba hawapendi kwenda vijijini ni kwamba inategemea namna alivyozungumza daktari bigwa kwamba ni madaktari *specialist* wanaofanya kazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwenye nyumba hizi watakaa wakunga kwa madhumuni ya kuzalisha. Napenda kumuhakikishia kwamba mara tu zikimalizika tutawaweka wauguzi ambao watakaoweza kusimamia suala la kuwazalisha mama wajawazito.

Nam. 16

Wizara ya Kilimo Kushirikishwa katika Kuvisaidia Vikundi vya Ushirika (*SACCOS*)

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, inavisaidia Vikundi vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Katika kufanikisha suala hili, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Amali imeishirikisha Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar.

(a) Kwa kuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupitia Idara ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, ndio Taasisi hasa yenye mamlaka ya kushughulikia Vikundi vya Ushirika Zanzibar kwa mujibu wa Sheria Nambari 4 ya Mwaka 1986. Je, Mhe. Waziri ni sababu gani zilizopelekea Wizara yako kutokuishirikisha kikamilifu Wizara hii katika kuvisaidia Vikundi vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*).

(b) Ijapokuwa Wizara zote zipo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi na wananchi wake.Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kutokushirikishwa Wataalamu wa mambo ya ushirika, yaani kutoka Idara ya Vyama vya Ushirika kunaweza kupelekea vikundi hivi kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.16 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu kupitia mradi wa Elimu Mbadala na Amali imeshirikisha Idara ya Vyama vya Ushirika katika mradi huu wa mkopo kwa wajasiri amali kwa kupata michango yao. Kama vile kuvitambua Vikundi vya Ushirika vya kuweka na kukopa vilivyosajiliwa, kushirikisha katika semina zilizoandaliwa kwa ajili ya vikundi vya ushirika vya kukopa na kuweka na pia kuazima wataalamu wa Idara hiyo ambayo hivi sasa wanafanya kazi katika mradi huu.

Aidha, mradi huu unashirikiana na kitengo kinachosimamia shuguli za mikopo inayotolewa kupitia Mfuko wa Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Kikwete. Ushirikiano huu umesaidia katika kubadilishana uzoefu kuhusu utoaji wa mikopo kwa Vikundi vya Ushirika. Changamoto zilizopo na kuelewa vikundi vilivyokopa kupitia mfuko mengine.

b) Kama nilivyotangulia kusema wataalamu wa Idara ya Vyama vya Ushirika wameshirikishwa na hivi sasa wataalamu wawili wameazimwa kutoka Idara ya Vyama vya Ushirika kwenda kwenye kitengo cha utekelezaji wa mradi kwa muda wa mwaka mmoja.

Wizara yangu inaamini vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa vinavyopewa mkopo kupitia mradi huu vitaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa kutokana na maandalizi mazuri yaliyofanywa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wananchi wetu wengi hususan katika vikundi vya ushirika hutegemea mikopo hii kwa kuendesha maisha yao na kujikwamua kiuchumi. Lakini kwa bahati katika mfumo huu uliokuwepo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na tumeelezwa kwamba kuna vikundi mbali mbali ambapo hupatikana mikopo hiyo.

Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kutueleza ni mafanikio gani yaliyopatikana kwa watu binafsi na kwa vikundi mbali mbali katika nchi yetu na anaweza kututajia vikundi gani ambavyo vimefaidika ili na sisi tuweze kuelekea upande wake yeye.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mafanikio makubwa yamepatikana katika mradi huu kwa vikundi mbali mbali kuweza kukopa na kuweza kurejesha mikopo ambayo wameweza kukopa.

Mhe. Spika, naamini kwamba mikopo hiyo ambayo wamechukua vikundi hivi basi wamekuwa wakifanyia kazi na ndio maana wameweza kurejesha mikopo hiyo. Pia kuna vikundi mbali mbali ambavyo tayari vimeshafanikiwa kupata mikopo hii na ushahidi ni kwamba juzi wakati Mhe. Rais anafungua vyuo vya Amali kuna vikundi mbali mbali vilikabidhiwa hundi kwa ajili mradi huu wa kuweka na kukopa.

Nam. 17

Mtaala wa Kufundisha Kutumika Sawa Baina ya Skuli za Serikali na Binafsi

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ipo katika mchakato wa kubadilisha Mtaala (*Curriculum*) wa Elimu Zanzibar na kwa kuwa mtaala huo unakusudia kuanza kutumika mapema mwakani.

(a) Je, Mhe. Waziri mabadiliko hayo yatatumika kwa Skuli zetu zote za Zanzibar (skuli za Serikali na watu binafsi).

(b) Kama hautotumika kwa skuli zote, ni lini serikali itaandaa utaratibu wa kutumika mtaala mmoja kwa skuli zote, ili kuwawezesha

wanafunzi wa skuli za watu binafsi kupata elimu kulingana na mataala wa skuli za Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.17 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya mabadiliko ya Mtaala wa Elimu ya Msingi na Mtaala huo unatarajiwa kuanza kutumika kwa darasa la kwanza kuanzia mwaka wa masomo wa 2010.

(a) Mtaala huo unakusudiwa kutumika kwa skuli zote za Serikali na za binafsi.

(b) Kama nilivyotangulia kusema, mtaala huo utatumika kwa skuli zote za Serikali na za binafsi. Hata hivyo, skuli za binafsi zinaruhusika kuongeza baadhi ya mambo katika mtaala huo pindipo kama watapenda na baada ya kupeleka maombi kwa wizara na kukubaliwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ubadilishaji wa mitaala unakusudiwa kuleta ufanisi katika taaluma na kuweza kutoa taaluma nzuri zaidi.

Je, katika kuleta ufanisi huo na kubadilisha mitaala huko Wizara imechukua hatua gani kuzidisha samani katika maskuli ambayo hakuna na pia kupeleka zana za maabara ambazo zana hizo hakuna.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Elimu katika kubadilisha mitaala unakusudia kuongeza ufanisi wa ufundishaji na kufaulu katika madarasa yetu haya.

Mhe. Spika, hatua ambazo zimechukuliwa katika kuongeza samani moja ni kwamba kila pahali ambapo panajengwa skuli sasa hivi tunahakikisha kwamba tunaweka samani katika madarasa hayo. Yeye atakuwa ni shahidi katika skuli ambazo zimejengwa hivi karibuni. Skuli hizo zote zinakuwa na samani ndani yake.

Pia tunakusudia kuweka kifungu maalum kwa ajili ya kununu samani za madarasa. Vile vile kuna miradi mbali mbali kwa mfano mradi wa Marekani sasa hivi wamekubali kutusaidia katika kuweka samani katika madarasa.

Mhe. Spika, kuhusu maabara tunajitahidi kuzihimiza skuli zetu kwamba kila wanapojenga basi kuwe na chumba cha maabara ambacho kitasaidia, na hivi karibuni tayari tenda ya vifaa vya maabara tayari imeshapelekwa na hivi karibuni tunatarajia kupata vifaa hivyo vya maabara.

Nam. 3

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza**:-**

Huduma za usafiri wa anga zinaendelea kukuwa kila siku katika nchi yetu na hili huchangia sana kuimarika kwa biashara ya utalii nchini kwetu inayotarajiwa kuwanufaisha wananchi wote wa Zanzibar.

(a) Kwa kuzingatia ukweli kwamba kiwanja chetu hakitoshi kwa huduma hii. Je, Wizara imefikiria kutenga eneo jengine kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Zanzibar?

(b) Kwa kuzingatia ukweli kwamba, kiwanja chetu kimezungukwa na nyumba za makaazi ya wananchi. Je, Ujenzi wa kiwanja chengine utazingatia haja ya kukilinda kisivamiwe na wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 3 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa, Wizara yangu iliwasilisha Serikalini Mpango Mkuu wa Usafiri hapa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Usafiri ya Zanzibar sambamba na utekelezaji wa "*Zanzibar Airport Master Plan"* ya Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar ambao pamoja na mambo mengine unahusisha suala zima la biashara katika Kiwanja cha Ndege na matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kuimarisha huduma ziliopo katika kiwanja cha ndege pamoja na kuanzisha vyengine vipya kama vile majengo ya abiria. Utaratibu huu wa kukiendeleza kiwanja kiliopo ni nafuu sana na wenye ufanisi ndani yake na ndio unaotumiwa takribani na viwanja vya ndege duniani kote.

Kutokana na udogo wa nchi yetu, pamoja na gharama kubwa za ujenzi wa uwanja mpya na kwa vile Zanzibar inavyo viwanja viwili, hivi sasa Serikali imeweka nguvu zake katika kuviimarisha viwanja hivyo kwa kuongeza

miundombinu ili kutoa huduma bora kwa wateja kulingana na matarajio ya ongezeko la wateja.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

(a) Kulingana na maelezo niliyoyatoa hapo awali ni dhahiri kuwa kiwanja kimoja kiliopo kinatosha kabisa katika kutoa huduma ya usafiri wa anga kulingana na mahitaji ya nchi yetu na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

(b) Kwa vile bado serikali haina nia ya kujenga kiwanja kipya cha ndege, mkazo zaidi umewekwa katika kuvilinda viwanja vyetu viwili cha Kimataifa kilichopo Unguja na kile cha Karume Airport kilichopo Pemba kwa kuvijengea uzio ili visivamiwe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kadri siku zinavyokwenda huduma mbali mbali za maisha zinaongezeka katika nchi yetu na hivi sasa tunasema kwamba tunaelekea katika utalii ambao ni nyanja moja wapo ya kuhakikisha kwamba mtalii anasafiri kwa urahisi anakotoka au anapopenda kwenda. Kwa mfano, tunachukulia ukanda wetu wa mashariki ni kwamba sehemu kubwa imo katika mazingira ya biashara ya utalii, na kuna baadhi ya wageni hupendelea kusafiri kwa njia za anga au barabara.

Je, hivyo Serikali au Wizara haioni pana haja kwamba kwa kuwa tuna wawekezaji ambao wako tayari kujenga viwanja vidogo vidogo baadhi ya maeneo hayo niliyoyataja, hivyo Wizara ina mpango gani wa kuzungumza wafanyabiashara hawa ili kuweka viwanja vidogo vidogo kwa ajili ya chata na ndege nyengine ambazo zinastahiki na wageni hao?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar ni visiwa ambavyo sio vikubwa sana na kwa bahati nzuri tunavyo viwanja viwili vya ndege, kiwanja cha kimataifa cha Zanzibar na Karume Airport Pemba kama alivyosema Naibu Waziri. Kuhusu hili ombi la kwamba wawekezaji waruhusiwe kuwa na viwanja vidogo vya ndege sisi kama Serikali tunaona kwamba ni jambo la kuzungumzwa katika maeneo, lakini bado tunahisi sio vizuri kuruhusu watu wenye uwezo kuwa na kiwanja cha ndege kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanahitajika kulindwa kutokana na taratibu za nchi.

Kwa hivyo, kama kuna muekezaji akitaka kuweka hivyo kwanza aje tuzungumze na tumpe masharti yetu, kama itawezekana basi ataweza

kuruhusiwa lakini lazima tuwe waangalifu katika suala hili kwa sababu umbali mkubwa kwa Zanzibar nafikiri ni kilomita 45 au 60. Kwa hivyo, kuwa na viwanja vingi inawezekana kukawa na mambo mengine yakaingia nchini bila ya serikali kuwa na taarifa zake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Spika, kwanza kuna msemo wa Kiswahili unasema "Mngoja maiti hungoja na kilio". Mimi napenda nimuulize Mhe. Waziri kwamba wakati kiwanja cha ndege hiki cha kimataifa cha Zanzibar kinangojea matengenezo haoni kwamba kuna haja ya kutengeneza mule ndani angalau spika ikasema. Wale abiria wanaoondoka wakajua sasa ndege inaondoka badala ya kukaa mtu mlangoni na kufumbua mdomo akasema kwenye *Gate No. 3* wapite abiria.

(b) Kuna huduma nyingi pale katika kiwanja cha ndege cha Zanzibar hazipatikani hasa pengine kwa hiyo biashara nzito ambayo sasa tunataka ikue ya utalii. Je, katika kipindi hiki wizara hii inashirikiana vipi na Wizara hiyo husika ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kuona kwamba huduma hizo zinapatikana wakati na hicho kiwanja kinafanyiwa matengenezo.

(c) Nilikuwa sitaki kuuliza swali hili, lakini kutokana na marekebisho yaliyofanywa na muulizaji swali naomba na mimi niulize swali. Kwa sababu ilikuwa swali linauliza kwamba kiwanja kimoja, lakini muuliza swali alisema lirekebishwe liseme kiwanja chetu. Sasa na mimi naulizia kiwanja chetu lini kitapata taa kule *Karume Airport?*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, sasa hivi sio kama tunangojea ujenzi, hivi sasa tuna ujenzi wa *run way* katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar na kazi imeanza inafanywa na Kampuni ya *SOGEASOTO* ya Ufaransa. Tunatarajia mpaka *July* mwakani Mwenyezi Mungu akipenda penye uhai na uzima itakuwa tayari. Tunaendelea na mazungumzo na *World Bank* ili tukubaliane tufanye pale na *tax way* na *apron* pia watusaidie. Lakini kwa upande wa pili tuna mazungumzo na China ya kujenga jengo jipya la abiria. Nafikiri mazungumzo yamefikia hatua nzuri tunatarajia Mwenyezi Mungu atatujaalia tufanikiwe ili tuweze kwenda mbele.

Sasa tukifikia hatua hiyo tukiweza kupata mambo hayo, Mhe. Rashid Seif na Waheshimiwa wengine nafikiri tutakuwa tena hatuna kukaa mlango pale na

kusubiri kuambiwa kwamba upite geti nambari ngapi, kutakuwa na mambo mazuri kabisa na huduma zitakuwa nzuri. Hata hizi hutubainishia kwamba pengine Waziri wa Biashara huduma gani anazozitaka pale. Lakini tunavyotaka kwenda kwamba serikali itoe huduma pale lakini pia tuwe na watu binafsi wanatoa huduma katika viwanja vya ndege. Kwa sababu kuna mambo mengi ambayo sio kazi za Serikali kuyafanya katika viwanja hivyo, lakini watu binafsi wanaweza wakafanya kwa faida ya watalii, Serikali na wananchi wa Zanzibar.

Kuhusu kiwanja chetu cha Karume Pemba, chetu sote kama vile cha Zanzibar, viwanja vyetu, basi tunaendelea na mazungumzo kama tulivyokwambieni katika bajeti tunazungumza na *ADB* kuweka taa na mambo mengine katika uwanja ule ukiwemo uzio. Lakini kwa uzio tumekubaliana tukichelewa tutaanza kutumia fedha za SMZ kuanza kujenga uzio kwa kiwanja cha ndege cha Pemba ili kuweka usalama kwa sababu hatutaki katika kiwanja chetu kuweza kupita punda, ng'ombe na mbwa; pale tunataka patumike kwa shughuli zilizokusudiwa.

Kwa hivyo, Mhe. Rashid Seif usiwe na wasi wasi, lakini pia hapo nyuma tulikuwa na mazungumzo na *Saud Fund* kulikuwa kuna pesa zetu kama dola laki tatu zimebakia kwa ajili ya kule Pemba kwenye kiwanja chetu. Sasa mimi nafikiri Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi viwanja vyote tunataka viwe vya kimataifa na tuna malengo mpaka 2015. Sasa hivi uwezo wetu wa kupokea abiria kwa mwaka kama laki tano lakini tunataka twende mpaka milioni mbili katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020. Kwa hivyo, nafikiri tutakuwa na wageni wengi .Tunataka wawe wengi kuliko wenyeji wa Zanzibar wanaoingia kwa mwaka.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nilipokuwa katika kamati tulitembelea Uwanja wa Ndege wa Dar es salaam, tukazungumza na kuulizia kiwanja kile ukubwa wake ule kinatua ndege ngapi kubwa za aina ya *Boing* kwa muda wa saa? Tukapata ufumbuzi kwamba zinatua ndege nane, kurusha pamoja na ku-*pack*.

Je, katika uwanja wetu wa Zanzibar kwa kuwa sasa hivi umo ndani ya matengenezo ya njia za kurukia na matanuzi mbali mbali, baada ya kwishakufanikiwa matengenezo hayo Mhe. Waziri anategemea zitatua ndege ngapi kubwa na ku-*pack* kwenye uwanja huo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema sasa hivi tunapata abiria kama laki tano kwa wastani wa ndege kubwa nane mpaka kumi na moja kwa wiki. Kwa hivyo, tunatarajia tukienda huko mbele tukiwa na uwanja mzuri, majengo ya kisasa na mashirika mapya ya ndege yatakuja kuleta ndege zao kwa sababu wapo wengine bado wanahitaji

kuleta ndege. Kwa hivyo, tunatarajia kuwa na ndege nyingi tu ambazo zitaletwa hapa na abiria watakuwa wengi, tutakuwa na ndege kubwa za kisasa na za kileo kabisa.

Nam. 15

Mishahara ya Wafanyakazi wa SMZ Kupokelewa Benki

Mhe. Ame Ussi Juma - Aliuliza:-

Takriban mwaka sasa, kumekuwa na utaratibu wa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapokelea mishahara yao Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*).

(a) Je, utaratibu huu una malengo gani na utazihusisha Wizara na Mashirika yote ya Serikali?

(b) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba, hali hii inapelekea kuwapo kwa msongamano wa watu katika Benki hii hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi wetu?

(c) Kwa kuwa wananchi na wafanayakazi hawa huwepo kwa wingi kabla ya kufunguliwa kwa Benki, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba, utaratibu wa kupokelea mshahara Benki, haujaandaliwa ipasavyo na ni sawa na kuanzisha jambo kabla ya kufikia muda wake?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.15 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, lengo kuu la kuanzisha utaratibu kwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupokelea mishahara yao Benki ya Watu wa Zanzibar ni kuweka utaratibu maalum na wa salama zaidi wa kulipa mishahara ya wafanyakazi, kudhibiti ubadhirifu unaoweza kutokea katika idara tofauti kupitia ulipaji wa mishahara hewa, kupunguza au kuondoa uwezekano wa wizi wa mishahara wakati wa usafirishaji wa pesa taslim, hata kupitia uvunjaji wa ofisi zetu.

Mhe. Spika, kupokelea mishahara Benki huwezesha benki kupata malipo yake moja kwa moja kutoka kwa wafanyakazi waliowakopesha.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kumekuwepo na msongamano katika matawi ya Benki ya Watu wa Zanzibar wakati wa utoaji wa huduma za kibenki hasa za mishahara. Kwa kuzingatia hali hiyo, Benki imechukua hatua mbali mbali za makusudi ikiwa ni pamoja na kurudisha huduma katika Tawi la Forodhani, kuanzisha mtandao wa *Automatic teller Machine* (*ATM*) huduma ambayo imo katika hatua za mwisho za majaribio na kuanzisha kituo cha huduma Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, lakini pia msongamano huu umekuja kwa wananchi wetu kuona umuhimu wa kupokelea mishahara yao benki na kuweka hakiba zao kwa matumizi yao y a baadae.

Katika kuhakikisha suala hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu, benki ina mpango madhubuti wa kuanzisha vituo vya huduma (*Service Centre*) katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba, ambapo kwa upande wa Unguja huduma hii inatarajiwa kupatikanwa Makunduchi na Kivunge na kwa upande wa Pemba katika maeneo ya Wete na Mkoani.

(c) Sio sahihi kuwa utaratibu wa kupitishia mishahara Benki haukuandaliwa ipasavyo. Kabla ya kuanzisha utaratibu kwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupokelea mishahara yao Benki, mpango na taratibu za msingi ziliandaliwa. Serikali pia imeanza kutumia utaratibu huu kwa majaribio kwa kuhusisha wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wapiganaji wa vikosi vya SMZ.

Lengo la majaribio haya ni kutoa fursa kwa serikali na Benki husika kutambua na kurekebisha kasoro zozote kabla ya utaratibu huu kuweza kutumika kwa wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa utaratibu huu mzuri ambao unaonesha ni usalama tosha kwa wafanyakazi ambao wanapokelea fedha zao Benki. Lakini pia Mhe. Spika, na

kuhakikisha kwamba fedha zilizokopeshwa kwa wafanyakazi hao zinapatikana pale bila ya usumbufu.

Pamoja na jibu lake alilojibu kwamba wameanzisha mpango kwenye kanda mbali mbali ili kupunguza msongamano kwa wananchi wetu. Kwa mfano, wametwambia kuna kitengo cha *ATM*, kuongeza tawi la Forodhani, lakini pia kuna kanda katika maeneo ya vijijini kama Makunduchi na Kivunge kwa watu wanaoishi katika maeneo hayo.

Mimi naomba kumuuliza je, kwa kuwa wafanyakazi wetu wanafanya kazi katika wilaya mbali mbali, tukiangalia kwamba mfano Wilaya ya Kati makao makuu yao Dunga, Wilaya ya Kaskazini 'B' Mahonda, Wilaya ya Kaskazini 'A' Mkokotoni, Wilaya ya Kusini Makunduchi, mfano tu tumechukulia. Je, haoni kama pana haja ya kuondoa kero au kuwasafirisha wananchi wetu watakaopata shida kutoka Makunduchi au wilaya nyengine mbali mbali, haoni hizi wilaya zetu zingekuwa kituo tosha cha kuhakikisha kwamba watu wa Benki wanakwenda mle kugawa pesa zile kwa urahisi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:

Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Uchumi na uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, tunapokea pongezi hizi na ni changamoto kwetu kwa hii niseme kadhia ndogo ndogo iliyotokea ambayo kama nilivyosema tutajipinda kuirekebisha.

Pili nakubaliana naye kweli Mheshimiwa kwamba wafanyakazi wetu wamesambaa katika sehemu nyingi za vijijini. Nafikiri hasa anachotaka kwamba tuongeze huduma zetu yaani ziwafuate huko waliko sio wao wazifuate Benki. Ushauri wake ni mzuri na kama nilivyosema tuna mipango ya mbali ya zile *stationary service center*s, lakini hata *mobile service centers* na magari yale mazito yatawafuata wale kwa siku maalum ili kurahisisha huo utaratibu. Isiwe mtu siku ya mshahara haonekani kazini, anakwenda mara moja anamfuata anapata pesa zake anaendelea na kazi. Nafikiri ushauri wake tumeusikia na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kulipoanzishwa utaratibu huu ni kudhibiti upotevu wa pesa hasa kupitia wafanyakazi hewa. Tangu mwaka huo tulipata taarifa kwamba ziliwahi kugunduliwa pesa ambazo zinavuja kwa njia hiyo, lakini tangu wakati huo hatujapata taarifa kwamba suala hili bado linaendelea la wafanyakazi hewa au haliendelei?

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atatwambiaje kwa hili, linaendelea au limesita kutokana na utaratibu huu mzuri wa kupitia mishahara Benki. Kama linaendelea kwa vile wahasibu wote wako chini ya Wizara ya Fedha haoni kwamba wafanyakazi wake hawafanyi kazi kwa uaminifu?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakiri kwamba kweli hapo nyuma tulikuwa na tatizo hili sugu la upotevu wa fedha kutokana na wafanyakazi hewa. Lakini kadiri tulivyorekebisha ufanisi wetu na hasa baada ya ku-*introduce* huu utaratibu wa mashine ile ambayo tumeiweka hapa Unguja na kule Pemba (*pay center*), *terminology* yake kidogo imenitoka, *voucher* zote zinapita pale.

Mheshimiwa kumradhi, nasema labda nimtaje mwanao tu Mati Ame Wadi yuko Mkwajuni anafanya kazi basi na mimi mwanangu labda niseme Makame Mwinyihaji basi tutamuona pale, hata awe anafanya kazi wapi lakini zamani tulikuwa hatuna utaratibu huo. Sasa imekuwa rahisi siku hizi kuweza kuona kila mfanyakazi, hata ile *voucher* inapopigwa basi inaangaliwa pale. Kwa hivyo, kwa kweli mapungufu haya ya zamani sasa kwa kiwango kikubwa yamepungua sana baada ya kuanzisha hii *Central Pay Main Center*.

Kama nilivyosema tulianza na Unguja na sasa tumeshafungua Pemba. Kwa hivyo,. Mambo yanakwenda sambamba.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Benki ni ile ile *BPZ* ukienda kuchukua pesa Darajani na *account* yako iko kule Mwanakwerekwe unaambiwa lazima urudi kule Mwanakwerekwe kwenda kuchukua pesa. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba tunawasumbua wateja na kuwahangaisha wakati compyuta ni zile zile na *account* inaonekana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na manung'uniko hayo na kwa kweli ni usumbufu. Kwa sababu kama mfano uko kwenye mtandao wa *NBC* na una kadi yao unaweza kupokelea popote, nafikiri hilo ndio lengo letu na sisi tunaendea huko. Lakini kwa sasa unajua haya mambo ya kompyuta ndio kwanza yanaanza kwenye Benki yetu na sisi tuna lengo hilo hilo kwamba ukishakuwa na kadi yako basi unaweza kwenda kwenye *ATM* popote lakini uweze kwenda kwenye Benki yoyote.

Vile vile tulikuwa na mpango na sisi *CRDB* uweze hata kuchukua kwenye *ATM* zao. Kwa hivyo, fikra yake ni nzuri na kwa kweli huko ndiko tunakoelekea. Ahsante.

Mhe. Spika: Kabla ya kuendelea kuna taarifa mbili. Taarifa ya kwanza ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe mara baada ya kumaliza kutoa hizi taarifa mbili tunategemea kumwita Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji ili kufanya majumuisho na *quorum* yangu ina matatizo humu ndani. Kwa hivyo, niwaombe tuliomo tubaki isipokuwa labda kwa dharura ambayo haiepukiki na tulio nje turudi ili kuimaliza kazi hii na kuendelea na shughuli nyengine tukihakikisha kwamba tuna *quorum* ya kutosha.

Lakini jambo la pili ni kwamba tulikubaliana katika vikao vyetu vya *briefing* kwamba wenzetu mashirika ya simu wale wanaosajili simu tuwaite hapa na kuanzia jana kama taarifa ilivyotolewa kabla walikuwepo, lakini ombi letu la kuwaita hapa naona halikufanya kazi ya kutosha, naambiwa ni waheshimiwa wawili tu waliokwenda kujisajili.

Kwa hivyo, tunaambiwa kwamba ndugu zetu wa *Zantel* wapo wanawasubiri Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wafanyakazi ambao bado hawajasajili simu zao, basi waende wakafanye shughuli hiyo kwa kuwa tuliwaita kwa ajili ya kuturahisishia usajili kwa upande wetu waheshimiwa pamoja na wafanyakazi wa ofisi yetu. Wapo katika eneo la maktaba wanafanya kazi hiyo ya usajili kwa siku. Nawashukuru waheshimiwa wajumbe.

Shughuli za Serikali

Mswada wa Sheria ya Utalii ya Zanzibar 2009

Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kama kawaida yako kuendesha vyema Baraza hili wakati wote wa mjadala wa Mswada wa Sheria mpya ya Utalii. Pamoja na shukurani hizo naomba vile vile nichukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Baraza hili kwa kuujadili mswada huu kwa ufanisi pamoja na kutaka ufafanuzi wa baadhi ya hoja. Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, maoni na mapendekezo yao waliyoyatoa tutayafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inahusisha sekta nyengine nyingi kama ardhi, umeme, maji, ujenzi, usalama wa nchi, usafi, ukusanyaji mapato, miundombinu na mengine kama hayo. Haya yote hutekelezwa na sekta husika na sio sekta ya utalii. Naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri walioko

katika sekta hizo na zilizochangiwa katika mswada huu, kuchukua jitihada ili tutengeneze mazingira mazuri kwa utalii.

Kwa mantiki hiyo, Waheshimiwa Wajumbe walijadili Mswada wa Sheria ya Utalii kwa mapana yake, hivyo basi, naomba uniruhusu nifafanue zile hoja zitokanazo na mswada huu na zile zinazohusiana nazo.

Mhe. Spika, mswada ulichangiwa na wajumbe 16 kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi)
2. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin (Waziri Kivuli Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji)
3. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
4. Mhe. Haji Mkema Haji
5. Mhe. Ali Abdalla Ali
6. Mhe. Abass Juma Muhunzi
7. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
8. Mhe. Ali Denge Makame
9. Mhe. Ali Suleiman Ali
10. Mhe. Ame Mati Wadi
11. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
12. Mhe. Rashid Seif Suleiman
13. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
14. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi

Aidha, Mhe. Spika, Wajumbe wawili Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba na Mhe. Asha Moh'd Hilal walichangia kwa maandishi.

Mhe. Spika: Samahani, umemsahau Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Spika, kweli na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, naomba radhi kwa kumsahau.

Mhe. Spika, kuna hoja nyingi zilizotolewa, lakini kama nilivyosema nataka niguse zile ambazo zilitokana na mswada ule na zinazohusiana nazo. Hoja ya kwanza iliyozungumzwa na wajumbe wengi ilikuwa ni hoja ya leseni, wajumbe walikuwa wana wasi wasi kwamba kutakuwa kuna urasimu lakini pia mzozo utakaotokana na taasisi nyengine ambazo nazo pia zinatoa leseni.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kwa sasa hivi ndani ya Kamisheni tumepunguza kwa kiasi kikubwa urasimu wa kutoa leseni. Ni kweli naomba nikiri huko nyuma kulikuwa na urasimu na mizengwe mingi, lakini sasa hivi tumeupunguza kwa kiasi kikubwa. Ndio maana tukaona haja pia ya kufanya marekebisho ndani ya sheria.

Suala la mzozo na taasisi nyengine, kulitoka mapendekezo hapa kwamba tufanye kazi vizuri katika kanuni na tuoneshe maeneo gani Kamisheni ya Utalii itatoa leseni na maeneo gani yatahusika na taasisi nyengine. Hilo tunalifanyia kazi pamoja na mradi ulioko Wizarani wa leseni zote kwa ujumla zinazotolewa Zanzibar. Kwa hivyo, hili tunalifanyia kazi.

Aidha, kulitoka hoja kutoka kwa Mhe. Waziri Kivuli kwamba katika kifungu cha 16(1)(a) kinasema kwamba ‘mtu hatapatiwa leseni mpaka atoe michango’. Naomba waheshimiwa wafanye marekebisho kwenye neno ‘michango’ waandike ‘ada’, hapa ilikusudiwa ni *license fee* na sio mchango kama *contribution.* Kwa hivyo, iandikwe ada badala ya mchango.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala pia kuhusu *package tour* na ninaomba nitoe ufafanuzi kwamba *package tour* katika miaka sita iliyopita ilikuwa iko katika kiwango cha asilimia 85. Lakini sasa hivi tumeweza kuipunguza mpaka asilimia 60. Hata hivyo, Kamisheni ya Utalii au tunakubali kupokea watalii wa aina zote, wa *package tours* na wale wanaokuja mmoja mmoja. Faida ya utalii huu wa *package tours* ni kwamba hawa wanatoka moja kwa moja wanakotoka mpaka Zanzibar na hivyo kuikuza Zanzibar kama *destination*, kama pahali pa mwanzo pa kufikia. Hapo pana mapato ya aina yake ambayo yanapatikana, sasa mtalii mmoja mmoja haji Zanzibar moja kwa moja kwanza anapitia labda Kilimanjaro anashuka kule, anakwenda kwenye mbuga anamaliza ndio anakuja Zanzibar, au anateremka Nairobi halafu ana-*conect* anakuja Zanzibar. Kwa hivyo, kuna aina fulani ya mapato yanakuwa yameshapungua kwa kiasi.

Kwa hivyo, kwa sasa hivi tunashughulika na yote ingawa tunajitahidi kupunguza. Lakini katika hapa kuna kitu ambacho kitatufanya kwa muda mrefu tuendelee kuwa na *package tours* kwa sababu nchi zote ambazo wana mashirika yao ya ndege ya nchi haya wanakwenda wenyewe katika *source* za kuchukua watalii katika masoko na kuwaleta nchini. Sisi ambao hatuna Shirika la Ndege la kufanya hivyo, bado tutategemea ndege za mataifa mengine kuleta watalii. Kwa hivyo, kwa urahisi kama nchi inakuwa ina watalii wengi kwa mfano sasa hivi tumefungua soko la Urusi.

Mhe. Spika, soko la Urusi tutapata watalii wengi watakaokuja kuanzia Disemba mwaka huu, lakini tukitegemea mtalii mmoja mmoja itakuwa tabu kupata watalii wengi. Kwa hivyo, badala yake kutakuwa kuna mpango ule ule wa

chata ambazo zitatoka Urusi moja moja kwa na kufika Zanzibar. Kwa maana hiyo wale ni *package* moja ingawa wizara au kamisheni tunafanyia kazi pia ya kuona tunafaidika kwa kiasi kikubwa katika mapato kwa mtindo huo. Zamani walikuwa wanalipa kila kitu wanakotoka lakini sasa hivi tunajitahidi kuvuta ili pato katika ujaji kama huu liweze kuongezeka ndani ya nchi.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja katika kifungu cha 27(4) kinachohusu wawekezaji kusaidia maendeleo ya vijiji. Hoja ya kwanza ilikuwa ni kwamba kungewekwa kiwango kitakachosema mwekezaji aliyepo kijijini atachangia kiwango kadhaa, lakini hoja ya pili kama kikiwekwa nani atasimamia utekelezaji huo?

Mhe. Spika, ufafanuzi ni kwamba wakati tunatunga sheria hii mpya hatukuona haja ya kuweka kiwango kwa sababu, katika sheria ya kodi ndani ya *ZRB* kuna kipengele kinachotoa mvuto kwa wawekezaji kusema kwamba wawekezaji watapimwa kwa kiwango wanachosaidia katika maendeleo ya vijijini au maendeleo ya nchi.

Kwa hiyo, kutakuwa kuna kiwango cha kusamehewa kodi kulingana na *percentage* unayoitoa katika maendeleo ya nchi. Kwa kupitia kule tumeweza kuwabana na kuweka kipengele ambacho kitawafanya wawekezaji wachangie zaidi ili waweze kupata misamaha zaidi. Kuliko tukisema labda asilimia 5 ya mtaji uliouweka ndio utaupeleka katika maendeleo tunawa-*limit* kutoa zaidi na zaidi. Sheria inasema mwekezaji atatakiwa kuchangia katika maendeleo ya nchi lakini kiwango itategemeana na *incentive* iliyowekwa katika sheria ya kodi.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala la tafsiri ya utalii na kwamba je, waheshimiwa nao ni watalii. Kwa bahati nzuri umeijibu vizuri sana kwamba waheshimiwa wanaotoka Pemba kuja hapa ni watalii na wanaotoka hapa kwenda Pemba ni watalii, lakini ni watalii wa ndani.

Niseme tu kwamba tafsiri za utalii ziko nyingi. Labda tukichukua Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani wana tafsiri yao, *ILO* wana tafsiri yao, nchi mbali mbali zina tafsiri yao. Kwa hiyo na sisi kwetu tuliona hii ni s*tandard definition* ya neno utalii.

Kifungu cha 4 (1) (a) kuna vifungu vinatoka (a) mpaka (t) kuna swali je, kifungu cha 2 kiko wapi na kinasemaje. Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wafanye marekebisho na yalikwishafanywa na kamati kuondosha ile *bracket* moja. Kwa hiyo, iwe kifungu cha 4 chenye (a) mpaka (t) na ile *bracket* moja iondoke.

Kulikuwa kuna hoja pia kwamba idara za ndani ya kamisheni hazikutajwa, wamesema tu kutakuwa na idara ndani ya kamisheni. Hii tuliiacha makusudi kwa sababu kama nilivyosema kwamba sekta ya utalii inabadilika kila mara, kwa hiyo kila mara kunakuwa kuna mabadiliko katika uendeshaji wake, idara zitaundwa kutokana na mahitaji ya wakati. Lakini tungesema hapa kutakuwa na idara 3 au 4 ina maana tusingeweza kuunda idara nyengine hata kama haja itatokea. Tuliiacha makusudi kuweka idara zipi na zipi kwa sababu sekta inakwenda na mabadiliko ya wakati.

Hii vile vile naomba niiunganishe na lile suala la kusema kwamba mwenyekiti hakuwekewa sifa. Tulishindwa kuweka sifa za mwenyekiti kwa sababu mwenyekiti nae pia anawekwa kutokana na mahitaji ya wakati. Wakati tunatengeneza sera hii tumetazama sera mbali mbali duniani na tukaona kwamba mwenyekiti anawekwa kutokana na mahitaji ya wakati.

Kwa mfano, wenzetu Tanzania Bara kuna kipindi kulikuwa katika *National Parks* kuna uvamizi kutoka nchi jirani wanavamia wanapiga wanyama na wanawachukua. Kwa wakati ule kulionekana haja ya kumuweka Mwenyekiti wa Bodi ya *National Parks* kuwa Generali wa Jeshi Mstaafu. Alipowekwa alichukua hatua zake kule na yale mambo yalipotea kabisa.

Lakini katika Bodi ya *TTB* wakati wa kubadilika kwa *crisis* ya kiuchumi wameweka mwenyekiti ambaye ni mchumi na angeweza kuendana na yale mambo ya sasa hivi. Kwa hiyo, hatuwezi ku-*fix* sifa za mwenyekiti ndani ya sheria kwa sababu tutakuwa tumebanwa, hatutakuwa *dynamic*. Ile mambo ya kubadilika *now and then* yatakuwa hayapo hatutokwenda na ule wakati.

Mhe. Spika, kulikuwa pia na hoja katika ukurasa wa 47 kifungu cha 28 kinachozungumzia kuweka kumbukumbu na ripoti zitakazotakiwa katika biashara ya utalii. Swali je, katika makosa na adhabu haikuwekwa hii atapewa adhabu gani akishindwa kufanya hivyo.

Lakini hii naomba niseme kwamba inakuwa *covered* na kifungu cha 28 (b), (c) na (d), vyote vinamuingiza huyu ambaye atashindwa kutoa taarifa sahihi kwa Afisa Utalii atakayemtembelea na kutaka kupata taarifa. Wakishindwa kutoa taarifa hizi vifungu vya (b), (c) na (d) vinamuweka katika makosa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna maoni kwamba sheria hii haikukamilika kwa vile hakuna kifungu kizuri kinachozungumzia mazingira ingawa kipo. Lakini pia walitaka wale ambao watafanya matatizo ya kujenga kinyume na sheria za mazingira au kinyume na maagizo adhabu zao zionekane humu. Nasema kwamba hayo yanaonekana katika sheria husika za ujenzi na ardhi.

Halafu pia kulikuwa na hoja ya kumpa Mkurugenzi Mkuu uwezo wa kumaliza makosa. Je, huku si kushawishi mazingira ya rushwa. Tunasema kwamba hii si kushawishi mazingira ya rushwa bali ni kuharakisha kuondosha makosa na kutoa adhabu kwa haraka haraka. Kwa sababu tunaposema Mkurugenzi Mkuu sio mtu ila ni ofisi yake. Kwa hiyo, kutakuwa na utaratibu mzima ndani ya kanuni unaoelezea jinsi ya kuendesha kesi hizi. Hizi ni kesi ndogo ndogo labda mtu amechelewa kukata leseni au makosa kama hayo, yatamalizwa ndani ili kuepuka urasimu wa Mahakamani.

Mhe. Spika, kulikuwa pia kuna matakwa ya kutaka Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ijitahidi katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya mapato yale. Niseme tu kwamba hizi ni sera za fedha na uchumi na zitashughulikiwa ndani ya Wizara husika ya Fedha na Uchumi. Kazi ya wizara yangu ni kuitengeneza tu ile pesa ikae hapo na wengine wanapita kuikusanya na kuipangia matumizi yake.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja pia ya askari wa utalii. Nitoe ufafanuzi tu kwamba tunapozungumza askari wa utalii wala hatukusudii askari makoti au wenye sare, vifirimbi na silaha. Kulikuwa kuna hoja hapa kwamba muwapatie silaha nzito kwa sababu majambazi wanakuja. Hawa ni maafisa wa utalii ambao kutakuwa na kitengo maalum, kazi zao ni kupitia katika maeneo ya utalii na kuangalia viashiria vya hatari zinazotaka kutokea katika maeneo yale na baadae kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kurekebisha hatari zile ambazo zinaonekana. Askari hawa hawatakuwa na uwezo wa kukamata wala kushtaki, kazi yao ni kuangalia viashiria na kuripoti polisi, wao na Jeshi la Polisi watafanya kazi hiyo kwa pamoja.

Nitoe taarifa tu kwamba tumekuwa tukitoa mafunzo baina ya askari wa polisi na hawa maafisa wetu jinsi watakavyoweza kufanya kazi kwa pamoja. Pengine baadae huko kuna mambo ya vitendea ambayo watakuwa wana-*share*. Kwa hiyo, hawa si askari makoti bali ni maafisa tu wa utalii ambao watakuwa wanazunguka *(patrol)* kuangalia viashiria vya hatari.

Mhe. Spika, kulikuwa pia na suala la maduka ya utalii kuwekwa karibu na watalii na kuyaondosha kule ambako mapapasi wanafanya fujo kwa watalii. Niseme tu kwamba hizi ni kazi za halmashauri za maeneo husika. Tutakapotakiwa sisi Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji tutatoa msaada tuchangie ili mambo haya yaende vizuri.

Kama mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe tulijitahidi sana kujenga soko la Mchekeni kipandoni na tukakabidhi kwa halmashauri ya kule Kaskazini “B” waendeshe soko lile. Lakini kwa sababu walishindwa kazi waliwaachia mapapasi wakenda wakatia moto na lile soko haliko mpaka leo. Kwa hiyo,

kama halmashauri wataona kuna haja hiyo wizara tuko tayari kutoa msaada unaotakiwa.

Hapa niunganishe na uuzaji wa vinyago. Mhe. Spika, uuzaji wa vinyago hatuupendelei sana lakini hatuwezi kupiga marufuku kabisa. Tunaweza kupiga marufuku watu kutoka nje na kuja kuuza vinyago Zanzibar, hilo tumelipigia marufuku mpaka ndani ya sheria. Lakini biashara yenyewe ya kuuza vinyago tunaifumbia macho kwa sababu kama nilivyosema kuna watalii wanaotoka kwao *destination* ni Zanzibar, wanakuja Zanzibar na wanaondokea Zanzibar. Kwa hiyo, kinyago kile akikinunua Zanzibar desturi ya wazungu anakitia alama kabisa anaweka kikaratasi Zanzibar, ingawa sio *product* yetu lakini ni biashara ambayo itawapa watu wetu uwezo wa kutengeneza fedha na kujikimu katika maisha yao. Kwa hiyo, kama biashara hatuwezi kupiga marufuku, lakini kuja watu wa nje wakafanya biashara hii tumeshazuia kisheria.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la kuhifadhi misitu katika maeneo na kukuza misitu yenyewe kama moja ya kutengeneza mazingira na kuleta hali ya hewa nzuri nchini kwa ajili ya watalii na kwamba mbona Tumbatu wameweza kwa nini wasiwe wengine. Mimi pia ningependa kumuuliza Mhe. Mwakilishi aliyelisema hilo kama Tumbatu wameweza na wana sheria, kwa nini sisi wawakilishi tusisimamie maeneo yetu tukaweka sheria za aina hii. Najua pia kwamba kuna maeneo mengine sheria za aina hii zipo na ni wakali kwa maeneo yao ya misitu na hata ya baharini. Kwa hiyo, ndugu zangu waheshimiwa tujitahidi maeneo yetu nayo yaweze kuhifadhi mazingira ipasavyo.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala pia la watembeza wageni kupewa mafunzo na unadhifu wao. Mhe. Spika, watembeza wageni *(tour guides)* tumekuwa tukiwapa mafunzo mbali mbali. Tulikuwa tumeanza na kozi ndogo ndogo lakini tukasema haitoshi tukaenda kozi za miezi mitatu mpaka miezi sita, lakini sasa hivi tuna kozi ya mwaka mzima ndio *tour guide* aweze kupata cheti. Tumeweka hivi makusudi kwa sababu akimaliza mwaka mmoja tunampa cheti, tunampa na leseni ya kufanyia ile kazi, lengo ni kuondosha yale ambayo sasa hivi yanatokea. Unadhifu utapatikana pale baada ya *tour guide* kutoka kwenye mafunzo yale. Tutamfunza unadhifu, historia ya Zanzibar na jinsi ya kujieleza kwa mgeni. Kwa hiyo, hili sheria ina makusudi ya kurekebisha hizi kasoro zilizopo sasa hivi.

Kulikuwa kuna suala pia kwamba je, kamisheni ina muundo wake kama ulivyoundwa hivi mmeiga mfano wa nchi gani. Je, wataweza kufanya kazi wenyewe nje kama kamisheni. Niseme ndio wataweza. Kama nilivyosema kabla wakati tunatayarisha sheria hii tulichukua sheria kama sita za nchi mbali mbali kupitia mitandao na tukaangalia yale mazuri ya sheria zile

tukayatengeneza kwa mazingira ya kwetu na tukaweka. Kwa hiyo, kamisheni imefuata mtindo huo.

Lakini pia hata sasa hivi kamisheni wanaweza kufanya kazi wenyewe nje bila ya kupitia popote. Kama nilivyosema kamisheni pamoja na wizara tumeweza kwenda nje kuzunguka nchi nyingi kufanya kazi zetu, kufanya semina na waandishi wa habari na *tour operators* na sasa hivi tumeanza kuona matunda. Kwa hiyo, kamisheni ina uwezo huo wa kufanya kazi.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja kwamba maeneo ya wenyeji Bwejuu, Paje, Jambiani yanauzwa kwa wingi na wenyeji wanasogea maweni. Mimi ningeomba Waheshimiwa Wawakilishi tukasaidiana na wananchi kuwaelewesha kwamba maeneo ya Bwejuu, Paje, Jambiani katika masterplan ya utalii yaliwekwa kwamba ni maeneo ya wawekezaji wenyeji. Ni kweli kwamba wawekezaji wenyeji waliwekeza kwa wingi katika maeneo yale. Kinachotokea sasa hivi mtu anakuja kuji-*register* kama mwekezaji mwenyeji, akishakupata mambo yote yanayotakiwa kutoka *ZIPA* anageuka anatafuta mgeni anamuuzia na yeye anabakia na asilimia ndogo. Baada ya miaka mitatu anaambiwa ongeza mtaji tuongeze biashara na kama huna nikurudishie *share* yako uliyokuwanayo mimi niendelee na biashara.

Sasa tumekuwa tukiwaambia wawekezaji wenyeji linapotokea hilo tafadhalini mripoti *ZIPA* ili hatua za haraka zichukuliwe na mlindiwe haki zenu. Lakini ni kweli kwamba kuna wenyeji wanawasaidia wageni kuingia nchini katika maeneo ambayo hayahitajiki.

Hata kufanya biashara ambazo hazihitajiki. Kuna kesi nimeipata karibuni mwenyeji kashirikiana na wageni ambao walikuja kama wafanyakazi, baadae wamefanya kazi wamekusanya pesa zao wametaka sasa kununua sehemu ya mwenyeji ambaye wao waendelee na biashara na wasihame Zanzibar. Ni mwenyeji ndie aliyekinga kifua akenda Uhamiaji, akenda ZIPA, akenda kila pahali kudai kwamba ile biashara ni yake, baadae wamemgeuka wamemzika sasa amekuja anatoa siri mambo yalivyokuwa.

Kwa hiyo, naomba tusaidiane katika hili kuwaelewesha watu wetu. Hawa watu wetu hawarudishwi maweni, wanajirudisha maweni. Naomba tusaidiane kulisimamia hilo.

Kuna suala la wawekezaji kupewa maeneo makubwa. Nasema hili kuna kamati kubwa ya kiufundi *(technical committee)* ambayo inaangalia aina ya mradi na eneo ambalo linatakiwa kupewa.

Kuna hoja imetoka kwamba ukienda Kempinski kibanda kimoja kiko kule, kibanda kimoja hicho huko. Hizi ndizo hoteli za daraja la kwanza zinavyotakiwa ziwe. Hatuwezi kujenga hoteli za daraja la kwanza tukafanya kama vibanda vya kwetu pale Kwahani, ukipigwa kofi paa, nyumba ya pili kasikia Samia kapigwa kofi hivyo jana kwa sababu vibanda vimeshikana shikana. Kwa hiyo, maeneo makubwa yanaendana na ukubwa wa mradi na haja ya mradi ule ndivyo unavyotoka.

Halafu kulikuwa kuna hoja kwamba *ZIPA* wanachukua maeneo kwa nguvu. Mhe. Spika, nataka niseme si kweli kwa sababu *ZIPA* hawana sheria inayowapa kugawa maeneo wala kutoa ardhi. Hii ni kazi ya ardhi lakini kama nilivyosema kuna *technical committee* inakaa na kuona eneo gani litolewe.

Kuna ubishi kwamba wakati eneo limeshatolewa mambo yote yameshakamilika bado wenyeji wanang'ang'ania kukaa kwenye eneo lile. Sasa kinachotokea huko mbele sikielewi lakini si *ZIPA* inayochukua maeneo kwa nguvu kwa sababu *ZIPA* hawana uwezo wowote wa kuingia katika ugawaji wa ardhi.

Kulikuwa kuna hoja ya wenye magari kufanya fujo kwa hiyo kamisheni ijitahidi waunde umoja wao na kamisheni iwarekebishe ipasavyo. Kama nilivyosema Mhe. Spika, sekta ya utalii ina nyanja nyingi, sasa ushirika wa magari na kamisheni aaa hii si kazi yao, lakini tunachokifanya kila gari linalochukua watalii kwa kawaida linakata kibali kamisheni kwa siku ile. Tunachukua namba ya gari, jina la dereva na ametoka ushirika gani. Kwa hiyo, lolote linalotokea tunajua moja kwa moja tunakwenda kwenye ushirika tunaweka namba ya gari na jina la dereva. Kama mtalii aliibiwa, alipigwa, alimuacha wapi, alikuwa wapi, mambo kama hayo.

Kwa hiyo, mimi nadhani tayari hawa madereva wana ushirika wao huko, lakini na sisi kupitia kamisheni tuna mtiririko wetu wa kujua nani, amechukua mtalii yupi.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala la Mjumbe wa Bodi kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Niseme tu kwamba hili tulilifanyia marekebisho toka ndani ya kamati na tulikubaliana kuondosha Mjumbe wa Bodi kutoka Afya. Tuiache tu kwamba wajumbe wawili watatoka *private sector* na wawili watatoka *public sector*. Kwa hiyo, ile specifical ya mjumbe kutoka Afya tumeiondosha kwa sababu kama nilivyosema utalii unabadilika, haja ya kuwa na wajumbe kutoka hapa, kutoka pale inabadilika kutoka muda mpaka muda.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la vyombo vya baharini. Je, vile vinavyoegeshwa Forodhani na ngalawa za Uroa pia zinaingia. Nasema kwamba

sheria hii ina makusudi ya kurekebisha hayo yanayotokea sasa hivi. Ngalawa ya ubavu mmoja inachukua mtalii, nani anaendesha mtalii. Vyombo tele pale Forodhani vinapeleka watalii kwenye makobe. Kwa hiyo, nia ya kuweka kifungu kile ni kurekebisha yale kwa ajili ya usalama wa wageni ambao tunawapokea.

Halafu pia kulikuwa na haja ya kubadilisha jina kwamba wanabadilisha tu majina au wanabadilisha mradi na kwamba tunakosa mapato. Mhe. Spika, niseme kwamba wakati mradi unabadilisha jina lazima anayebadilisha jina wakae pamoja na Kamisheni ya Ardhi na Mrajis wa Makampuni kama mradi umepitishwa na kamisheni. Kama mradi umepitishwa na *ZIPA* basi wanakaa Kamisheni ya Ardhi, Mrajis na *ZIPA* kujadili kwa nini mradi ubadilishwe jina na kusema sawa au si sawa. Kwa hiyo, yote yanatazamwa.

Kama mradi unahaulishwa au kuuzwa, mradi unatoka kwa mmiliki mmoja unakwenda kwa mmiliki mwengine, basi kuna kamati inaitwa *land transfer committee* (kamati ya uhaulishaji) inakaa na kujadili kwa nini mradi ule unahaulishwa, halafu kutoa ruhusa au kunyima ruhusa.

Kulikuwa na suala la *retention* kwamba haikuonekana. Nataka niseme kwamba *retention* ipo kwa sababu tukiangalia katika vifungu vya vyanzo vya mapato tulisema kule nyuma kwamba kamisheni ilikuwa inafanya kazi zake kama idara ya kawaida ya serikali. Lakini sasa hivi inakuwa mamlaka inayojitegemea kama sheria hii itapita. Kwa hiyo, kama mamlaka inayojitegemea tumeweka kabisa vyanzo vyake vya mapato vitatokana na yafuatayo. Kwa hiyo, vyote vile vine vilivyowekwa vitabakia ndani ya kamisheni. Hiyo ndio *retention* ya mfumo mpya wa kamisheni.

Kulikuwa na hoja kwamba kwa nini kuwe na *parks* ziweke wanyama kama ngamia, ndovu, chui na wengine wakati sisi hatuna asili ya wanyama wale. Mhe. Spika, watalii sio wazungu peke yao, lakini watalii pia wenyeji wa Zanzibar wanaweza kwenda kwenye *parks* wakiwa kama watalii. Watoto wetu wanaona simba na wanyama wengineo kwenye vitabu na kwenye TV. Kwa hiyo, ni vizuri kama kuna mwekezaji ataweka wanyama na mtoto wetu atakwenda kumwona simba ndio huyu hapa, wale wote watakuwa hawana uwezo wa kwenda huko kwenye *National Parks* kama Ngorongoro, Manyara na kwengine kwenda kutazama simba, ndovu na wanyama kama hao.

Kwa hiyo, kama kunakuwa na wawekezaji wanajitolea kuweka wanyama hao sisi tunawakaribisha kwa ajili ya elimu ya watoto wetu lakini pia na watu wetu humu ndani.

Kuna suala la vituo vya kuogelea, kuna mchangiaji alisema mimi sivifahamu hata vilipo. Sasa hapa naomba Waheshimiwa Wajumbe tufanye marekebisho, badala ya vituo vya kuogeela tuseme vituo vya kuzamia. Hapa tumekusudia *diving centers* ambazo ziko Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja kwamba sheria haikuangalia wafanyakazi wa mahotelini. Kama nilivyosema mwanzo utalii una sekta nyingi wafanyakazi wa mahotelini watatazamwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Halafu ujenzi wa mita 30 kutoka ufukweni. Mhe. Spika, mheshimiwa aliyelichangia hili wizara yake ndio iliyoweka hii kwamba sheria ya ujenzi katika mahoteli ya utalii au biashara yoyote ambayo itawekwa ufukweni ni mita 30 kutoka ufukweni kuingia ndani ujenzi uanze kule. Sasa kama kuna fikra mbadala tunaomba wizara inayohusika ikae waijadili fikra hii na sisi kama wadau tuwepo katika mjadala huo.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nyingi zilizofafanuliwa vizuri kabisa na Mhe. Abass Juma Muhunzi zinazotokana na mswada huu. Niseme kwamba yote aliyoyajadili tumeyatazama tena kwa undani tunakubaliana nae na tutafanya marekebisho yanayopaswa kufanywa.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala la kutangaza utalii. Kuna hoja kwamba hakuna msukumo wa kutosha na wanaokwenda ni viongozi wa juu tu wa kamisheni pamoja na wizara. Lakini pia hapa niunganishe na lile lililosema kwamba ndani ya wizara pia kuna nani, katoka wapi na ndivyo kazi zinavyoendeshwa.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba mpaka miaka miwili iliyopita na huko nyuma kote zoezi la kwenda maonesho lilikuwa linamhusisha kila mtu. Mimi nilikuwa nashangazwa watu wananiaga kwenda maonesho nikitazama list kuna Afisa Leseni anakwenda maonesho, kuna Mwangalizi wa Afisi na Afisa Uhusiano ndani ya wizara anakwenda maonesho, yaani ilikuwa kama kila mmoja aweze kutoka nje ya nchi akatembee arudi. Kwa kweli utaratibu ule nimeurekebisha mimi baada ya kuingia na miaka miwili nyuma ndipo nimeanza kurekebisha.

Kwa sababu sikuwa naona tija inayoletwa na mtindo ule. Lengo la pesa zile zilizowekwa kwa *marketing* si kufanya watu wakatembee, lengo ni kwamba watu waende wakafanye kazi na matunda yaonekane. Kwa hiyo, nikachukua hatua za kurekebisha utaratibu ule na sasa ni maofisa wanaoshughulikia *marketing* ya utalii ndio wanaokwenda na wala sio mmoja wapo wengi tu, huku anakwenda huyu, kule anakwenda huyu. Lakini Mkurugenzi anayehusika na utangazaji wa utalii lazima aende kote.

Kuna sehemu ambazo tunaangalia labda safari hii inataka *political push* na ndipo waziri ninapoingia, nakwenda nafanya *political push*, natoa *political statement* na watalii wanaridhika wanakuja. Katika mtindo huu tumeweza kufungua masoko mapya, lakini kule nyuma hatukuwa tumefungua masoko mapya, tulikuwa tunakwenda uzoefu tu kila mtu aende akaone nje. Kwa hiyo, si ubaguzi ila ni mpangilio wa kazi na kuona matunda ya kazi hii yanapatikana.

Lakini jengine ni kwamba ndani ya wizara yangu jamani, hii wizara mimi naweza nikaiita *mosaic*. Kwa sababu nikianza na wizarani waziri ni Mkizimkazi mimi, lakini Katibu Mkuu Mpemba, Naibu Katibu Mkuu Mmakonde mwenye asili ya Pemba, Mkurugenzi Mipango Mmakunduchi, Mkurugenzi Biashara Mpemba, Mkurugenzi Viwanda simjui kwao yule mtoto lakini mshamba wa Unguja. Tukienda Kamisheni Mwenyekiti Mpemba, Mkurugenzi Mkuu anayekaimu sasa hivi Bahran sijui kabila gani Mwarabu yule pale. Halafu tukienda chini kuna Mkurugenzi mmoja mshamba mtoto wa kike Ashura, halafu mwengine Mpemba. Sasa katika hii ukinambia kwamba wizara inafanya kazi kuwa huyu katoka wapi mimi sielewi si kweli, wala maamuzi yetu hatuyatoi kwa aina hiyo.

Kwa hiyo, katika wizara inayojitahidi kutokuangalia hilo katika utendaji wake ni hili kwa sababu utalii ni wa kila mtu wala hauna upande mmoja. Mhe. Spika, shutuma hizi pamoja na kwamba nitapenda sana nikae na Mhe. Mwakilishi *chamber* tujadili hili nipate undani wake lakini nalikanusha hapa kwamba sio kweli.

Mhe. Spika, utalii wa daraja la kwanza na miundo mbinu. Kama nilivyosema watalii wa daraja la kwanza tunao tunawapokea na kama mjumbe mmoja alivyosema kwamba serikali inajitahidi sasa kutengeneza miundo mbinu ili waweze kuja zaidi na zaidi.

Ongezeko la lugha katika maeneo yetu ni kweli watoto wetu wanasema sana Kitaliana, Kipotugizi na Kispaniola. Tuna jitihada za makusudi kupitia chuo kufundisha lugha ya Kirusi kwa sababu tumeshaona watapata watalii wengi wa Kirusi kuja huku, lakini pia Kiingereza na lugha nyengine.

Kulikuwa kuna suala la biashara ndogo ndogo matunda na mboga mboga kwamba hawaachiwi Wazanzibari. Hata zile zilizosemwa za magari ya taka na magari ya kubeba wafanyakazi kwenda na kurudi kwamba zinapewa watu wengine na sio Wazanzibari.

Mhe. Spika, mtu anayefanya biashara yake hasa ya chakula anataka *constant supply* ya kile chakula. Wazanzibari *from time to time* wamekuwa wanakuja wanatuomba tuwatafutie masoko mahotelini, tunawa-*connect* na masoko ya

mahoteli. Lakini ukimalizika msimu mmoja hana cha ku-*supply* na yule mtu mwenye hoteli anataka *supply* iwe ya moja kwa moja. Hivi sasa nina mtu nimem-*connect* hoteli ya Neptune kupeleka mayai. Pale Neptune wanataka *stock* ya wiki mbili, yeye anapeleka *tray* 30 za mayai. Wamenirudia wananambia mbona mheshimiwa *supplier* wako hafanyi vizuri. Nikamwita nikamwambia kwa maana hiyo wewe tafuta wazalishaji wengine wadogo wadogo waku-*supply* wewe, halafu wewe upeleke kule.

Kwa hiyo, tatizo kubwa linalotokea hapa jamani ni wingi wa ile bidhaa inayotakiwa kule, sisi tukishavuna msimu moja hatuna tena. Pengine hata huo msimu mmoja hatutimizi ile *turn age* inayotakiwa kule. Lakini kama wako wanaozalisha kwa wingi na wamenyimwa masoko waje wizarani tutawasaidia. Tumesema soko la utalii lililopo litumike kwa Wazanzibar na sheria mpya ndivyo inavyosema. Kwa hivyo, kama wapo wamekwama na hawapokewi na huduma yake itahakikisha kwamba haitakatika sisi tutamuunganisha.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengine watu wamepewa fursa za kutoa magari au huduma hizo za kuzoa taka, lakini kuna wajanja wanatokea maeneo yale yale wanachukua huduma ile na kuiuza kwa watu wengine. Lakini lawama zinapokuja Waziri Kiongozi akitembea, lawama kwa wizara hatusaidiwi serikali. Lakini wananchi wanazipoteza nafasi wanazopewa, na sisi kama wizara hatuna uwezo wa kila siku kutizama huyu kapewa hiki anakwenda vibaya au anakwenda vizuri.

Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe tusaidiane, sisi ndio tunaotoka huko kwenye maeneo. Kama haya yanatokea basi tusaidiane na wizara ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanafaidika na soko liliopo, wanaitumia kikamilifu fursa hii iliopo.

Mhe. Spika, kulikuwa na kutakiwa kwa ufafanuzi katika ukurasa wa 41 katika kifungu cha (3) kinachosema,

Kifungu cha 7(3)

> "Bodi inaweza wakati wowote kutengua jukumu ililoipa kamati, bila kujali kama kamati imekamilisha au haijakamilisha jukumu au majukumu ambayo imepewa na bodi".

Hapa tulisema kwamba bodi itakuwa na uwezo wa kuunda kamati vikundi kazi. Kwa mfano, bodi inataka kubadilisha mfumo wa kamisheni na katika kubadilisha mfumo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naelewa kwamba mnatoka nje kwa dharura, najua hivyo. Mara baada ya dharura hiyo naamini mtarudi sasa hivi ili tumalize kazi hii.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Kwa mfano, nimesema kama bodi inataka kubadilisha mfumo wa kamisheni, katika kubadilisha mfumo ule kuna wafanyakazi ambao itabidi wabadilike katika kila sehemu ya kamisheni. Kwa hivyo, bodi itaunda kamati, kwa mfano shughulikieni hii. Lakini wakati kamati inaendelea labda kuna mabadiliko ya *policy* kutoka wizarani yanakwenda kwenye kamisheni.

Kwa hivyo, kamisheni itaripoti kwa bodi, na bodi wataitaka kamati ile isimame kwanza, acheni hiyo kazi mliyokuwa mkifanya. Sio kwa dharau bodi itawaambia wacheni hiyo kazi hatutaki kuiona, hapana. Bodi itakuwa na uwezo wa kusimamisha kazi kwa sababu maalum, sio tu kwa uamuzi wa bodi waache.

Mhe. Spika, pia kulitakiwa ufafanuzi katika kifungu cha 6(9) katika ukurasa wa 42 kuhusu *corum,* kwamba leo haikutimia utaitwa tena mkutano wakija tena wale wale mkutano utaendelea. Hili tumeliona na tutalifanyia marekebisho kama Mhe. Abass Juma Muhunzi pia alivyolijadili.

Mhe. Spika, kulikuwa na mengineyo kwa ruhusa ya Spika, ambayo yalizungumzwa hapa nayo ndio niliomba ruhusa kwamba nisiyaingie kwa sababu hayaendani na mjadala huu. Mhe. Spika, nimemaliza kutoa hoja, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati ya Baraza zima ili kuupitia mswada wa sheria mpya ya utalii kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na Kuanza Kutumika pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 2	Tafsiri pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Uanzishaji kazi na Uwezo wa Kamisheni

Kifungu 3	Kuanzishwa kwa Kamisheni na marekebisho yake
Kifungu 4	Kazi za Kamisheni na marekebisho yake
Kifungu 5	Bodi ya Wakurugenzi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hapa palikuwa na maoni yametolewa na wajumbe mbali mbali na Mhe. Waziri aliyakubali kwamba atayarekebisha, kuwa bodi ile kama ilikuwa haikutimia *corum* kwa kikao cha kwanza, kwamba siku ya pili ile kama ilivyo ndani ya mswada hivi sasa, itakapoitwa tena basi wale watakaohudhuria iwe shughuli iende.

Sasa hapa alisema kwamba patarekebishwa. Lakini hayo marekebisho hatujayaona hapa. Kwa hivyo, ilibidi tuseme hasa ni marekebisho gani, maana ndio tunakwenda kifungu baada ya kifungu hapa. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji hebu tusaidie.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, wakati tunalijadili hili na timu yangu ya wataalamu, waliniambia kwamba ilikuwa ni ufundi wa kisheria katika kuandika mambo haya, tukakubaliana kwamba tuende kama sheria nyengine zinavyoandikwa, kwamba kama bodi haikutimiza *quorum* mkutano hautakuwepo na utaitishwa mwengine siku nyengine na kuhakikisha kwamba *corum* inafikiwa ndio mkutano uende.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa. Sasa hayo ndio marekebisho, iliyobakia ni uandikaji.

Kifungu 6 Kazi za Bodi

Kifungu 7 Kamati za Bodi

Kifungu 8 Kueleza Maslahi pamoja na marekebisho yake

Kifungu 9 Mikutano ya Bodi

Kifungu 10 Kuandaa Mpango wa Kazi

Kifungu 11 Mkurugenzi Mkuu wa wafanyakazi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Fedha na Usimamizi wake

Kifungu 12 Mfuko wa Fedha za Kamisheni na marekebisho yake

Kifungu 13 Makisio

Kifungu 14 Ripoti za Mwaka

Sehemu ya Nne

Utoaji wa Leseni kwa Biashara ya Utalii

Kifungu 15 Leseni

Kifungu 16 Utoaji wa Leseni pamoja na marekebisho yake

Kifungu 17 Kutoa Upya Leseni

Sehemu ya Tano

Masharti na Wajibu wa Waendeshaji Biashara ya Utalii

Kifungu 18 Mmiliki wa Hoteli au Nyumba za wageni Kuweka Kumbukumbu na kuzitoa zikihitajika

Kifungu 19 Kutembeza Watalii

Kifungu 20 Waongoza Watalii

Kifungu 21 Vyombo vya Utalii pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 22 Maegesho ya Vyombo vya baharini pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 23 Vituo vya Kuzamia

Sehemu ya Sita

Masharti ya Jumla

Kifungu 24 Biashara Zilizotengwa kwa Watanzania

Kifungu 25 Hatua za Dharura

Kifungu 26 Uundaji wa Taasisi za Kitalii

Kifungu 27 Majukumu ya Kijamii na marekebisho yake

Kifungu 28 Makosa

Kifungu 29 Haki ya Rufaa

Kifungu 30 Kumaliza Kosa

Kifungu 31 Kanuni pamoja na marekebisho yake

Kifungu 32 Kufutwa na Kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wa Sheria Mpya ya Utalii kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali mswada huu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyuwe mikono juu. Wale wanaokataa?. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Utalii Zanzibar 2009

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Utalii ya Zanzibar ya mwaka 2009, usomwe kwa mara ya pili

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kuusoma mara ya pili wanyanyuwe mikono. Wale wanaokataa?. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mswada wa Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, 2009 na Mambo yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, pamoja na makamo wake na kamati nzima ya Fedha na Uchumi, kwa kweli tumefanya kazi ya pamoja na namshukuru sana Mhe. Burhan Saadat Haji Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira ambaye alikaa na kamati kwa kuanzia, mimi nilikuwa kidogo na dharurura katika safari za kikazi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kazi nzuri sana waliifanya ya kupitia kifungu kwa kifungu na hatimaye kuwa katika hali nzuri ya kuweza kuwasilisha vizuri na ipasavyo hapa hii leo.

Pili Mhe. Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe watakaposoma mswada huu mbali kama ulivyotolewa kwenye Gazeti rasmi la Serikali, lakini wachukuwe zile *document* walizopewa wakati wa semina, nafikiri zile zinarahisisha sana. Utaona kwamba mswada ni mkubwa na una mambo mengi lakini hautishi. Kwa sababu kama tulivyozungumza wakati wa semina, kwa kweli hatukusudii kuanzisha sheria mpya moja kwa moja, kuna marekebisho tu tunayoyafanya kutokana na sheria zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar. Sheria hizo zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar ziko saba.

1. Sheria ya *Revalue added tax* nambari 4 ya mwaka 1998.

2. *The stamp duty act* nambari 6 ya mwaka 1966.

3. *The hotel levy act* nambari 1 ya mwaka 1995.

4. *The port service charge act* nambari 2 ya mwaka 1999.

5. *The petrolium levy act* nambari 7 ya mwaka 2001

6. *Propart tax act* nambari 14 ya mwaka 2008 na

7. *The trade linces act* nambari 3 ya mwaka 1983

Mhe. Spika, ukizipitia kodi hizi utakuta kwa kweli kuna mambo yaani ndani ya sheria hizi za kodi kuna mambo yaliyojirudia rudia katika kila sheria. Katika sheria zote hizo nilizozisoma ambazo zinasimamiwa na bodi ya mapato Zanzibar, yaani ZRB zilianzisha kodi hizo nilizozisema na kuainisha mambo yafuatayo:-

1. Kiwango cha kodi husika
2. Walipa kodi husika
3. Muda wa ulipaji
4. Taratibu za usimamizi wa kodi
5. Taratibu za kukomboa kodi na makosa na adhabu

Mhe. Spika, ukiacha kiwango na mlipa kodi, mambo yote kwa kiasi kikubwa yanatakiwa na yanapaswa kulingana, lakini utakuta hayalingani na hayana mtiririko. Kwa hivyo, kutoa niseme ni usumbufu mkubwa kwa walipa kodi wetu na kufanya kidogo wababaike ni sheria gani itumike wapi na wao wanapaswa kwenda wapi.

Mhe. Spika, mambo yaliomo ndani ya sheria za kodi. Ukweli uliopo hivi sasa kama nilivyosema ni kwamba katika sheria zinazosimamiwa na bodi ya mapato

Zanzibar, mambo hayo yanatofautiana na hata kugongana kati ya sheria moja na nyengine.

Kwa mfano, kutofautiana kwa adhabu kwenye makosa yanayolingana, kutofautiana kwa taratibu za usimamizi na kugomboa kwa kodi.

Mhe. Spika, umuhimu wa kuwepo taratibu za aina moja za usimamizi wa kodi. Muhimu ni kutunga sheria itakayoweka utaratibu wa aina moja katika usimamizi wa sheria zote za kodi zinazosimamiwa na bodi ya mapato kwa sababu zifuatazo:

1. Itaimarisha usimamizi bora wa sheria za kodi
2. Itaongeza ufanisi kwa watendaji
3. Itaongeza uwajibikaji
4. Itasaidia kuimarisha mapato ya serikali na
5. Itawapunguzia walipa kodi usumbufu kama nilivyoeleza.

Mhe. Spika, madhumuni hasa na sababu ya mswada huu ni kutunga sheria itakayoweka utaratibu wa kusimamia kodi zinazokusanywa hapa Zanzibar. Mswada huu unakusudia kuwasajili walipa kodi wote ambao watasajiliwa na bodi ya mapato Zanzibar, ambapo itarahisisha kuwafahamu, kuwahakiki na kuwafuatilia walipa kodi pale itakapotokea mlipa kodi kushindwa kulipa kodi inayostahili.

Mhe. Spika, mswada wenyewe wa sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2009 una sehemu 10.
Sehemu ya Kwanza inahusiana na vifungu vya utangulizi ambavyo vinaelezea jina la sheria, utumikaji wa sheria na vifungu vya ufafanuzi wa maneno yatakayotumika katika sheria.

Sehemu ya pili Mhe. Spika, inahusiana na vifungu vinavyoeleza,

1. Sifa na taratibu za usajili wa walipa kodi
2. Usajili wa muda
3. Cheti cha usajili
4. Taratibu za kufuta usajili

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inaelezea masharti ya kupata hati ya kutokudaiwa kodi kabla ya kutolewa kwa leseni ya biashara.
Sehemu ya nne inaelezea taratibu za uwasilishaji wa fomu ya marejesho ya kodi, uwezo wa kamishna wa kufanya makisio ya kodi na taratibu za utayarishaji na uwasilishaji wa hati ya makisio ya kodi.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ya mswada huu inaelezea mambo manne,

1. Taratibu na masharti ya uwekaji wa kumbukumbu za mlipa kodi
2. Utoaji wa risiti
3. Ukaguzi na
4. Uwezo wa Kamishna wa kutaka taarifa na udhibiti wa taarifa zilizopatikana katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, sehemu ya sita inazungumzia taratibu za malipo ya kodi, muda wa malipo ya kodi na utozaji wa riba.

Sehemu ya saba Mhe. Spika, inaelezea taratibu za ugomboaji wa kodi ikiwemo;

a) Kutoka kwa mdaiwa wa mlipa kodi
b) Ulipaji wa vipindi
c) Ufungaji wa biashara na
d) Kukamata mali au bidhaa za mlipa kodi.

Sehemu ya nane Mhe. Spika, inaelezea masuala ya utawala na usimamizi wa kodi, uwezo wa kamishna kuomba taarifa, wajibu wa kutunza siri, uteuzi wa mawakala wa kuzuia kodi, taratibu za usafirishaji wa bidhaa na mwisho ni uwezo wa kuomba msaada wa polisi.

Sehemu ya tisa Mhe. Spika, inahusiana na makosa ya ujumla kama ukwepaji kodi, uwezo wa kamishna wa kusamehe adhabu na riba, uwezo wa kukasimu madaraka ya kamishna, taratibu za rufaa, utoaji wa *notice* na uwezo wa waziri wa kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya mswada huu.
Mhe. Spika, ya mwisho ni sehemu ya 10. Sehemu hii inafanya marekebisho kwenye sheria za kodi za *VAT*, kodi za mafuta, kodi za hoteli, ushuru wa stempu na ada ya bandari.

Mhe. Spika, kwa muhtasari huu ndio mtiririko wa sheria nzima hii ya bodi ya mapato ambayo tunajaribu kuileta mbele yetu kwa ajili ya kurekebishwa, kama nilivyosema kupata mtiririko mzuri na mfumo mzuri ambao utatusaidia sana katika utendaji wa kazi zetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, ifuatayo ni hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, juu ya Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa rehema zake ambazo leo tunaendelea kuzitumia tukiwa hai na wenye afya njema.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kabisa, kuweza kuchangia na kuweza kutoa maoni kwa niaba ya kamati ya fedha na uchumi, juu ya mswada wa sheria wa masharti ya usimamizi wa sheria za kodi.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi kwa kutuwasilishia mswada huu.

Aidha, wasaidizi wake, Katibu Mkuu, Manaibu pamoja na watendaji wengine wote ambao kwa njia moja ama nyengine wanachangia sana maendeleo na ufanisi wa wizara hii.

Mhe. Spika, nitakuwa sijawatendea haki hata kidogo wajumbe wenzangu wa kamati endapo sitaitumia nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Pia ni kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa na yanayoifanya kazi yangu ya kuiongoza kamati kuwa nyepesi.

Naomba niwatambue na kuwataja kama ifuatavyo:

1.	Mimi Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti,
2.	Mhe. Ali Abdallah Ali	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asaa Othman Hamad	Mjumbe
4.	Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	Mjumbe
5.	Mhe. Ashura Abeid Faraji	Mjumbe
6.	Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	Mjumbe
7.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
8.	Mhe. Said Kheleif Ali	Mjumbe
9.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	Mjumbe
10.	Ndg. Amour Mohamed Amour	Katibu na
11.	Ndg. Maryam Husein Rajab	Katibu

Mhe. Spika, nchi zote duniani zinaendesha shughuli zao za kijamii kwa kupitia malipo ya kodi ndio maana serikali imetunga sheria ya kuanzisha bodi ya mapato ya Zanzibar, sheria nambari 7 ya mwaka 1996 kama wakala wa ukusanyaji wa kodi mbali mbali, ambapo kwa mujibu wa sheria hiyo, bodi ya mapato Zanzibar imepewa jukumu la kusimamia sheria zifuatazo;

1. Sheria ya ongezeko la thamani yaani VAT nambari 4 ya mwaka 1998
2. Sheria ya kodi ya ushuru wa stempu nambari 6 ya mwaka 1996
3. Sheria ya kodi ya hoteli nambari 1 ya mwaka 1995
4. Sheria ya kodi ya huduma za bandari nambari 2 ya mwaka 1999
5. Sheria ya kodi ya mafuta nambari 7 ya mwaka 2001
6. Sheria ya kodi ya majengo nambari 14 ya mwaka 2008
7. Sheria ya leseni ya biashara nambari 3 ya mwaka 1983

Mhe. Spika, sheria zote hizo zimeainisha viwango vya kodi husika. Nani anahusika na kulipa kodi, muda wa kulipa kodi hiyo, taratibu za usimamizi wa kodi na makosa yanayotokea pamoja na adhabu za makosa hayo kwa wale wote wanaokwenda kinyume na sheria hizi.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa na sheria hizo ambazo zote zinasimamiwa na taasisi moja yaani *ZRB*, ambazo aina ya makosa yake yanalingana wakati adhabu zake zinatofautiana katika sheria nyengine. Halikadhalika taratibu za usimamizi na kugomboa nazo zikatafautiana.

Kilichotia moyo ni kwamba, ili kuondoa utata huo Sheria ya Bodi ya Rufaa na Kodi Nam. 1 ya mwaka 2006 ilitungwa, ambayo imeanzisha chombo kimoja tu cha kusikiliza mashauri yanayohusiana na kodi zote zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar kwa kutumia taratibu za aina moja.

Mhe. Spika, katika azma hiyo ya usimamizi wa kodi, serikali leo imetuwasilishia mapendekezo ya sheria inayohusiana au itakayoweka utatibu wa aina moja, katika usimamizi wa sheria zote za kodi zitakazosimamiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar.
Lengo ni kuona kwamba ufanisi wa ukusanyaji wa kodi unapatikana. Kwa maana hiyo, tutainua uchumi wetu, kwani ongezeko la mapato litachochea maendeleo ya wanajamii wetu.

Mhe. Spika, siku zote katika kuelekeza jambo au kulirahisishia utungwaji wa sheria ni hatua moja, lakini utekelezaji wake ni hatua nyengine. Nia ya kutungwa kwa sheria hii ni kudhibiti makusanyo ya kodi na katika kufanya hivyo tunatarajia sana kuwapunguzia walipa kodi usumbufu, kutokana na kufanya kwa taratibu zote za msingi za usimamizi na ugomboaji wa kodi.

Kwa kawaida hakutakiwi kutokuelewana kati ya wakusanyaji wa kodi na walipa kodi. Lakini sheria zetu zinazotungwa kwa madhumuni hayo zitakapokuwa na urasimu mkubwa na kuvifanya baadhi ya vifungu kuwa vigumu kutekelezeka au kuleta usumbufu kwa aina yoyote, basi zinaweza kuleta migogoro, ambayo hatimaye ama zitayakaribisha mazingira ya rushwa

au kuleta mapato madogo kutokana na walipa kodi wengi kukwepa kulipa kodi hiyo.

Mhe. Spika, kamati yetu ingependa na inaendelea kusisitiza kwamba wataalam wetu wajitahidi kutumia uwezo wa taaluma yao, ili waweke miundombinu mizuri yenye kuleta mvuto wenye kushajihisha malipo ya kodi kwa hiari zaidi kuliko kusukumwa na sheria pekee.

Jambo muhimu ambalo ninaweza kusaidia sana katika mambo yetu mengi ni kuwashirikisha sana wadau, yaani sekta binafsi endapo tutakuwa mara kwa mara tunawaweka karibu wadau katika kila hatua, basi hao ndio wanaoweza kutoa elimu kwa wenzao.

Mhe. Spika, tunaelewa fika katika mazingira ya ulipaji kodi kila mmoja wetu kwa njia moja au nyengine anahusika, kwa maana hiyo elimu inayohusiana na masuala hayo ni muhimu sana.

Wananchi wetu wengi wakati mwengine hawaoni umuhimu wa kulipa kodi kwa sababu ya kukosa elimu ya kutosha, wamekuwa na manung'uniko mengi kwani wanahisi kwamba mwananchi wa kawaida ndiye mlipa kodi mkubwa, wakati mwengine wanahisi wanalipa kodi zisizokuwa na kumbukumbu au wasizostahili kulipa.

Mhe. Spika, haya yanaonekana sasa kwenye sehemu ya tano ya mswada huu pamoja na taratibu zilizowekwa za uwekaji wa kumbukumbu za mlipa kodi, utoaji wa risiti, ukaguzi, uwezo wa Kamishna wa kutaka taarifa pamoja na udhibiti wa taarifa zilizopatikana katika utekelezaji wa sheria hii. Kwa kweli haya yamekuwepo na yametandikwa kwenye sheria zilizotangulia, lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu. Baadhi ya wafanyabiashara wahatoi risiti na wanunuzi nao hawana utamaduni wa kudai risiti.

Mapendekezo ya mswada yameainisha vifungu vingi vilivyompa uwezo Kamishna wa Bodi ya Mapato katika maeneo mengi na mote humo ni kuhakikisha kwamba kuna usimamizi bora wa ukusanyaji wa mapato hayo. Tunaamini kwamba hili litarahisisha zaidi kuwafahamu, kuwahakiki na kuwafuatilia walipa kodi kwa pale mlipa kodi anaposhindwa kulipa kodi inayostahili.

Mhe. Spika, misingi ya sheria ya kodi mara nyingi hufanana duniani na huwekwa katika mazingira ya kuhakikisha katika kila hali anayestahili kulipa kodi analipa. Lakini sheria hizi ni muhimu pia zikazingatia fursa ya mlipa kodi kuweza kulipa kodi anayostahili kulipa bila ya usumbufu.

Mhe. Spika, kamati inaona serikali haihakikishi kwamba tunakuwa na utekelezaji mzuri wa usimamizi wa kodi katika maeneo yote. Sheria hii iwe na nafasi kwenye sheria nyengine kama zile zinazohusiana na uwekezaji, ili nako makusanyo ya kodi yawe yanapatikana kama tulivyokusudia. Kwa hivyo, kusiwe na ujanja wa uwekaji wa kumbukumbu na taarifa zinazohusiana na mapato.

Aidha suala la umiliki na uhamishaji wa umiliki hasa katika uwekezaji wa mahoteli ya utalii nao uangaliwe vyema, ili mikataba yao isipoteze uhalali wa viwango vya malipo ya kodi.

Mhe. Spika, ni matarajio makubwa ya kamati yetu kwamba baada ya kupita sheria hii kutakuwa na matokeo mazuri ya ongezeko ya makusanyo ya kodi. Halikadhalika taarifa za matokeo hayo zitakuwa wazi kwa wananchi kupitia chombo hiki.

Kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi na wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono mswada huu na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kuujadili, kuchangia na hatimaye waupitishe, ili uwe sheria itakayompa nyenzo Mhe. Waziri pamoja na watumishi wenzake kufanyakazi hii nzuri.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny: Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kutujaalia afya na uwezo wa kuhudhuria katika kikao hiki kitukufu.

Mhe. Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mswada huu unalenga kuweka taratibu za aina moja za usimamizi wa sheria zote za kodi zinazosimamiwa na *ZRB* ambazo ni:-

1. Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998,
2. Sheria ya Kodi ya Ushuru wa Stamp Nam. 6 ya mwaka 1996,
3. Sheria ya Kodi za Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995,
4. Sheria ya Kodi ya Huduma za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999,

5. Sheria ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya mwaka 2001,
6. Sheria ya Kodi ya Kumiliki Majengo Nam. 14 ya mwaka 2008 na
7. Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983.

Mhe. Spika, ili sheria iwe ya wanaotungiwa, yaani iwe na *sense of ownership*, basi ushirikishwaji wa wadau wanaohusika ni walazima. Kambi ya Upinzani ina mashaka kama kweli serikali inakubaliana na dhana nzima ya *Public Private Partnership*.

Kwa kweli serikali haikuwashirikisha wadau mbali mbali katika hatua za awali za marayarisho ya mswada huu wa sheria. kwa hivyo, Kambi ya Upinzani inaona kutokushirikishwa kwa wadau mbali mbali kama vile *Zanzibar Chamber of Commerce, NGO's* na wengine kuanzia katika hatua za awali ya matayarisho ni mapungufu makubwa.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo tunaishauri serilkali ione umuhimu wa kushirikiana na wadau katika kila hatua, ili nao watoe maoni yao na sio kualikwa katika hatua za kuujadili mswada wenyewe.

Mfumo uliotumika katika uandishi wa sheria hii wa kuweka adhabu kwenye kila kifungu, unaonekana kuifanya sheria iwe ngumu kufahamika na pia kuwapa unyonge walipa kodi. Kambi ya Upinzani inashauri ni bora adhabu zote zingekuswanywa mwisho kwenye *schedule* na walipa kodi wangefahamu vizuri zaidi hasa ilivyokuwa adhabu na makosa yenyewe yanafanana.

Mhe. Spika, katika kifungu cha pili cha mswada wa sheria hii kinachoelezea juu ya usajili na kufuta usajili. Kambi ya Upinzanzi inaona Kamishna amepewa madaraka makubwa mno. Mfano halisi ni kwenye kifungu cha 11 (1) na (2) ambapo Kamishna atamsajili moja kwa moja mlipakodi na kuamua tarehe ambayo atatakiwa kulipa malimbikizo ya kodi, uwezo huu unaweza kutumika vibaya na kuleta usumbufu mkubwa kwa walipakodi wetu.

Kambi ya Upinzani inashauri kifungu hicho kifanyiwe marekebisho, ili kumlazimisha mlipakodi kujisajili kwa kutumia vigezo vya nyaraka zake alazimike kulipa kodi kuanzia tarehe aliyotakiwa kuwa awe amejisajili na sio Kamishna kumsajili moja kwa moja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, uwezo kama huo pia na kumuachia Kamishna uwezo mkubwa wa kuamua kama anavyoona yeye nani amsajili katika kulipa kodi gani bila ya kuwekewa vigezo, unaweza kusababisha malalamiko makubwa kwa walipakodi ambao wako kwenye sekta moja na wakiwa na biashara sawa. Kwa mfano, kwenye Biashara ya Hoteli za Kitalii wengine kutakiwa kulipa *VAT* na wengine *Hotel Levy*.

Kwa hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri Kamishna asipewe madaraka yasiyo na mipaka wala yasiyo na vigezo vilivyo wazi na vinavyoeleweka ndani ya sheria.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani haina tatizo na sheria hii kama ilivyoelezwa kwenye madhumuni yake. Kweli sio tu itarahishisha ukusanyaji wa mapato, lakini itawabana mno walipakodi katika kuwajibika.

Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kama ambavyo serikali inajirahisishia kisheria ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi, basi pia wakati umefika wa kuhakikisha kwamba nao walipakodi wanadhaminiwa na kupewa haki zao kisheria *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika mtazamo wa karne ya leo mlipakodi anapaswa kuwa ni rafiki, mshauri tena ni mbia katika maendeleo ya nchi. Kwa kweli inasikitisha kuona kwamba bado serikali yetu haijawathamini na kutambua nafasi ya walipakodi wetu pamoja na mchango mkubwa wanaotoa katika jamii yetu. Kwa sababu walipakodi wanakabiliwa na matatizo na usumbufu mkubwa katika kutekeleza shughuli zao.

Ikiwa kweli tunayo nia ya kuwapunguzia usumbufu walipakodi wetu, basi sambamba na sheria hii serikali inahitajika kuzipitia mara kwa mara sheria za kodi, ili kuondoa mapungufu yaliyomo hasa yanayowakwaza walipakodi wetu kwa ajili ya kujiona na wao wanathamani kama wachangiaji wa maendeleo na hivyo hali hiyo itawafanya wawe na ridhaa ya kulipa kodi.

Mhe. Spika, wakati tunazungumzia suala la kuweka utaratibu bora wa ulipaji kodi, ni lazima serikali ioneshe nia ya kuwaondoshea usumbufu na kuwasaidia walipakodi wetu.

Mhe. Spika, awali ya yote serikali inabidi kuliangalia kwa makini sana suala la kuwaondoshea usumbufu walipakodi wetu, kwa kulipa kodi zao kwa mamlaka mbili tofauti ambazo zipo kisheria, yaani *ZRB* na *TRA*.

Hata kama mamlaka hizo mbili zinakusanya kodi tofauti bado Kambi ya Upinzani inaishauri serikali kuijengea uwezo wa kifaa pamoja na utaalamu *ZRB*, ili iweze kuwa wakala wa kukusanya kodi za *TRA (Makofi)*.

Mhe. Spika, suala la kuwa na mamlaka moja ya ukusanyaji kodi ni muhimu, ili kuwaondoshea usumbufu walipakodi wetu kwa kupoteza muda wao mwingi, kwa ajili kushughulika na mamlaka hizo mbili.

Vile vile sio tu ni usumbufu na wakati mwengine husababisha mamlaka moja kutowaamini walipakodi wetu hasa pale wanapodaiwa *file* na likawa lipo kwenye mamlaka nyengine. Pia walipakodi wanapotezewa muda wao mwingi ambao wangeutumia katika kufanyabiashara zao kwa lengo la kuongeza mapato ya nchi pia kuwatia gharama za ziada ambazo si za lazima *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo limekuwa kikwazo kikubwa kwa walipa kodi wetu hasa wenye mitaji midogo, sheria inawataka kukusanya *VAT* kwa biashara inayouzwa kwa mkopo kwa mwezi sambamba na ile inayouzwa kwa fedha taslim.

Tunaishauri serikali kwa kuelewa hali ngumu waliyonayo walipakodi wetu ikafikiria kubadilisha matakwa hayo na kuruhusu kodi hiyo inayotokana na biashara ya mkopo kukusanywa baada ya miezi mitatu, ili walipakodi wetu waendelee kuwa kwenye biashara zao.

Mhe. Spika, kwenye Sheria ya *VAT* Nam. 4 ya mwaka 1998 walipakodi wetu wanakilio kikubwa kutokana na kukosekana na kipengele cha *Tax Refund*, ambacho huwemo kwenye sheria za kodi za nchi nyingi.

Kambi ya Upinzani inaishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na kipengele hicho ndani ya Sheria ya *VAT*, kwa madhumuni ya kuwapa haki walipakodi wetu. Mhe. Spika, hili si jambo geni limo kwenye Sheria za *VAT* na hata kwenye Sheria ya *VAT* ya Tanzania Bara. Kwa sababu kuwepo kwa kipengele hiki ni sifa muhimu ya sheria za kodi inayowezesha kuwepo kwa *equity* kati ya mamlaka husika na walipakodi.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba sheria hiyo ya *VAT* inaruhusu *Tax Credit*, bado pia utekelezaji wake wa kipengele hicho ni kikwazo kwa walipakodi. Hii inatokana na mfumo uliowekwa na *ZRB*, ambao haumpi haki mlipakodi kujipunguzia katika mauzo ya mwezi ujao iwapo *ZRB* imeshindwa kufanya ukaguzi baada ya miezi 6 kama sheria inavyoeleza.

Kambi ya Upinzani inaishauri serikali kuangalia upya utekelezaji wa kipengele hicho, ili walipakodi nao wajione wanatendewa haki kwa upande mmoja na kwa pande mwengine itasaidia kuzidisha *compliency*.

Mhe. Spika, kwa kuwa Kambi ya upinzani haina nia ya kuwatoa wajumbe kwenye maudhui ya mswada huu tunaozungumzia, isipokuwa iliona ni busara kuitanabahisha serikali kwamba inao wajibu wa kushughulikia na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili walipakodi wetu, ili madhumuni mazima ya mswada huu ya kuweza kuzidisha ukusanyaji wa mapato yaweze

kufikiwa. Kwa kweli hatuwezi kutegemea maziwa ya kutosha Kwa ng'ombe ambaye hatunzwi na kupatiwa malipo mema.

Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na waheshimiwa wajumbe wote kwa kunisikiliza.

Baada ya hayo kwa heshima kubwa Mhe. Spika, naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Waheshimiwa wajumbe nataka kusema mawili au matatu na baadaye twenda tukasali sala ya Ijumaa na michango ya jumla tuje tuifanye jioni.

Waheshimiwa wajumbe tumeanza kufanya shughuli zetu, lakini tuna matatizo mawili ambayo ni vyema tukakumbushana. Kwanza kuhusu suala la simu tumejisahau sana, ambazo zinatukera, zinatuvunjia utaratibu, kwa hiyo nakusudia tuitekeleze Kanuni yetu kama ilivyo, mwanzo ni kumuonya na baadaye kumtoa nje na akiendelea kukata ile kitu, sikitaji na kwa mujibu wa kanuni zetu tumeshaelewa.

Jambo la pili, tumekuwa tunachelewa mno, kwa maana hiyo hata shughuli zetu pia zinachelewa. Kuchelewa kwetu kunasababisha waheshimiwa wajumbe wakati mwengine wanayo nia ya kuchangia lakini wakati wa saa ya kuchangia upo na wajumbe wenyewe ambao wana nia ya kuchangia hawapo, mpaka tunamalizia kutaka kufunga mjadala ndipo wengine wanapojitokeza kwamba wanataka kuchangia.

Kwa hivyo, nadhani turudi kwenye wajibu wetu kwamba tufike mapema kwa mujibu wa Kanuni kama hakuna dharura ambayo haiwezi kuepukika basi tubaki, ili tuendelee na mjadala na hatimaye tufikie pahala tumalize shughuli hii.

Waheshimiwa wajumbe, tokea mapema asubuhi nilikuwa nikiwasiliana na wanadhim, ili kuona *quorum* inatimia. Kwa kweli nimewatoa wahudumu wetu mara mbili mpaka tatu kwa ajili ya kuhakikisha tunakusanya mjumbe mmoja mmoja warudi na kwa bahati mbaya wakati mwengine warudi wale na wengine wanatoka, sasa inakuwa kazi kubwa kweli.

Kwa hivyo, huo si utaratibu mzuri na unatuondoa katika kutekeleza wajibu wetu, ambao ni wajibu mkubwa sana kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinakwenda kwa utaratibu tena kwa nidhamu.

Nashukuru muda wote tumekuwa na mashirikiano hasa Mkutano uliopita wa Bajeti na tunaendelea tena kwa mashirikiano mazuri hayo. Lakini hili la kuhudhuria kwa wakati vikao vyetu kwa kweli hili tumetetereka kwa muda mrefu sana, kiasi cha kuwa na wasi wasi ya shughuli zetu kama zitakwenda vizuri hadi mwisho, kwa sababu akidi mara nyingi inakuwa ni tatizo kubwa.

Waheshimiwa wajumbe niwaombe turudi katika kanuni kwa kuzingatia wakati wa kuingia na kutoka, masuala ya nidhamu ni muhimu kudumishwa, ili shughuli zetu ziende vizuri.Hivyo, Waheshimiwa wananchi ambao ndio waliotupa mamlaka na madaraka ya kufanya kazi hii waridhike, kwamba tunafanyakazi waliotutuma vizuri kama wanavyohitaji *(Makofi)*.

Kwa hivyo, nilitaka niyakumbushe hayo, ili kuhakikisha shughuli zetu zinakwenda vizuri. Kwa mfano, jana wakati nilipokuwa nikiingia humu ndani basi wahudumu waliniambia hebu subiri maana hakuna watu humu ndani. Lakini niliwaambia kwamba sisi tunaongozwa na wakati, hivyo ni vyema watu kushirikiana, ili kuongozwa na wakati kwa mujibu wa Kanuni zetu zilivyo.

Kwa kweli tuliingia humu ndani mkiwa na wajumbe watano, hali hii haipendezi na wala wananchi wetu hawafurahi na sisi hatutimizi wajibu wetu. Kutokana na hali hiyo, kila Mheshimiwa mjumbe tunamuomba atimize wajibu wake kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni.

Waheshimiwa wajumbe, nakushukuruni sana *(Makofi)*.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya mwanzo kabisa ya kuchangia mswada huu ambao unahusiana na mambo ya kodi.

Mhe.Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu muhimu katika Baraza hili tukufu ili upate baraka zako na upitishwe na baadae uweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, pili napenda niwashukuru wafanyakazi wote wanaohusiana na mambo ya kodi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kufanikisha kuleta

mswada huu. Mhe.Spika, kama tutakumbuka kodi katika nchi ni suala muhimu sana kwa sababu ndio ambayo inaendesha masuala yote yanayohusiana na nchi.

Mhe. Spika, mswada huu kwa kweli mimi binafsi naona ni mswada ambao umekuja kwa wakati, wakati ambapo nchi yetu sasa hivi iko katika harakati za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Katika suala hili la kupunguza umasikini na kukuza uchumi bila ya kodi basi hatutaweza kufika pahali. Pia tukumbuke kwamba kodi ndio suala muhimu katika nchi yoyote ile ambayo inataka kuleta maendeleo kwa sababu sehemu kubwa ya nchi inategemea kodi za wananchi pamoja na miradi mbali mbali.

Mhe. Spika, vile vile napenda niwashukuru Bodi ya Mapato kwa uamuzi ambao wameufanya wa kujenga ofisi ya kisasa pale Mazizini. Mhe. Spika, kwa kweli ofisi hii itakuwa ni chachu na nyenzo nzuri ya kuwezesha ukusanyaji wa kodi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kama tunavyokumbuka kwa sasa hivi Bodi ya Mapato iko katika ofisi ya kukodi na ufanisi wake kwa kweli katika ofisi ile tunaweza tukasema kwamba unakwaza kutokana na mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, nianze na sehemu ya pili. Sehemu ya pili inahusiana na mambo ya usajili na kufuta usajili. Suala la usajili ni muhimu kwa maana kwamba unapoweza kuwasajili walipa kodi, unapoweza kujua walipa kodi wako ndio utakuwa na wigo mzuri wa kuweza kukusanya kodi. Lakini sio kukusanya kodi tu, wigo mzuri wa kuweza kujua au kukisia mapato ya nchi yako. Hukuweza kujua kwa mwaka unawalipa kodi wangapi na kodi za aina gani, basi hapo Mhe. Spika utakuwa katika mstari muhimu wa kuweza kujua mapato yako ya nchi.

Mhe. Spika, kipengele hiki cha usajili wa kodi kinamtaka kila mmoja ambaye anafanya shughuli ambazo zinamuajibika alipe kodi ni lazima kwanza asajiliwe. Mhe. Spika, hili ni muhimu. Taarifa ni muhimu kila pahali kwani bila ya taarifa huwezi kujua mafanikio na pia huwezi kujua matatizo yanayokukabili. Mhe. Spika, tunapozungumzia taarifa tunazungumzia jambo muhimu la kuweza kujua kila kitu katika mambo ambayo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, walipa kodi katika nchi yetu wako wengi na wako wa aina mbali mbali. Kuwajua walipa kodi ndio suala muhimu katika ukusanyaji wa kodi, bila ya kujua walipa kodi hutaweza kufanya kazi zako kwa ufanisi zaidi.

Kipengele hiki nadhani kinakusudia kuwatambua na kuwajua walipa kodi wote kwa wakati wowote ambapo itahitajika. Mhe. Spika, ili uweze kukusanya kodi

vizuri basi ni lazima umjue mlipa kodi, na unapoweza kumjua mlipa kodi ndipo utakapoweza kukusanya kodi hiyo vizuri. Kwa hivyo, kipengele hiki nadhani ni muhimu sana katika sheria hii ili kuweza kuleta ufanisi wa ukusanyaji wa kodi katika nchi.

Mhe. Spika, tumekuwa tukikusanya kodi kwa muda mrefu, lakini wakati mwengine tunakuwa tunashindwa kuwajua walipa kodi wetu kwa sababu tu taarifa zao hazikuwekwa vizuri. Kwa maana hiyo sheria hii inakusudia kuweka mfumo mzuri wa ukusanyaji wa kodi kwa kuwajua na kuwatambua walipa kodi wote ambao wanastahiki kulipa kodi. Pale ambapo mmoja au mtu mwengine hataweza kulipa kodi, basi itakuwa ni rahisi kuweza kufuatilia na kuweza kumjua nani kwa wakati huu anawajibika kulipa kodi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilitaka nichangie kwanza ni suala la madhumuni na sababu ya mswada huu. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 35 kuna madhumuni ya mswada huu ambayo yameelezwa kuwa mswada huu unakusudia kutunga sheria itakayoweka utaratibu wa kusimamia kodi. Vile vile kodi hizo zitakusanywa hapa Zanzibar kwa maana ya kwamba mswada huu unahusisha zaidi kodi ambazo zitakusanywa hapa Zanzibar. Pia mswada huu unakusudia kusajili walipa kodi wote ambao watasajiliwa na Bodi ya Mapato hapa Zanzibar ambapo itarahisisha kuwafahamu, kuhakiki na kuwafuatilia walipa kodi.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema madhumuni au umuhimu wa kuwasajili walipa kodi ni kuweza kuwatambua na kuweza kuwafuatilia. Mhe. Spika, tunahitaji kujua kodi zinazolipwa katika nchi, huwezi kujua kodi ambazo zinalipwa katika nchi bila ya kuwa na utaratibu au mfumo ambao utakuwa unawasajili.

Mhe. Spika, hivi karibuni Bodi ya Mapato ya Zanzibar ilikuwa na utaratibu wa kukusanya kodi ambazo zinahusiana na magari. Mhe. Spika, tulishuhudia kwa kiasi gani kazi kubwa ambayo inaikabili Bodi hii ya Mapato ya Zanzibar. Tuliona kwamba kwa kiasi gani kodi kama itashughulikiwa hapa Zanzibar basi inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba hapo awali kulikuwa hakuna utaratibu mzuri wa kukusanya kodi hizi kwa mfano kodi za magari. Lakini baada ya kujua kama kuna umuhimu wa kuwasajili walipa kodi hawa ambao wanahusiana na magari, basi imeonekana kwa kiasi gani kwamba Zanzibar inavyoweza kunufaika na ulipaji wa kodi mbali mbali.

Mhe. Spika, nawashukuru kwa kuwa na utaratibu huu ambao sasa hivi kwa kweli kila mlipa kodi awe muendesha gari ama pikipiki sasa hivi anajijua

kwamba ikifika wakati fulani nawajibika kulipa kodi na nisipolipa basi faini yangu ni kiasi gani.

Kwa hivyo, madhumuni haya ambayo yamekusudiwa kuwekwa hapa kama yalivyoelezwa kwamba kuwahakiki, kuwafuatilia vile vile kuwafahamu ni jambo la kwanza kabisa katika kufanya kazi yote.

Mhe. Spika, kodi katika nchi kama nilivyosema mwanzo ni muhimu sana, na kama nchi haitaweza kukusanya kodi basi nchi hiyo haitaweza kusonga mbele katika hatua za maendeleo mbali mbali. Mhe. Spika, ukisafiri nchi nyengine za nje ukijaribu kudadisi jinsi gani wananchi wanawajibika kulipa kodi utajua kwamba nchi hiyo inawajibika vipi. Kwa mfano, kuna wenzetu tunasema kila siku hapa kwamba wanapatiwa kila kitu bure, kwamba huduma za jamii ziko nzuri na sisi wakati mwingi tumekuwa tukilalamika kwamba pengine huduma za jamii hapa Zanzibar haziko bora zaidi. Lakini nafikiri kuna sababu ambayo ndio inapelekea hivyo, jambo kubwa hapa ni kuwajibika katika kulipa kodi, wananchi wakijua na wakifahamu umuhimu wa kulipa kodi, bila shaka huduma za jamii nazo zitakuwa nzuri.

Mhe. Spika, lazima tukubali kwani sasa hivi wakati umefika wa kuhakikisha kwamba kila ambaye anawajibika kulipa kodi awe analipa kodi hii kwa wakati kwani ndio ambayo itatupelekea katika kuweza kutoa huduma mbali mbali za kijamii.

Mhe. Spika, Serikali kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wa wanapata huduma mbali mbali zikiwemo huduma za kijamii. Vile vile huduma ambazo wanawajibika kuzipata kwa maana ya kwamba wazipate. Vipi wataweza kuzipata huduma hizi ni lazima kuweko na mapato na mapato haya yanategemea sana na uwezo wa kodi. Kwa nchi kama zetu ambazo sasa hivi zimejitoa katika mfumo wa uendeshaji wa miradi ya kiuchumi, inategemea zaidi uwigo wa kodi ambayo inakusanywa.

Mhe. Spika, nadhani nimetoa utangulizi kuhusu madhumuni na sababu ya kuja mswada huu. Sasa niendelee na sehemu ya tatu ambayo inahusu masharti na ridhaa ya kulipa kodi.

Mhe. Spika, katika kipengele hiki kuna masuala mazima ya leseni ya biashara kwa mtu ambaye anafanya biashara. Mhe. Spika, ni lazima tuhakikishe kwamba wanaofanya biashara wanaweza kupatiwa leseni lakini pia wawe wanalipa kodi. Katika kipengele hiki cha 3 wanasema kwamba leseni yoyote itakayotolewa kinyume na masharti ya kifungu hiki basi itakuwa ni batili.

Mhe. Spika, nadhani tumekuwa tukishuhudia katika nchi yetu kwamba kuna watu ambao wanajihusisha na vitendo vya ubadhirifu. Moja ya mambo ambayo yamejitokeza na tuna uzoefu nayo kwa mfano katika leseni hizi za magari. Mimi nilibahatika kuwa na gari na gari lilikuwa ni gari la abiria na nimewakabidhi watu, lakini baadae nikaja nikagundua kwamba nimepewa leseni feki ya barabara. Mhe. Spika, kwa kweli vitendo hivi ni lazima tuvikemee na tuhakikishe kwamba vitendo hivi haviendelei.

Mhe. Spika, ni lazima tuhakikishe kwamba leseni ambazo zinatolewa ni sahihi na zinatolewa kwa mamlaka inayohusika. Kwa maana hii , sharti ya kulipa kodi ni kwamba lazima mtu awe na leseni. Kwa hivyo, mamlaka inayohusika ni lazima ihakikishe kwamba leseni hizi ambazo zinatolewa ni zile ambazo zina wajibu wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, wakati mwengine unaweza ukapewa risiti, lakini risiti hii ikawa sio risiti ambayo inawajibika kulipa kodi. Kwa maana hiyo kuna mwanya ambao unaweza ukajitokeza ikiwa hatutakuwa makini katika kuangalia mtu gani anaendesha biashara na aina ya leseni ambayo anaitumia.

Mhe. Spika, kwa kweli ni lazima tukubali kwamba bila ya kodi na bila ya utaratibu mzima wa leseni basi kodi hiyo haitaweza kukusanywa vizuri. Hapa ninachokusudia kusema Mhe. Spika ni kwamba mamlaka ambayo inahusika ni lazima ifanye utaratibu wa kuzikagua leseni zote ambazo zinatolewa kwa ajili ya kudhibiti mapato haya ambayo yanahitajika kupatikana.

Mhe. Spika, lakini tukirudi nyuma tumekuwa na tofauti kubwa baina ya kodi ambayo inatolewa na *VAT* pia na kodi ambayo inatozwa hapa visiwani. Mimi nimekuwa nikijiuliza kwa nini haya yajitokeze, hivi kwa kweli hatuna kumbukumbu muhimu ambazo zinatuwezesha kwamba kujua nani alilipa kodi kiasi gani?

Mhe. Spika, mfano ni suala hili ambalo linapigiwa kelele kwamba ukitoa mzigo Zanzibar utalipa kodi hii, lakini ukenda Bara ulipe kodi hii. Nimekuwa nikijiuliza *TRA* na Mamlaka ya Kodi hivi wanakuwa hawana uhusiano wa karibu wa kuweza kuhakiki kodi ambayo inalipwa hapa au hapa kwa kiasi fulani tunapata nafuu ya kodi ambayo pengine ukenda kule Bara inawezekana ikawa ni tofauti.

Nadhani jambo kubwa hapa ni taarifa ambazo tunahitaji kuziweka vizuri, tukiwa na taarifa vizuri nadhani hili lisingeweza kujitokeza. Kwa hivyo, ninachokusudia kukizungumza hapa ni kwamba taarifa hizi ni muhimu kwa maana ya kwamba ya kuweza kufuatilia suala zima la kodi na kuweza

kupunguza manung'uniko ambayo yanaweza yakajitokeza wakati wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la tathmini, katika kifungu cha 19 ambacho kinasema uwezo wa kufanya tathmini. Mhe. Spika, wakati mwengine inakuwa inashangaza kodi ambayo anapaswa kulipa mtu kwa mujibu wa thamani ya mali aliyonayo, lakini wakati mwengine tunafanya tathmini pengine inawezekana ni tofauti na thamani ile. Inawezekana tunakisia wakati mwengine tunafanya mambo mengine tofauti. Ninachokusudia kusema katika kifungu hiki cha 19 ni kwamba imeelezwa wazi kuwa mtu yeyote ambaye analipa kodi kutakuwa na adhabu ama riba ambayo itatozwa kwa mtu ambaye ama atafanya udanganyifu , ama atafanya uzembe au dharau ya kuwacha kulipa kodi kwa makusudi.

Mhe. Spika, kipengele hiki ni muhimu kwa sababu tumekuwa na mtindo sasa hivi watu ama wanapunguza thamani ya mali walizonazo ama wanafanya ujanja wa kulipa kodi. Kama kutakuwa na kipengele hiki ambacho kitamlipisha faini ama adhabu au riba kwa yule ambaye amecheleweshe kodi basi nadhani itaweza kuwabana walipa kodi na kuweza kulipa kodi kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, hili ni muhimu kwa sababu tayari kuna uzoefu wa ukwepaji kulipa kodi. Mhe. Spika, lakini hili ni lazima wafanyabiashara walifahamu, ni lazima tuwe na taaluma nzuri kwa wafanyabiashara wetu ili waweze kujua kwamba ukifanya hivi ni kosa na usipofanya hivi utawajibika kulipa kitu fulani. Kwa hivyo, hapa pamoja na kupitisha sheria hii tunahitaji zaidi kuwaelimisha wafanyabiashara wetu, tunahitaji zaidi kuwapa taaluma wafanyabiashara wetu waelewe ili wasiweze kuingia katika makosa.

Mhe. Spika, makosa wakati mwengine mtu anafanya makosa bila ya kutegemea kwamba anaweza kufanya kosa fulani ambalo kwa kweli linaweza likamtia hatiani. Lakini tutakapokuwa tunawapa taaluma muhimu wafanyabiashara wote, basi hawataweza kuingia makosani na kuweza kupata adhabu ambazo hazistahiki.

Mhe. Spika, ni lazima tuhakikishe kwamba kodi katika nchi hii inakusanywa. Lakini tutahakikisha vipi kodi katika nchi hii tunakusanya ni lazima tuwe na sheria ambayo itaweka utaratibu wa ulipaji wa kodi.

Mhe. Spika, migogoro mingi imekuwepo ya ulipaji kodi katika nchi yetu. Inawezekana kwamba utaratibu haufuatwi lakini pia inawezekana kwamba udhaifu wa utaratibu tulionao. Mhe. Spika, sheria hii nina amini kabisa ikipita nina uhakika kwamba walipa kodi watakuwa makini katika kutekeleza sheria hii ambayo kwa kweli itawezesha nchi yetu kupiga hatua ya maendeleo.

Mhe. Spika, mara nyingi Mhe. Rashid Seif Suleiman amekuwa akiniuliza masuali lini nchi yetu itaweka samani pengine madarasani. Lakini mara nyingi samani za madarasa inategemea na ukuaji wa uchumi, inategemea na hali ya uchumi pia inategemea na hali ya fedha. Mhe. Spika, makusanyo yakiwa mazuri bila shaka huduma hizi ambazo mara nyingi tumekuwa tukizilalamikia hapa Barazani basi nazo pia zitaboreka.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ambayo inahusu kumbukumbu, nyaraka na ukaguzi. Mhe. Spika, hapa kumewekwa utaratibu mzima kwamba kila mlipa kodi atawajibika kuweka kumbukumbu za hesabu katika sehemu yake ya biashara iliopo Zanzibar ikijumuisha nyaraka zifuatazo. Kwa mfano, nyaraka halisi za mauzo, nakala ya Ankara ya kodi, nyaraka za bandari na kadhalika.

Mhe. Spika, bila ya kuwa na nyaraka hatuwezi tukamtoza kodi mtu inayostahiki. Wafanyabiashara wetu wengi hawaelewi umuhimu wa nyaraka hizi, ama wakati mwengine wanapuuza kuweka nyaraka hizi na ndio pale wanapotasmiwa kodi ambayo pengine haina msingi fulani ambao wa thamani wa ile mali yake. Pia wamekuwa wakilalamika wafanyabiashara kwamba wanatozwa kodi pengine mali ambayo haistahiki, lakini kwa nini walalamike wakati wanawajibika kuweka kumbukumbu hizi ambazo ndio itakuwa msingi wa kutoza kodi.

Mhe. Spika, kama nyaraka hizi zitakuwa zinawekwa vizuri basi hakuna sababu ya kulalamika kwa mfanyabiashara kwamba anatozwa kodi zaidi ya thamani ya mali ambayo aliyonayo. Nadhani kiwango cha kodi kiko wazi, asilimia ya kodi iko wazi hasa inapotokea mtu analalamika kwamba ametozwa kodi kinyume au zaidi ya thamani ambayo aliyonayo ni dhahiri kwamba kuna udhaifu katika kumbukumbu ambazo anastahiki aziweke.

Mhe. Spika, mimi sioni sababu kwa nini mfanyabiashara alalamike kwamba ametozwa kodi nyingi wakati kiwango cha kodi kinaeleweka kwamba ni asilimia pengine 18 ama asilimia ngapi. Kama ataweza kuweka kumbukumbu hizi basi itaonesha dhahiri kwamba yeye hatoweza kuonewa katika kulipa kodi hiyo kwa hiyo kipengele hiki kinakusudia kuweka mfumo au kuweka utaratibu mzuri na kuweza kuondoa malalamiko katika ulipaji kodi.

Mhe. Spika, mara nyingi kumekuwa na mtindo ukenda dukani hupewi risiti inayostahiki kupewa. Mhe. Spika, kwa nini wafanyabiashara wafanye kitu kama hicho? Ni dhahiri kwamba wanakwepa kulipa kodi.

Mhe. Spika, mimi ningependekeza kwamba katika sheria hii ni lazima kuweko na adhabu ambayo mtu ambaye hakuweka kumbukumbu vizuri basi aweze kupata adhabu fulani kwa uzembe ambao utakuwa umesababishwa na kuikosesha kodi serikali.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba kumbukumbu ni muhimu na kipengele hiki nacho kimetilia mkazo kwa kiasi kikubwa kwamba ule msingi wa kulipa kodi uweze kuegemea wapi. Ni nyaraka ndizo ambazo zitaweza kuelezea kodi ya muhusika. Pia katika kipengele hicho hicho cha nyaraka, kipengele cha 29 kimeelezwa kwamba ili kuweka udhibiti mzuri wa kulipa kodi ni lazima kwamba kwa madhumuni ya sheria hii kuwa Kamishna anaweza kuchukua au kutoa nakala au kuchomoa kutoka kwenye nyaraka za kumbukumbu zinazohifadhiwa chini ya masharti haya.

Mhe. Spika, ni lazima kwamba kumbukumbu hizi zipatikane kwa sababu bila ya kupatikana kumbukumbu hizi watoza kodi hawatakuwa na msingi wa kutoza kodi, ili aweze kutoza kodi halali ni lazima awe na kumbukumbu na kama mfanyabiashara anafanya biashara bila ya kumbukumbu basi huyu tujue anakusudia kukwepa kulipa kodi. Kwa hivyo, nadhani kipengele hiki cha 5 kinakusudia kuwabana au kuweka mfumo mzuri kwa ajili ya kupata kodi halali na kupunguza manung'uniko ya wafanyabiashara ambao mara nyingi wamekuwa wakinungunika kwamba wanatozwa kodi isivyo halali. Lakini kumbe inawezekana kwamba tatizo ni lao wao kwa sababu hawaweki kumbukumbu halisi za biashara ambazo wanazoziendesha.

Mhe. Spika, sehemu ya 7 inahusiana na mambo ya kurejesha kodi, kwa maana ya kwamba kiwango chochote cha kodi, fani, adhabu, riba au kiasi chochote kinachohitajika kulipwa kodi chini ya sheria hii, kitachukuliwa kama ni deni kwa serikali na kitatakiwa kulipwa kwa mujibu wa utaratibu ambao umewekwa.

Mhe. Spika, tumekuwa na utaratibu ama pengine udhaifu ama kutokufahamu. Mara nyingi mfanyabiashara anachelewesha kulipa kodi kwa maana tu pengine yakutokufahamu kwamba wakati sasa hivi umefika ama anaona labda atakwenda kulipa kesho kutwa.

Mhe. Spika, kama kutakuwa na utaratibu wa faini, kama kutakuwa na utaratibu wa adhabu basi naamini kabisa kwamba wafanyabiashara wataweza kulipa kodi hizi kwa haraka kabisa na Serikali kuweza kupata mapato yake. Katika vifungu hivi nadhani mfanyabiashara ambaye hatalipa kodi kwa wakati basi atawajibika kulipa faini au atawajibika kulipa riba au kuwa na adhabu fulani ambayo tu kwa sababu amechelewesha kulipa kodi.

Mhe. Spika, suala la kulipa kodi ni suala ambalo hatuwezi tukalifumbia macho, ni lazima sasa hivi wakati umefika tujue kwamba kodi inayostahiki kulipwa inalipwa kwa madhumuni au kwa malengo yakuweza kutoa huduma za jamii katika nchi yetu. Lakini Mhe. Spika, vyanzo vyetu vya mapato ni vingi na kama tutakuwa makini kabisa kukusanya kodi basi nchi hii nadhani haitakuwa na shida ya mapato. Pamoja na kwamba tunayo matatizo lakini kama tutayadhibiti matatizo haya basi kodi katika nchi hii itakuwa inakusanywa vizuri na nchi itaendelea vizuri.

Mhe. Spika, katika sehemu ya tisa nadhani hapa kuna masharti mengineyo kwamba mtu yeyote atakayejaribu kukwepa kulipa kodi atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa kodi ambayo kama alilipa asingelikuwa ametenda kosa. Mhe. Spika, tukubali kwamba sheria ni lazima tuifuate na kama tutashindwa kuifuata sheria basi lazima tukubali kuingia makosani kwa maana ya kwamba lazima tuwajibike, sheria lazima iwe na meno.

Mhe. Spika, bila ya kuwa makini na sheria hii tutakuwa tunatunga sheria kila siku, lakini matokeo yake sheria hizi hazitekelezwi. Kwa maana hiyo sheria hii nina amini kabisa kwamba itaweza kuweka msingi wa kukusanya kodi katika nchi yetu na kuwabana wale ambao wanakusudia kutokulipa kodi na kuikosesha mapato nchi yetu.

Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba nchi hii itaendeshwa kwa kodi za wananchi, na kila ambaye ana uwezo wa kulipa kodi basi ni lazima alipe kodi kwa maslahi yake. Mhe. Spika, mtu anapolipa kodi ni maslahi yake kwa sababu kodi hii inakwenda ama katika hospitali, kodi hii ama inakwenda katika mashule, kodi hii ama inakwenda kwenye barabara. Tutakuwa tunalaumu kila siku kwamba nchi hii haijengi barabara, barabara ni mbovu, miundombinu ni mibovu lakini tunawajibika vipi katika kulipa kodi ni lazima tujiulize na tuwahamasishe wananchi wetu umuhimu wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, jana tulikuwa tunajadili mswada wa utalii na mengi yalijitokeza ya kuwa na malalamiko au shutuma kwamba serikali haijaanzisha miundombinu kama barabara ya kuwezesha utalii kuweza kukua. Lakini vipi Serikali itaweza kuanzisha miundombinu bila ya fedha. Mhe. Spika, ni kutokana na kodi ambazo zinatonzwa ndizo ambazo zitaweza kuweka au kufanikisha miundombinu hii.

Mhe. Spika, nilibahatika kwenda Marekani mwaka mmoja na nilitembelea skuli kama tano na nikawa najaribu kuwauliza wale wazee ambao wanawapeleka watoto wao skuli. Mtoto kule anaondoka asubuhi mpaka jioni ndio anarudi nyumbani, nikawa nawauliza hivi nyinyi mnalipa kiasi gani katika

shule hizi? Wakanambia kwamba sisi hatulipi chochote kwenye shule, lakini tunalipa kodi, tukishalipa kodi wajibu wetu umekwisha katika kutoa huduma hizi. Ni kweli kwamba wanalipa kodi na zinafanya kazi, serikali za majimbo ndizo ambazo zinakusanya kodi na kuweza kutoa huduma hizi muhimu za kijamii. Kwa hivyo, watoto kule wanasoma vizuri lakini ni kwamba kila mzazi anawajibika kulipa kodi.

Mhe. Spika, Marekani ni tofauti na kwetu, watu wetu ni wanyonge, watu wetu walio wengi hawafahamu umuhimu wa kodi hata kama mtu anao uwezo wa kulipa kodi. Wakati umefika sasa hivi tuhakikishe kwamba wananchi tunawaelimisha umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo yao. Kwa sababu watalalamika kila siku lakini bila ya kodi nchi haitaweza kwenda, hatuna mjomba wa kuweza kutupa fedha sisi kila siku kwa ajili ya kuendesha huduma zetu za kijamii.

Mhe. Spika, sheria hii kama nilivyosema imekuja kwa wakati na ni sheria muhimu sana katika nchi yetu kwa sababu ndio uti wa mgongo wetu sasa hivi. Sasa hivi kama tunavyosema karafuu si zao la kutegemewa sana katika nchi yetu, nazi si zao la kutegemewa sana katika nchi yetu, tunategemea zaidi kodi za wananchi.

Lakini pia nirudi tena kwa viwanyo vya kodi. Mhe. Spika, tunahitaji kuweka viwango vya kodi ambavyo vinalipika na viwango ambavyo vitawahamasisha wananchi wetu kulipa kodi kwa hiari. Ni lazima tujenge utaratibu kwa wananchi wetu kulipa kodi kwa hiari bila ya kusukumwa.

Mhe. Spika, utakapoweka kiwango cha kodi ambacho kitampa motisha mwananchi ndivyo atavyoweza kulipa kodi vizuri. Nina uhakika viwango vilivyopo sasa hivi ni viwango ambavyo vinawashawishi na vinawahamasisha wananchi kulipa kodi, linalotakiwa ni taaluma tu kwa wananchi sasa hivi kwamba wajue umuhimu wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, naamini kabisa kila mtu anaweza kulipa kodi ambayo anaweza kulipa kama atashajihishwa na kama atakuwa na taaluma muhimu ambayo inampasa alipe kodi.

Tunashuhudia ongezeko la mapato kila baada ya muda, kama Bodi ya Mapato ikiweza kuweka mkazo kidogo basi utakuta kwamba mapato yanaongezeka. Lakini naamini kabisa kuwepo kwa sheria hii basi kutaweza kutoa motisha zaidi na kutahamasisha wafanyakazi pamoja na wananchi kuweza kulipa kodi.

Mhe. Spika, nadhani unanitizama kwamba nimeshachukua muda wako mwingi, kwa hivyo, nadhani nimalizie ili niweze kuwapisha wenzangu waweze

kuchangia nao. Naomba nimalizie kwa kusema kwamba kodi katika nchi ndio suala muhimu na ndio suala la mwanzo la kutiliwa mkazo katika kukusanya mapato ya serikali, bila ya kodi nchi haiwezi ikaendeshwa lakini pia bila ya kodi hatuwezi tukaendesha huduma za jamii kwa sababu tutakuwa hatuna mapato.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hayo, natamka rasmi kwamba naukubali mswada huu mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri kwa Spika kumuangalia mjumbe hasa yule anayezungumza hiyo ndio kawaida na ndio utaratibu hasa, lakini nakushukuru kwamba umeokoa jahazi kwa kiasi kikubwa sana. Kwa sababu karibu ilikuwa nimwite Mhe. Waziri.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni ya leo kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza kuhusiana na mswada uliopo mbele yetu wa usimamizi wa kodi.

Namshukuru Allah Subuhana Wataala kwa kutuweka hai na wazima tukaweza kufika siku ya leo na tukaweza kuwepo jioni hapa kuchangia machache katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, nikiunganisha maneno na mjumbe aliyamaliza napenda kidogo nitofautishe baina ya ukuaji uchumi na ukusanyaji wa kodi. Mhe. Spika, serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yake unakua. Kwa sababu utakapokua uchumi na ule mbano wa kodi utakuwa unapungua. Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri alisema jambo ambalo mimi tayari nimeshali-*site* ni zuri kuliunganisha hapo hapo kwamba kukubali watu kwa hiari kutoa kodi au kufuatilia watu zile kodi ni kwa sababu zile kodi huwa zinaonekana. Unapokwenda katika sehemu ya huduma ile kodi unaiona kwamba hii.

Kwa mfano, tunayo taarifa kwamba katika nchi za *Scandinavia* basi mishahara ya wafanyakazi mingi sehemu kubwa kidogo inakwenda kwenye ulipaji wa kodi, lakini wao huwa hawajali hilo kama alivyosema hapa kwamba wanaloliona ni kwamba wakienda hospitali wanaiona ile kodi yao na huduma wanazopata, wakiwapeleka watoto wao skuli wanaiona ile kodi yao na huduma wanazopata.

Sasa nadhani haya mambo yawe *parallel*, wakati tunapokamua kuhakikisha kwamba tunasimamia kodi nzuri basi tuhakikishe vile vile kodi ile inaonekana na wale wananchi, wale wananchi wenyewe wafike wakati waweze wao wenyewe kuisimamia ile kodi yao ndipo wafanyabiashara watakapoona kwamba wanadaiwa risiti, wanadaiwa na hili, lakini bado tukimwambia

kwamba mzazi achangie shilingi 40,000 katika wodi haioni ile kodi, kwa hivyo, hata akipewa risiti asipewe inakuwa bado yeye anaona hapana jambo kubwa.

Kwa hivyo, ni muhimu mambo haya mawili yende sambamba, wakati huo huo fedha ile inayopatikana itumike vizuri kwa maslahi ya wananchi na mwananchi ajue kwamba ni kodi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nazungumza sana kwamba labda mirathi ya ukoloni kidogo imetupeleka mbali sisi, hizi fedha kuziita fedha za serikali wenzetu wanaita *tax pairs money*, yaani fedha za mlipa kodi. Kwa hivyo, tayari ile *definition* anayo mtu ndani ya nyumba yake, kazini kwake kwamba hizi fedha ni za mlipa kodi. Sisi tafsiri yetu kwamba ni fedha za serikali wala isiitwe fedha ya umma ni fedha ya serikali mtu anaona huko ndani au majumbani kwamba serikali ni dude kubwa lenye fedha nyingi ziko benki kwa hivyo ni pesa za kuponda tu.

Sasa nafikiri tungeanza hata maskulini tukaanza kuwaelewesha wanafunzi wetu wakafahamu nini maana ya fedha ya serikali na nini maana yake katika matumizi, ingelisaidia. Lakini kuita fedha ya serikali siku zote ndio inapelekea kwamba watu hawaamini kuwa kodi ndio inayotumiwa kufanya mambo mengine kwa sababu wanajua serikali ni dude ambalo lina pesa.

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kwanza nilipongeze Baraza lako tukufu kwamba sisi kwa mara ya kwanza katika kamati mara hii tumepata wasaidizi waalikwa wa sekta binafsi wakiwemo viongozi wa *NGO's* kuja kutupa mawazo yao katika miswada hii. Huu mmoja tulionao sasa hivi ni mmoja katika hiyo miswada ambayo muliwaalika. Kwa hivyo, mimi natoa pongezi na shukurani sana kwa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kufikia kiwango hiki cha kuwaalika sekta binafsi kuja kushirikiana pamoja na kamati kwa kutoa mawazo katika mswada.

Vile vile wakati Baraza limefikia katika kiwango hicho wale wateja wakuu au wadau wakuu tuliowaalika wameleta malalamiko yao wanasema kwa mswada huu wizara haikuwashirikisha tangu matayarisho ya awali. Sasa hili limezungumzwa na Mhe. Waziri Kivuli, limezungumzwa na Mhe. Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mimi napenda kulitilia mkazo kwamba wadau madhali tayari ipo sera iliyokubaliwa na serikali ya kushirikisha sekta binafsi katika maamuzi, basi ni vizuri kuwashirikisha tokea awali, ili huu mswada ukifika hapa uwe una *component* zote za upande wa serikali, upande wetu Wajumbe wa Baraza na upande wa sekta binafsi. Sasa hapo utakuwa kidogo makali yake yamepungua, yani sio makali ya kwamba sasa utakuwa ni laini, lakini utakuwa unaingia

katika jamii kwa ulaini kidogo kuliko vile unavyotoka mswada au sheria inavyopenya katika jamii moja kwa moja tu bila ya kupitia kwa wadau wakubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kupitia kwako tunamuomba Mhe. Waziri kwa mara nyengine akiwa na mswada ambao wadau wakuu wapo na Baraza limeona kwamba wawaalike basi wapewe nafasi hii tokea awali.

Mhe. Spika, jambo jengine kabla sijaingia katika vifungu vya mswada huu, ni suala la kulipa kodi kwa hiari. Sisi tulipotembelea *TRA* tayari tumekuta kwamba wana *list* kamili ya wafanyabiashara wao. Pamoja na matatizo yaliyoko, lakini wana *list* ya wafanyabiashara wao ambao wao mizigo yao wanahaulisha na wao wanapeleka zile *document* zao kwa *TRA* hali ya kuwa wao watakuja kulipa baadae. Ni hao wadau ambao wanalipa kodi yao kwa hiari na wameshachunguzwa kwa muda mrefu.

Sasa katika usimamizi wa kodi hii *ZRB* ina wajibu wa kufanya kazi hii, kila baada ya kipindi wanaangalia lakini ni vizuri basi kila mwaka wangetoa katika *list* yao watu wawili au watatu hata mmoja lakini wakasema huyu tumeshamtenga kwamba ni safi na kila mara mizigo yake ipo. Sio kwamba hatofanyiwa uchunguzi huyo, lakini ni kwamba atarahisishiwa kiasi cha kwamba iwashawishi na wale wengine kukubaliana na kulipa kodi kwa hiari badala ya kufukuzana.

Jambo jengine ni viwango vya kodi, sijui kama katika makubaliano ya Afrika Mashariki kuna viwango maalum vilivyopangwa, lakini mimi nafikiria kwamba Zanzibar kwa sababu ya udogo wake, nchi ndogo na biashara kwa hivyo haiendi kwa kasi sana kama katika nchi kubwa. Nchi yenye *population* kubwa na ambayo mipaka yake ni kwa gari tu, *volume* yake ya biashara wanayofanya ni kubwa. Kwa hivyo, hata kama wataweka viwango vikubwa vile vya kikodi vinawaruhusu kwa sababu wale wanaolipa zile kodi wanafanya biashara haraka haraka.

Lakini nchi kama Zanzibar ambayo mipaka yake ni bahari na sisi Mhe. Spika, kwa taarifa ni kwamba tulipokwenda *TRA* walisema pamoja na kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini bado kuna sheria inayosema bidhaa yoyote inayogusa bahari inaangaliwa upya, inafanywa hivi upya, iko sheria hiyo iliyoko *TRA.*

Kwa hivyo, tungelipaswa na sisi kutizama kama itaruhusu kuvitizama upya viwango vyetu vya kodi kwa maslahi ya wananchi wetu. Kwa sababu *population* yetu sisi ni ndogo na kasi ya kwenda biashara ni wanunuzi wale waliopo. Sasa ikiwa wanunuzi ni wale wale wa kukutana nao ukawatolea

Assalamu Alaykum mara tano kila siku akishapita mara moja hapiti tena, lakini kama Dar es Salaam akija mteja mmoja akija wa pili na mwengine na mpaka usiku pengine yule humuoni tena hata njiani. Sasa tuvitizame hivi viwango.

Lakini kama ilivyofanyika mara hii kwamba Bunge limetangaza asilimia 18 *VAT* basi, bahati nzuri Mhe. Waziri wetu akaidaka ile na yeye asilimia ile basi haiwi hivyo, tungefika angalau asilimia 15 sisi halafu tukawaambia wafanyabiashara wetu mnaona hivi tulivyowafanyia? Kwa hivyo, naomba suala hilo lingefanyika kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, sasa nikienda katika baadhi ya vifungu niende kifungu cha 5 katika mswada huu ambacho kuna mambo ambayo yangewekewa ufafanuzi ili kusije kukawa na mparaganyo wa mawazo. Kama nilivyosema mwanzo sasa hivi kwamba nchi yetu ni ndogo, kwa hivyo, hata hawa wafanyabiashara si wafanyabiashara wengi wanaoshughulika na *item* moja tu. Kwa mfano nchi kubwa kama Tanzania Bara au nchi nyengine za Bara anaweza mtu akashughulika na *tiles* tu ikawa yeye analeta *tiles* tu duka ni kwake huendi kununua kitu chengine.

Mhe. Spika, utastaajabu, mimi mara hii nilipokwenda safari ya Hijja kule kuna ndugu yanngu akanambia twende nikakupeleke katika maduka ya nje ya hii sehemu ambayo mahujaji wanakwenda. Sasa tukenda katika duka moja la kanzu, Mhe. Spika, kwa taarifa ya Baraza hili hauzi isipokuwa kanzu tu, tena ya kabila moja tu hakuna kabila nyengine yoyote. Kwa sababu nchi ni kubwa na wateja wanajua wakienda pale wanakwenda kununua kanzu zile, lakini maduka yetu hatuwezi hivyo ikiwa kanzu ya Oman ipo, ya Yemen ipo, ya Zanzibar ipo, ya Dubai ipo, kwa sababu wateja wake ni kidogo.

Sasa hapa katika kifungu hiki cha 5(2) pameandikwa ‘mtu anayekusudia kufanya biashara zaidi ya moja atalazimika kusajiliwa kwa kila biashara’. Hapa ndio tunaposema kwamba toka katika kamati na sasa nasisitiza kwamba lazima pawe na *definition* hiyo biashara kwa hapa Zanzibar ni ipi? Kama tukisema *item* zote za nguo ni biashara moja basi tukubaliane na mabegi nayo ni sehemu ya nguo kwa sababu nguo zinataka kuingizwa katika begi, nyuzi nazo ni nguo kwa sababu ikifumuka inataka kushonwa. Kwa hivyo, tukubaliane aina ya biashara bila ya hivyo hatutakwenda hilo ndilo ninalotaka kusema.

Kifungu hicho hicho cha 5 tulikijadili katika kamati lakini nazidi kusisitiza, kwamba mtu anayekusudia kufanya biashara katika eneo zaidi ya moja atalazimika kusajiliwa katika kila eneo. Sasa huyu asipewe fomu mpya, malipo yake yatizamwe kwa sababu ana duka lake la bati Darajani lakini kaona Darajani wakati mwengine watu hawafiki siku hizi watu wanafika Saateni, basi akafungua kiduka chake na kule Saateni lakini bati ni ile ile na *store* yake

kubwa ipo hapa hapa kule anapeleka bati zake 10 tu. Sasa je, ajisajili tena na pale alipofungua bati yake ni ile ile.

Kwa hivyo Mhe. Spika, lazima wafanyabiashara wanataka kupewa elimu madhubuti na iwe *inconsistence*, lile lile, ikiwa maamuzi kwamba lile liitwe tawi basi na mwengine atakapoweka liitwe tawi, sio huyu tawi lakini mwengine wewe madhali unamuweka mtu mwengine hukai weye hii ni biashara nyengine, lakini ni mie mie.

Naambiwa kuna mtu mmoja katika *Suleiman Haji Trader* ndio ana maduka mengi, sasa akiandika tu kama ambavyo mswada unasema kwamba sasa pawe na *sign post*, kwa hivyo iandikwe *Haji Traders* Saateni, *Haji Traders* Darajani, kwa hivyo huyu ajulikane kwamba ni mteja mmoja au ikiwa ni *branch* basi iwe *consistence* kwa wote kusije kukawa na mparaganyiko.

Suala jengine Mhe. Spika, liko katika kifungu cha 6(2)(b). katika kifungu hiki kinasema maombi yote ya usajili yatalazimika kufuata masharti yafuatayo. Kifungu (b) kinasema ithibati kutoka kwa chombo chenye mamlaka au mamlaka ya leseni. Sasa hapa pana utata hapa, ingawa kamati tuliiipitia lakini kila ukienda mbele wanazidi kuona. Mamlaka au Mamlaka ya leseni pana matatizo hapa, kwa sababu mamlaka ni jambo kubwa, hata Mamlaka ya Maji ni Mamlaka kwa sababu ina mamlaka katika maji. Je, wakitoa wao karatasi itakubaliwa hawa? Kwa hivyo, ama iwe moja kwa moja mamlaka ya leseni au hii mamlaka iainishwe ni mamlaka gani?

Katika kifungu cha 6(e) sharti jengine lolote kama itakavyoamuliwa na kamishna, sasa hapa tumempa uwezo mkubwa sana kamishna, ikiwa haitotolewa (e) basi mimi pendekezo langu liwe ndani ya mamlaka ya sheria hii. Kwa sababu anaweza kuamua tu kamishna. Unajua wazungu wanasema tukitunga sheria au tukitunga kanuni tuwe *objective* na tusiwe *subjective.*
Objective maana yake tunatizama mazingira na kila kitu na hali zote na *subjective* unakuwa unamtizama mtu usoni, pengine yule kamishna uliyonae au mkubwa aliyepo wakati ule ni mzuri sana anasikiliza kwa hivyo unamtizama usoni aa huyu hawezi, lakini yule ni binadamu anaweza akaondoshwa, akaondoka kwa njia yoyote ile akija mwengine je atakuwa kama yeye.

Sasa ukimpa uwezo mkubwa kama huu kuwa sharti jengine lolote atakalosema kamishna, kanikoshee gari langu leo ndio upate leseni hapa hii itakuwa si nzuri. Napendekeza kwamba kiondoshwe hiki au kifanyiwe marekebisho kwa kuingizwa jambo jengine litakalomfunga yule kamishna kwamba asije akatumia madaraka yake visivyo.

Mhe. Spika, twende katika kifungu cha 11 katika mswada huu, kifungu hiki kiko katika *marginal note* ya kusajiliwa. Kinasema "bila ya kujali masharti ya kifungu cha 5 cha sheria hii endapo mtu anayewajibika kusajiliwa chini ya sheria hii ameshindwa kuomba usajili mtu huyo atahesabika kuwa amesajiliwa chini ya sheria hii kuanzia tarehe aliyopaswa kusajiliwa au tarehe nyengine kama itakavyoamuliwa na kamishna".

Mhe. Spika, hapa vile vile pana mashaka kidogo. Kwa sababu huko nyuma kulitangulia masharti ya kujisajili, kuna vitu na *document* zinazotakiwa apeleke, sasa tulitoa hoja katika kamati kwamba hii iwe alazimishwe kujisajili. Kwa sababu atamsajili vipi *automatic* yule wakati *document* zake hajapeleka na saini yake haijapatikana, itakuwaje kwamba kamishna awe anamsajili bila ya kumpa fursa ya kujieleza.

Kamishna kapata zana kwamba huyu mtu hajajisajili na angestahiki kujisajili katika ulipaji wa kodi, lakini yeye hajapata ithibati, kwa hivyo atalazimishwa kwenda kujisajili na sio isomeke kwamba kamishna atajisajili moja kwa moja. Hii itaondoa ile Wazungu wanaita *prejudice* ya kumdhania mtu halafu pengine ukampa hukumu iliyokuwa sio yake. Sio kusajili tu hapa kwamba malipo ya kodi yataanza katika tarehe hiyo aliyotarajiwa kujisajili wakati yeye hajaitwa na hajatakiwa atoe ithibati yake.

ZRB ambayo itasimamia sheria hii imekiri kupatikana kwa mamlaka za leseni, kwa hivyo ina maana wako ambao watatoa leseni iliyokuwa yeye si *ZRB*. Kwa njia hii ina maana taarifa zilizoko za leseni zitakuwa nje ya *ZRB* hivyo inapaswa imwite huyu pamoja na hizo *document* zake. Sasa ikithibitika kwamba yeye kweli anastahiki kujisajili basi atajisajili, huenda ikawa ni yale maduka ambayo yaliyosemwa biashara zaidi ya moja anauza *branch* tu yeye ya duka sio duka lote.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 33(2) na (3), ilikubaliwa katika kamati na nashukuru kwamba katika masahihisho imekuja hivyo hivyo kwamba riba itakayotokana na adhabu ya kodi itatozwa kwa *PBZ*. Mimi binafsi naona bado haijaridhi, kwa sababu huku chini imetajwa Benki Kuu na Benki Kuu ndio inayotoa riba ambayo iko katika viwango vilivyo vya chini katika riba za mabenki. Kwa hivyo, ilivyokuwa yule mtu atalipa kodi na atalipa riba ya kodi, kwa nini alipishwe riba iliyotokana na benki za kibiashara? Itakuwa ni kumkwamisha na ukimkwamisha biashara yake itakapokufa itakuwa hata huyo mlipa kodi humpati tena. Kwa hivyo, matokeo yake itakuwa kodi huipati na hiyo riba itakuwa huipati, bora kuchukua hicho kidogo.

Mheshimiwa mmoja alitoa mfano wa bata aliyetaga yai la dhahabu akaona bora amchinje apate yote yaliyomo ndani, matokeo yake hakupata chochote

chengine. Basi bora ungojee hili hili moja litakalotagwa kila siku kuliko kumchinja ukapata yote yaliyomo ndani kwa mara moja. Kwa hivyo, afadhali tukubali kwamba riba itakayotozwa ni ile ya Benki Kuu kama mnavyolipania serikalini mkichukua hundi gani sijui hati fungate.

Sasa Mhe. Spika, hapa kifungu cha 3 kinasema tena, tazama mkwamo huo. Riba itakayolipwa chini ya kifungu hiki ikiwa haitolipwa itachuma riba. Hii inaitwa *compound interest*, haifai hivi jamani. Hao ni wafanyabiashara na wao watarazaki, basi ikiwa hakupata ile riba na riba nayo inachuma *compound interest* tutafika wapi. Hii tungojee angalau *drill* ya mwanzo ianze kule Tundaua. Ikiwa kisima cha mwanzo kitakuwa *pumped* kule Tundaua sasa tunasema nchi imeshaingia neema basi wafanyabiashara likizo yao imekwisha kwa sababu neema ipo.

Lakini tukumbuke kwamba kuna kipindi kimoja katika uislam tunajua kwamba mwizi anakatwa mkono. Lakini kuna kipindi Sayyidna Omar aliisitisha hukumu ile kwa sababu ya njaa iliyokuwepo, watu walikuwa wakiiba kwa njaa. Sasa katika umaskini kama huu tulionao sisi, umaskini wa kipato wa shilingi 1,500/= kwa kila siku kwa mtu, hii ndio pato la serikali lililosema earning yetu. Halafu wafanyabiashara wanatozwa kodi hizo pamoja na *VAT* ambayo tunaitoa sisi wananchi, lakini mzigo wote unamuangukia yule yule mwananchi kwa sababu hakuna mfanyabiashara ambaye atakubali kuuza bidhaa yake akala hasara.

Kwa hivyo, kadri unavyomkamua mfanyabiashara wakati huo huo unamkamua mwananchi.Sasa tusiweke hizi adhabu zikawa kali mno kiasi cha kuwafanya hawa ni wafungwa ndani ya nchi yao. Ingawa ukitetea sana wanakwambia hupati kitu kwa sababu wafanyabiashara wagumu hawatoi kodi haitapatikana. Ndio nikasema kwamba nafikiri hakujaendelezwa tu. Kwa sababu hii *ZRB* haikuanza zamani kwa kihistoria, lakini namna inavyofanya kazi ni kwa kuwa watu wamekubali kulipa hizo kodi. Sasa wale waliokubali kulipa zile kodi wasikamuliwe zaidi na zaidi wafanyiwe njia ambazo riba ile itakapopita muda wa zaidi ya miaka mitatu haitolipwa. Lakini riba ya chuma riba Mhe. Spika, ni kubwa kidogo hiyo.

Mhe. Spika, pamoja na hayo ya kusema kwamba kiwango kichukuliwe na benki. Lakini kifungu cha 34 (2) kinasema hivi:

> “Kwa kufuata masharti ya kifungu hiki, Kamishna ataamua kiwango cha riba kwa madhumuni ya kuwasilisha marejesho ya kodi na malipo ya kodi chini ya sheria hii”.

Sasa,kwa nini imeshawekwa kiwango ni cha benki halafu aachiwe Kamishna tena kuamua. Kwa hivyo, kidogo kuna mazonge mazonge.

Mhe. Spika, huu mswada ni mrefu, nawaomba wenzangu waendelee kuuchangia. Lakini madhumuni iwe ni serikali kupata mapato kwa njia inayostahiki. Hivi sasa kuna ushindani mkubwa uliojificha baina ya biashara Dar es Salaam na biashara Zanzibar. Tayari sasa hivi kuna tetesi nyingi na pengine ukweli uliokuwa upo zaidi kwamba bidhaa Dar es Salaam ni rahisi kuliko Unguja. Tusije tukawafanya wafanyabiashara wetu wale wanaotuletea bidhaa kubwa wakatuponyoka wakenda wakafanya biashara nje ya hapa na sisi tukabaki hatuna kitu. Tuuangalie sana utekelezaji wa sheria hii. Pamoja na kwamba tumechelewa si vibaya wakati wa kutunga kanuni na uendeshaji yaani *regulations* za kufuatana na hii, basi wakaitwa hawa wafanyabiashara wa sekta binafsi na baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wakasikilizwa.

Kwa sababu kwenye kanuni ndio Kamishna anaweza akafanya baadhi ya marekebisho ambayo yana matatizo ndani yake wakaweza kupata fursa wale wafanyabiashara wetu. Mimi sina hisa katika biashara yoyote ya nchi hii. Nikifa leo basi wanangu hawendi wakasema kwamba tuna hisa pahala fulani. Lakini nahisi kwamba kwa sababu wafanyabiashara wananufaisha hii nchi, wananufaisha kizazi chao na wananufaisha maendesho ya serikali, ni watu muhimu.

Tumeona Mhe. Spika, tulivyokwama katika viwanda, viwanda Zanzibar tumekwama kabisa sasa hivi na viwanda vingelikuwa ni sehemu muhimu ya kutoa kodi kwa sababu inaleta bidhaa halafu inasafirisha bidhaa. Sisi kodi tunayotegemea ni *readymade goods*, ni bidhaa tayari zimeshafanywa huko zinakuja kuuzwa tu. Lakini viwanda vingechechemua zaidi kodi, wangetumia umeme, wafanyakazi wao wangelipa kodi. Tumekwama katika viwanda ni kwa sababu gani?

Kwa hivyo Mhe. Spika, hii *ZRB* kazi yake ni kukusanya kodi lakini mimi nazungumza na wizara sasa hivi kwamba wakitaka ongezeko la kodi wachechemue na shughuli za kiuchumi. Moja ni hivi viwanda. Kuna *group* ambayo ilikuwa inatoka hapa Zanzibar ipo Dar es Salaam pale, nilisahau ile sijui ni kwa mwezi au vipi, lakini wanalipa bilioni 9 kwa mwaka nafikiri pale, kwa ile kodi ya viwanda tu basi sio kwa mambo mengine. Ni wafanyabiashara wa viwanda wa hapa Zanzibar wamekwenda kuhamia kule na wana viwanda vyao. Kwa hivyo, yote mawili yaende sambamba.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni muhimu tutazame na zile kodi za Muungano zilizokwama kwa sababu wakati hautungoji. Mhe. Spika, sisi juzi tumekuja tumeapa mbele yako hapa, kesho tukijaaliwa tunataka kuaga kwa sababu tuna

chini ya mwaka mmoja. Kwa hivyo, wakati hautungoji, tukisema kwamba mambo yapo katika pipeline na nini, lakini kodi za Muungano ni kubwa, wafanyakazi waliopo wa sekta ya Muungano hapa ni wengi na kodi yake haipatikani hapa wanatumia huduma za hapa. Sasa kwa nini hayajatatuliwa mambo hayo? Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao hiki cha jioni. Pia Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji katika Mswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pili naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake kwa ujumla kwa kuwasilisha mswada huu ambao umeletwa mbele yetu. Mswada unajieleza vizuri na umefahamika vizuri na ni mswada muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, mimi binafsi niseme kwamba nakubaliana na utaratibu mzima ambao unachukuliwa na Wizara ya Fedha na Uchumi na hasa kupitia kitengo hiki ambacho kinasimamia kodi.

Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia wamesema kwamba usimamizi ambao umewekwa sasa hivi ni mzuri na hasa wa ile *registration* inayofanywa kwa kutumia vitambulisho na data mbali mbali kuona kwamba kila mmoja anahakikisha amesajiliwa katika utaratibu unaokubalika.

Mhe. Spika, utaratibu huu kama ulivyokwishaelezwa katika michango mbali mbali umeiwezesha serikali kuweza kukusanya mapato na mapato yale yanakuwa hayavuji kirahisi. Lakini hata hivyo, Mhe. Spika, hiyo ni njia moja tu ya kuweza kukusanya mapato na kuonekana kwamba kila mmoja analipa kodi.

Mhe. Spika, tatizo kubwa ambalo tunalipata nafikiri ni kwamba ile thamani ya kodi ambayo mtu analipa na thamani ya mali aliyonayo. Hapa Mhe. Spika, nafikiri wenzetu hawa wangekwenda ndani zaidi kuona kwamba mtu analipa kodi kwa mujibu wa thamani ya bidhaa ama biashara ambayo anaifanya. Vyenginevyo tutakuwa na walipaji kodi wengi lakini hatuwezi kupata kodi halisi kwa sababu ile thamani yenyewe inakuwa haijafikiwa kwa kufanya tathmini halisi ambayo ya mlipa kodi.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba mfanyabiashara siku zote ni mtu ambaye anapendelea kupata faida zaidi. Ni wachache tu ambao pengine wanakuwa waumini ambao wanaweza kusema ukweli kwa kile ambacho wanakifanya. Sasa ili twende vizuri katika ukusanyaji wa mapato hayo ya kodi basi ni lazima

tuhakikishe kwamba wakusanyaji wetu wa kodi wanakwenda ndani zaidi na kuona kwamba yule mtu analipa kodi kwa thamani halisi ambayo anaifanyia kazi.

Mhe. Spika, jengine hapo hapo tuone kwamba hakutakuwa na mtu ambaye anakwepa kulipa kodi. Hii itapatikana tu kuona kwamba kila mmoja anawajibika kulipa kodi kama tutakuwa na ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yetu mbali mbali.

Kwa mfano, kama wanavyofanya katika ukaguzi wa dharura kwenye magari. Kuna siku tu wanaamua wanakaa barabarani kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanafanya ukaguzi wa dharura. Pale Mhe. Spika, kunapatikana kodi za aina mbali mbali, kuna wale ambao hawana leseni, kuna magari ambayo hayajawahi kufanyiwa register kwa mwaka ule, lakini kuna mengine bima hayajakata. Kwa hivyo, mapato mengi yanapatikana kwa wakati mmoja kwa sababu ukishakamatwa maana yake lazima utahakikisha kuona kwamba ili pengine usipate adhabu unarekebisha yale makosa yote ambayo umekamatwa nayo siku ile. Mhe. Spika, hili nafikiri ni jambo ambalo linahitajika lifanywe ili kuokoa fedha nyingi ambazo zinavuja kupita njia hizo.

Mhe. Spika, jengine niungane na wenzangu ambao wamesema kwamba ili tupate maendeleo basi ni kuhakikisha kwamba kila mmoja analipa kodi. Hii Mhe. Spika, ni utamaduni ambao utajengeka tu kwa usimamizi mzuri. Tukiweza kusimamia vizuri basi kila mmoja atakuwa na utamaduni wa kuweza kulipa kodi. Mhe. Spika, ulipaji wa kodi ni jambo muhimu na karibu nchi zote duniani nafikiri zinategemea suala hilo la ulipaji wa kodi.

Mhe. Spika, nikitoa mfano mwengine hai tulikuwa na tatizo kubwa la maintenance ya barabara, lakini baada ya kuanzisha ule Mfuko wa Barabara hivi sasa kwa kweli wenzetu wale wa mfuko ule wameweza kusaidia mambo mengi yanayohusiana na matatizo ya utengenezaji wa barabara. Pia mbali na kutengeneza barabara lakini kufanyia grading baadhi ya mabarabara ambayo hayapitiki na bado ujenzi wake haujaanza wanatusaidia sana. Hii inatokana na yale mapato ambayo yanakusanywa. Hii vile vile inatokana na usimamizi mzuri katika ukusanyaji.

Mhe. Spika, jengine ambalo tungelitazama zaidi kwa wawekezaji. Jana nafikiri nilizungumzwa hapa kwamba wawekezaji walio wengi wanakwepa kulipa kodi kwa kubadilisha majina ya hoteli mara kwa mara au kuyauza baada ya muda mfupi, alimradi baada ya ule muda waliopewa kwa ajili ya kutokulipa kodi kwa muda fulani, basi yeye anachukua muda ule ule ukimalizika aidha anaamua kubadilisha jina au anaamua kuiuza hoteli ile kwa mtu mwengine katika

misingi ya kuona tu kwamba anakwepa zile kodi na yeye kujipatia kitu ambacho hajakiharamia.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 10 “Kuweka jina la biashara”. Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kwenye magari tuko vizuri kwa sababu gari lako limesajiliwa na namba na kila kitu, kwa hivyo ikitazamwa tu ile plate number basi akisoma kama yumo mtu wa mapato pale anajua tu kwamba gari hili ni mali ya Fulani na linafanya kazi gani.

Mhe. Spika, katika mfano huo ambao nimezungumza wa magari, magari unalipa kwa mujibu wa uzito wa gari lako, gari la tani tatu utalipa kwa thamani ya gari la tani tatu, tani nne unalipa kwa thamani ya tani nne. Kwa hivyo, hizi biashara nyengine kama nilivyosema basi ni vyema tukaingia katika mfumo huo kuona kwamba tunaitathmini mali iliyopo na inalipwa kwa mujibu wa thamani yake.

Mhe. Spika, jengine nataka nipongeze hatua ambazo zinachukuliwa. Kwa mfano, kifungu cha 41 (1) kinazungumzia malipo yanayoweza kufanywa na mtu wa tatu. Nafikiri kama nimeifahamu vizuri ni kwamba pengine mimi ni tajiri na nina mfanyakazi wangu ambaye ndio anafanya kazi hiyo kusimamia ile mali. Kwa hivyo, maana yake yeye ana uwezo wa kulipa yale malipo yanayohusika bila ya kunihusisha mimi, kama nimefahamu vizuri.

Hii itasaidia kuona kwamba hata kama kumekuwa na dharura pengine kwa yule tajiri aje afanye kazi hiyo, basi yule aliyekabidhiwa mali atakuwa na uwezo wa kulipa na akalipa kwa wakati. Lakini nasema kama nimefahamu vizuri kwa sababu sina hakika kama imekusudiwa hivyo.

Mhe. Spika, jengine linahusu kifungu cha 41 (4) naomba kunukuu.

> “Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya taarifa iliyotolewa chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na si zaidi ya milioni mbili au kifungo kwa muda usiopungua miezi sita na si zaidi ya mwaka mmoja au adhabu zote mbili ya faini na kifungo”.

Hapa pametajwa mkosaji pengine atalipa faini ya shilingi laki mbili na isiyozidi milioni mbili na kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja.

Mhe. Spika, hili nalo nilipongeze, lakini mimi mwenyewe binafsi sipendi sana kuona kwamba mtu anaadhibiwa kwa adhabu kubwa. Ningefurahi kuona

kwamba wenzenu hawa wanatoa taaluma kwa walipa kodi ili watu waweze kuelewa hasa nini wameelekezwa na athari yake ni nini iwapo utafanya jambo fulani.

Kwa sababu Mhe. Spika, mtu unapompeleka pale Chuo cha Mafunzo siku moja tu basi kwa kweli ni tatizo. Kwa hivyo, ili kuepusha hili mimi ningeomba kwamba taaluma itolewe zaidi pamoja na kwamba ninahakika tumeshatoa taaluma, basi tusiache kutoa taaluma mara kwa mara ili wenzetu hawa wasipatwe na kadhia hii ya kufikia hatimae kufungwa.

Mhe. Spika, kama walivyotangulia kusema mchangiaji wa mwanzo na wa pili kwamba waweze basi kujenga utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari kwa sababu itasaidia kuondoa manung'uniko.

Mhe. Spika, jengine kifungu cha 43 "Kufunga biashara". Mhe. Spika, hapa vile vile niseme kwamba kwa maoni yangu tusifike pahala ambapo tutamfanya mtu afike kufunga biashara kwa sababu ambazo ziko ndani ya uwezo wake au uwezo wa mfanyabiashara huyu. Hili pia linahitaji kupata taaluma ya kutosha ili kuona kwamba kila mmoja analipa kodi kwa wakati na kwa utaratibu uliowekwa.

Mhe. Spika, sina tatizo katika kifungu hiki ambacho pengine kimemsema kwamba mfanyabiashara anaweza kuzuiliwa kufanya kazi kwa kipindi cha siku 90 katika kufanya biashara zake, ili kuona tu kwamba anatekeleza hili jukumu kama alivyopangiwa.

Mhe. Spika, jengine kifungu cha 52 kinachozungumzia afisa huyu kutaka msaada wa chombo cha polisi pale ambapo pengine anataka kumchukua mtu ambaye amekwepa kodi au kutaka kumshtaki au kuzuia hiyo mali yake. Mhe. Spika, hapa mimi ningetoa pendekezo kwamba unaposema unataka msaada wa polisi maana yake anaweza pengine polisi akatoa maamuzi ya kutoa huo msaada au la. Lakini kwa sababu polisi kwa mujibu wa utaratibu wa sheria za nchi yetu ni kwamba moja katika kazi zake ni hizo, panapotokea tatizo maana yake yeye anaweza kushirikiana na chombo cha serikali katika kuhakikisha kwamba anasimamia suala hilo kikamilifu. Kwa hivyo, pale kusingekuwa na haja ya kumuomba, ni kuigeuza lugha kusema kwamba kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi basi atafanya kazi hiyo afisa huyo husika na sio kuomba msaada.

Kwa sababu unaposema unaomba msaada kama labda yeye anayeombwa msaada hahusiki kwa njia moja au nyengine. Lakini kwa kuwa yeye ana wajibu wa kufanya hilo basi mimi nafikiri ni moja katika majukumu ya kazi zake hiki chombo chetu cha polisi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na mchango mdogo sana katika hapa. Lakini hata hivyo, la mwisho ambalo ningetaka nilichangie ni vizuri pamoja na kwamba tunaelewa kuwa hiki kipo kwa wafanyakazi wetu hawa ambao wanafanyakazi katika ukusanyaji wa mapato, basi kuwajengea uwezo ili kuona kwamba hawashawishiki na mambo madogo madogo ambayo yatawafanya pengine kukiuka hizi taratibu za ukusanyaji wa fedha. Ninahakika kwamba kwa upande wa mishahara yao ukilinganisha na taasisi nyengine ni afadhali, lakini ni vizuri tukawajengea uwezo zaidi ili kuona kwamba hawashawishiki na mambo madogo madogo pengine wakaweza kuingia katika mtego ambao utawasababisha kupunguza mapato haya ya serikali.

Mhe. Spika, mimi binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Kama nilivyosema mchango wangu hautakuwa mrefu lakini niliona tu kwamba na mimi nitoe baraka zangu na ningekuwa nimewanyima haki wananchi wa jimbo langu kama ingekuwa sikuchangia hili.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu ambao umeletwa hapa ili kupata kuuchangia na kuupa baraka.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka masuala ya kodi yapo katika nchi nyingi tu, kodi mara nyingi huwa inapunguza makero mbali mbali katika nchi. Hii si kama nchi zetu tu, hata hizo nchi ambazo zinazotoa misaada huwa mara nyingi zinategemea kodi za ndani ya nchi. Kwa mfano, kuna baadhi ya nchi huwa tunaziomba misaada na huwa wanatuletea misaada mbali mbali kama ya mambo ya afya, barabara na kadhalika. Lakini ukitazama undani wa nchi zile huwa na wao wanakusanya kodi kutokana na wananchi wao, halafu wakipata makusanyo yale ndio hayo hayo na sisi wanatusaidia katika masuala mbali mbali ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, hili suala la kodi lisiwe geni katika nchi yetu. Hiki ni kitu muhimu kitakachotatua makero mbali mbali ya wananchi wetu. Nataka kuwaambia wanaotusikiliza pindipo mswada huu ukipitishwa wawe tayari na wawe karibu kutoa kodi hizi ili zisaidie katika maendeleo ya nchi yetu. Usikae tu ukasema unakwenda hospitali kutafuta dawa ukategemea zile zinakuja tu, lakini zinapatikana katika michango mbali mbali ya kodi tunayochangia. Ningeshauri mswada huu kwa sote tuliokuwepo hapa tukaupitisha ili kusaidia maendeleo yetu.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 13 kifungu cha 4 “Thamani ya Kodi”. Iangalie ukubwa wa bidhaa au duka isiwe kodi sawa hata bidhaa ikiwa ndogo. Mhe. Spika, kama inavyoeleweka baadhi ya wananchi wetu wengi maduka yao

yanakuwa ya mchanganyiko. Baadhi ya maduka tunayo madogo ambayo tunayo mitaani na kuna baadhi ya maduka ni makubwa, pia tunao wafanyabiashara wakubwa ambao ni wawekezaji, wenye mahoteli na wenye shughuli mbali mbali.

Kwa hivyo, katika utozaji wa kodi hii ningeomba waangalie sana kulingana na hali ya biashara ilivyo kwa wafanyabiashara wetu hawa. Isiwe kodi inatozwa kwa kila mfanyabiashara ikawa wafanyabiashara wote ikawa sawa tu. Hii italeta mapungufu kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo. Au ichukuwe mfano wa biashara iko mtaa wa Mji Mkongwe tu, kwa hivyo kwa kuwa iko pale ikawa thamani ya kodi yake ikawa moja tu, hii italeta mapungufu.

Kwa hivyo, ningewaomba watendaji katika kutoza kodi hizi waangalie ukubwa wa ile biashara yenyewe ilivyo, mfanyabiashara huyu yuko vipi au duka lake liko vipi, ndipo itolewe thamani kwa mujibu wa ile bidhaa iliyokuwemo ndani ya duka lile. Kuna njia nyingi tu za kupatia kodi na wafanyabiashara tunao wengi tu, lakini pindipo tukienda kwa uangalizi kama huo, naamini tutapata kodi ya kutosha ya kufanikisha mipango yetu.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 14 kifungu cha 5, kusajili na kufutwa usajili. Mhe. Spika, mtu hatofanya biashara Zanzibar mpaka asajiliwe. Hii Mhe. Spika, naona kidogo italeta utata, kwa sababu kuna baadhi ya wafanyabiashara wadogo wakati anapoanza kufanya biashara yake anaanzia hatua ndogo ndogo, tusema kama atakuwa anauza viguo viguo, mafuta mazuri na mengineyo.

Kwa hivyo, tatizo la mfanyabiashara yule kama itakuwa kabla ya kufanya vile unamsajili, wakati mwengine anaweza akashindwa kulingana na masharti yale ya kusajili, basi ikawa biashara ile asiifanye. Mimi ningependekeza hapa atizame kwa uwiano. Kama mfanyabiashara kaja kaanza kufanyabiashara, kwa hivyo katika kule kuanza kutakuwa na wafanyakazi wanaohusika ikiwa kama ni masheha au mabalozi pamoja na madiwani ili kuiona ile biashara yake kama inakua au keshaisimamisha sawa sawa, kwa hivyo kumripoti katika chombo kinachohusika cha usajili ili na yeye atambuliwe na waje wakaguzi wa bodi ya usajili ili kupata kumtoza na yeye kodi kulingana na ile biashara yake. Lakini kusema kwamba mfanyabiashara kwanza asije mpaka asajiliwe, hii naona wengi tutawakosa.

Kwa hivyo, kama tutafanya wepesi wa kuwaacha kwanza waanze halafu ndio wasajiliwe, hii kidogo itasaidia tutawapata wafanyabiashara wengi na kupata kutoza kodi mbali mbali.

Mhe. Spika, katika usajili kuwepo na uwiano, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba usajili uwepo na uwiano kutokana na ukubwa wa ile biashara. Kama inavyoeleweka hapa kwetu tuna wafanyabiashara wengi tu na wana biashara mbali mbali. Kuna biashara za uwekezaji, kuna biashara za uvuvi, kuna biashara za maduka ya vyakula na kuna biashara za vitu mbali mbali tu. Kwa hivyo, hapa ni vizuri kuwepo na uwiano wa kuangalia zile biashara zilivyo na namna gani ya kutoza kodi. Tusitoze tu kodi, kama mfanyabiashara basi mfanyabiashara yeyote tu yule tukamtoza, tutizame na uwiano wa biashara yake halafu ndio tutoze kodi.

Mhe. Spika, halafu kuna wafanyabiashara wengine huwa biashara zao wanafanya katika maduka yao zaidi ya biashara moja. Duka hilo hilo moja, utakuta kuna nguo, vipodozi, vinyago na vyengineo. Kwa hivyo, utakuta mfumo wa wafanyabiashara wetu hapa Zanzibar bado haujawa kama mfumo wa wafanyabiashara wenzetu nchi za nje. Kama alivyosema Mhe. Rashid Seif hapa kwamba kuna baadhi ya maduka ukienda nje utakuta duka lina urefu zaidi ya mita moja au kama urefu wa futi kumi, lakini utakuta mna biashara moja tu, ikiwa ni nguo basi ni nguo tu, ikiwa ni majembe basi ni majembe tu. lakini hapa kwetu bado hatujafikia mfumo huo ni maduka machache tu ndio utayakuta yana mfumo huo.

Kwa hivyo, ningependa hao watoza kodi wakayaangalia sana baadhi ya maduka hayo kwa kulingana na wingi wa zile biashara zao walizokuwa nazo ili na wao wakawatoza kodi kwa mfumo wa zile biashara zao.

Vile vile kama mfanyabiashara mmoja akiwa na maduka kama manne au matatu katika eneo moja, kwa hivyo ningependekeza na hayo maduka kila moja likatozwa kwa mujibu wa duka lake. Kama itakuwa yote anayasimamia yeye basi yawe na namba au *alphabet*. Kama maduka ni matano basi ataanza na mfano Suleiman Abdallah duka ‘A’, Suleiman Abdallah duka ‘B’, yaani yanakuja kwa utaratibu huo mpaka maduka yake yote matano yanamalizika na kila duka linatozwa kwa mujibu wa biashara yake aliyokuwanayo. Hapo ndio tutakapofanikiwa kupata mapato na kodi ile ambayo tuliyokuwa tumeikadiria. Isiwe mfanyabiashara yule kwa kuwa ana maduka matano msajili ni yeye tu peke yake, basi ikawa kodi yake inalipwa kwa lile jina lake yeye moja kwa maduka yake yote matano, kwa njia hii tutakuwa hatufiki pahala. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, watoza kodi hawa waangalie kwa mfumo huo.

Mhe. Spika, nakuja katika marejesho ya kodi. Marejesho ya kodi yako katika ukurasa wa 18 kifungu cha 2. hapa imezungumzwa kwa kila mlipa kodi aweke kumbukumbu za mauzo yake na risiti inapofika tarehe 15, kwa kila tarehe 15 aweke kumbukumbu hizo. Hapa Mhe. Spika, mimi ningeomba kabla ya hapo basi wakaguzi hawa wawe na kawaida ya kuwapitia wale waliokuwa

wamesajiliwa kulipa kodi ili kuangalia mabuku yao kabla ya tarehe hiyo, kwa sababu kuna mbinu nyingi ambazo zinatumika. Mlipa kodi yule huwa wakati mwengine ana mabuku mawili au matatu, jengine inakuwa siri yake na jengine ndio analotoa risiti. Kwa hivyo, utakapokwenda wewe kuangalia malipo yale na kodi ile jinsi alivyoifanya basi anaweza kukupa wewe lile lililokuwa nyeti ambalo lililokuwa silo alilokuwa analitumia kwa wale wateja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeomba wakaguzi wetu wazidishe kasi kwa walipa kodi hawa waliosajiliwa ya kuwapitia mapema kabla ya ile siku, ili kupata kujua ni namna gani mauzo yale wameyafanya na namna gani watakavyolipa kodi, ili kuzuia mwanya wa kutorosha mapato ya kodi.

Mhe. Spika, kwa kweli tuna wafanyabiashara wengi hapa visiwani kwetu na wanajitahidi kufanya biashara. Mhe. Spika, hawa walipa kodi ningeomba tu katika mikakati yao wawe makini na wazidishe uadilifu ili wafanyabiashara hawa wapungukiwe na baadhi ya mambo mengi katika kutaka kulipa kodi. Kwa mfano, kuwepo urasimu kama baada ya kutaka kulipa kodi kupitia ngazi moja au mbili, kuwepo ngazi kama tatu au nne hii inaleta usumbufu. Kwa hivyo, ningewaomba waratibu hawa wachukuao kodi basi wafanye mipango mizuri ya kupanga ili kupunguza masuala ya urasimu kwa yule mteja ambaye anataka kulipa kodi kuwa na njia nyingi ambazo za kupitia ili kuweza kulipa kodi hiyo. Kwa hivyo, wafanye urahisi ili mlipa kodi huyo awe na hamu ya kulipa kodi kwa urahisi ili na sisi tufanikiwe kwa urahisi kupata mapato yale.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 20 kifungu cha 22 kumbukumbu, nyaraka na ukaguzi. Nyaraka halisi za mauzo ankara za kodi na risiti. Hii kwa kweli Mhe. Spika, inataka iangaliwe kwa kina, kwa sababu kama inavyoeleweka sasa hivi katika nchi nyingi sana kumekuwa na wataalamu na watu wengine waliokuwa wanaiga. Mfano kitu kinatayarishwa rasmi au kinatengenezwa, lakini utakuta kitu kile kile watu wabaya wachache tu wanakiiga na wao kikawa mkumbo mmoja yaani vile vile kama kile halisi ambacho kimetegemewa na umma.

Kwa hivyo, kwa hapa nitawaomba wawe makini sana katika utoaji wa risiti hizi na mabuku haya ya kulipia kodi. Kama kutakuwa na risiti au mabuku ya kulipia kodi, basi mihuri iwe inalingana na taasisi ile husika, na yule aliyekabidhiwa iwe yakienda kukaguliwa basi yawe yanaoana. Bila ya hivyo itakuwa kazi yetu haitofua dafu, itakuwa ni sawa sawa na kutia maji kwenye kinu ukatwanga na ukawa hufanikiwi na lolote. Kwa hivyo, nawaomba watendaji hawa wawe waangalifu sana katika utoaji wa risiti na vielelezo mbali mbali juu ya ulipaji wa kodi hizi.

Mhe. Spika, kwa kuwa mara nyingi nchi ikiwa na wafanyabiashara wengi ndio inaleta matumaini ya kufanikiwa kwa kodi hizi ambazo tunazihitaji. Kwa hivyo, ningewaomba watendaji hawa waangalie nini kilichokuwa ni mvuto, ambacho kinasababisha baadhi ya wafanyabiashara wengi kuja hapa nchini kuvutika na wao kufanyabiashara ili kupata kutuingizia mapato. Nawaomba sana hili waliangalie na wajaribu kuangalia baadhi ya nchi jirani za wenzetu, kwa nini wanafanikiwa kuwa na wafanyabiashara wengi ili kupata mapato. Kwa hivyo, na wao wabuni kama kuna mbinu ya kutoa unafuu kidogo basi wautumie, kwa njia kama ya kuingiza au ya kutoa. Japo njia moja ambayo itakuwa inaonesha dhahiri kwamba tunaweza kufanikiwa na wadau wengi pamoja na wafanyabiashara mbali mbali kupata kuja kufanya biashara hapa ili kupata mapato. Nawaomba wabunifu wetu wabuni zaidi ili na sisi tufaidike.

Mhe. Spika, kuna nchi moja inaitwa Dubai, nchi hii kwa kweli wengi tunaijua na tunaisikia. Utakuta nchi ndogo tu Mhe. Spika, lakini mfumo wa biashara yao kwa kila mwaka inakua na kupata wateja wengi wa kuingia na kutoka. Kwa hivyo, utakuta inaingiza mapato mengi. Kwa vile nchi yetu na sisi ni kisiwa, ningeomba hawa wabunifu wetu wangeangalia zaidi nini kitawavutia zaidi wafanyabiashara ili wavutike kufanya biashara kubwa zaidi na sisi tukaweza kufaidika na mapato.

Kwa mfano, katika kipindi cha nyuma tulikuwa na biashara nzuri tu, walikuwa wafanyabiashara wengi tu wakubwa wakubwa, ukija wakati wote mji wetu ulikuwa na wateja mbali mbali ambao walikuwa wakifunga mizigo kusafirisha na kuingiza kwa kipindi kirefu. Lakini ilifika kipindi hapo katikati ikakatika na ikawa usumbufu baadhi ya watu wakawa wanahamisha biashara zao kwenda katika baadhi ya nchi jirani. Sasa hivi tunashukuru *Alhamdulillahi* wengi wameitikia wito na sasa hivi wanarudi kushiriki katika biashara zile. Kwa hivyo, kasi hii isipunguwe izidi zaidi na itizamwe nini kilichokuwa ni mvuto zaidi ili kuwapata wafanyabiashara wale na kuweza kuendeleza biashara zetu ili tuweze kupata mapato ya kujinyanyua katika mipango mbali mbali ya kimaisha.

Mhe. Spika, kwa kuwa nyanja hii ni muhimu sana katika nchi. Kwa hivyo, mimi naunga mkono mswada huu kwa kushirikiana na wananchi wangu wa Jimbo la Amani mia juu ya mia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu katika mswada huu uliowasilishwa na Mhe. Waziri. Kwanza niungane na wenzangu kwamba suala la kodi ni muhimu katika nchi zote kwenye dunia hii, serikali inawajibu wa kuweka utaratibu mzuri wa kuweza kuzisimamia utaratibu wake. Pia na kutoa taaluma kwa wananchi ili waweze kuelewa nini kodi na faida yake ni kitu gani. Kwa sababu tukitoa

taaluma kwa wananchi pamoja na wafanyabiashara, basi kila mmoja atachukua juhudi ya kuweza kuisaidia serikali kupatikana kodi hizi. Kama taaluma haikutolewa vya kutosha, bado kodi itakuwa ina sehemu mbali mbali ya kupenya.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, pamoja na jitihada zote za kuweka sheria, lakini bado taaluma tuitowe kwa wananchi wetu pamoja na wafanyabiashara kwa kufanya vipindi vya aina mbali mbali na vijarida ili watu waweze kuelewa na wakielewa tutapata nafasi nzuri ya kuweza kukusanya kodi zetu.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu katika mswada huu ambao una vifungu kama vitano. Nianze sehemu ya kwanza katika ukurasa wa 12 unaotoa ufafanuzi wa maneno. Nilikuwa nina mawazo mapya katika baadhi ya sehemu, namuomba Mhe. Waziri kama yatakuwa ni ya msingi basi ayaongezee ili kuweza kuiweka sheria yetu katika hali nzuri.

Mhe. Spika, mwanzo kabisa nakuja kwenye ufafanuzi au tafsiri ya neno ‘biashara’ naomba ninukuu, anasema;

Neno ‘biashara’ maana yake ni aina yoyote ya biashara au shughuli ya kibiashara.

Mhe. Spika, sasa nimepata mtihani na wenzangu wamezungumza. Unajua biashara zinapitana, anaweza mtu akauza uji, akapanga tungule na akapanga nazi lakini anapata riziki yake. Kuna mtu mwengine ana maduka anauza mabati na anauza magari. Sasa ukisema ni biashara yoyote kidogo inaleta utata, kwa sababu huyu wa chini unamchanganya kwenye kundi ambalo si lake.

Kwa hivyo, napendekeza kama itakubalika, basi biashara tungezigawa kwa makundi. Tungesema biashara ni aina yoyote ya biashara inayoanzia kiasi fulani cha fedha au kiasi fulani cha mtaji, hiyo ni biashara kubwa. Biashara ndogo inayoanzia mtaji fulani kuja chini, itakuwa kidogo muuza tungula na uji umemtoa kwenye kundi kubwa ambalo halimuhusu. Lakini hivi ilivyowekwa imekuwa unamchanganya na atakuwa hajisikii raha. Wengi ukiwachanganya namna hii basi wataogopa hata kufanyabiashara.

Kwa hivyo, nashauri kwamba wataalamu wapo na yeye mwenyewe Mhe. Waziri basi tutizame hivi biashara katika tafsiri hii kisheria tunawatia kundini watu waliokuwa hawamo. Sasa kama itawezekana basi tutenge biashara kubwa na biashara pengine za kati na biashara zinazokuja chini. Hilo ni wazo langu la kwanza.

Mhe. Spika, wazo langu la pili liko katika ukurasa wa 13 tafsiri ya mtu, naisoma kwanza ilivyo halafu na mimi nitowe mawazo yangu. Naomba kunukuu;

'Tafsiri ya mtu ni mtu binafsi au taasisi inayojumuisha mlipa kodi'.

Mhe. Spika, hapa pia vitu viwili tumevichanganya. Mtu binafsi ni mimi naweza kuuza duka la nguo. Taasisi ni kama ushirika ambao wanaweza kufungua kampuni au kitu chengine, sasa ukinichanganya ukatafsiri basi umenitia kundi si langu. Kwa hivyo, nashauri mtu tumtafsiri peke yake.

Kwa mfano, mtu maana yake ni mtu binafsi anayejumuika kulipa kodi. Halafu tunakuja taasisi ama ushirika unatafsiriwa, kwa sababu taasisi humu imetumika na ushirika imetumika lakini haimo kwenye tafsiri. Kwa hivyo, nawaomba wanasheria, mimi sio mwanasheria ni mwanasiasa, sasa kama inaelekea inakuja basi tungetafsiri ushirika kwa sababu umetumika humu ama taasisi pia tungetafsiri. Lakini sio mtu achanganywe na taasisi. Kwa mawazo yangu naomba na hilo kama litakuwa ni la msingi basi wataalamu wapo na wanasheria wapo tungebadilisha kidogo.

Mhe. Spika, suala la tatu nakuja kwenye ukurasa huo huo katika neno 'kodi' naomba ninukuu halafu nitowe mawazo yangu.

Kodi inajumuisha kodi, malipo, gharama, ushuru, ada, faida, faini, adhabu, riba inayowekwa chini ya sheria hii. Sasa nakuja kwenye neno 'riba'. Naomba kunukuu;
Riba ni kitu mbali na pia tumeshakitumia humu, sasa nadhani kodi ingetafsiriwa mambo yote ikatolewa riba, halafu riba ikatafsiriwa upande wake, riba ni nini. Riba ni mtu ambaye kakusudiwa alipe kodi hakulipa, sasa ikifika muda fulani ndio inakuwa riba, lakini tunachanganywa mahala ambapo nahisi mimi kama sipo. Kwenye kodi tungesema tu hivi hivi kulipa faini ni nini, lakini ukisema riba, riba ni kitu chengine na kimeelezwa ndani ya sheria.

Kwa hivyo, nadhani wanasheria wapo kama ni jambo la busara basi riba tuitafsiri mbali, ili mtu akisoma riba ni nini. Riba ni mtu kakaa muda fulani hakulipa, sasa ikifika muda fulani ndio inakuja riba. Kwa hivyo, kila mtu anaelewa kwamba aah! Kumbe kama mimi sikulipa kodi kwa muda fulani inabidi nitowe riba ili kufidia pale. Sasa nadhani kitafsiri tungeweka riba mbali ingeeleweka zaidi, na humu pia imetumika.

Mhe. Spika, baada ya kutoka kwenye tafsiri nije kwenye ukurasa wa 14 usajili. Sehemu ya pili na kufuta usajili, mimi nitakuja kwenye, kwanza nashukuru kwamba sheria imeweka wazi kuwa wafanyabiashara wote wanasajiliwa halafu

ndio wanapata hivyo vibali. Pia nilikuwa nina maelezo katika kifungu cha pili na kifungu cha 3. Pamoja na kuwa wenzangu wamechangia kidogo, lakini na mimi nilikuwa nina mchango wa mawazo niliona niongezee inaweza ikasaidia.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 2 naomba ninukuu, kinasema kwamba:-

Kifungu cha 2 ‘Mtu anayekusudia kufanya biashara zaidi ya moja atalazimika kusajiliwa kwa kila biashara’.

Mhe. Spika, nadhani mifano imetoka. Mtu anaduka, duka hilo hilo kachanganya vipodozi, mashati, vitambaa na inategemea mwenyewe anaona biashara yake inatoka vipi. Kwa hivyo, itakuwa ni vigumu mtu asajili kuuza vitambaa tu duka hilo hilo, halafu asajili kuuza mabegi duka hilo hilo. Mimi nadhani tungefanya utaratibu kwa sababu biashara zetu wengi ni wanyonge hawezi mtu akauza biashara moja, labda sheria ingetafuta utaratibu ili hawa tayari wanafanya hivi isijeikawashika na watu wakashindwa kufanya biashara, kwa sababu sasa hivi isije ikawashika na watu wakashindwa kufanya biashara, kwa sababu sasa hivi wanafanya *Yallah*, halafu anaambiwa na wewe kutokana na sheria iliyopita sasa hivi basi masharti uza mbali akakodi kontena. Kwa sababu wengi wanaofanya biashara mjini yale maduka sio yakwao wanakodi tu kwa watu na kodi sasa hivi zinakuwa kubwa.

Sasa kama nchi yetu kweli inataka kodi basi haya masuala yote tuyatizame, la tumkamuwe ng’ombe maziwa, hana basi tutamuuwa na tutakosa yale maziwa. Mwenzangu alitoa mfano wa bata anayetaga yai la dhahabu. Mimi natoa mfano wa ng’ombe kumkamua wakati maziwa hana.

Kwa hivyo, naomba na hili wanasheria wapo na wataalamu wetu wapo wa biashara tutizame kama sheria hii ikipita nadhani wengi watashindwa kufanya biashara kwa sasa hivi. Sasa naona wakati bado haujafika wa kuiwacha hivi hii sheria, kama kuna njia ya kuweza kuirekebisha basi tungeomba ikarekebishwa ili hawa wanaotarazaki wakaendelea na kazi zao.

Mhe. Spika, nakuja kwenye nambari 3, naomba ninukuu vile vile, kinasema;

Kifungu cha 5(3) ‘Mtu anayekusudia kufanya biashara katika eneo zaidi ya moja atalazimika kusajiliwa katika kila eneo’.

Mhe. Spika, na hili pia ni tatizo. Hivi sasa wapo wanaofanya biashara hizi. Kwa mfano, Suleiman Haji analo duka jiti kubwa Magomeni, analo duka sehemu nyengine Kwamtipura na analo duka Mlandege, Sasa mtu yule anauza mabati katika maduka matatu, wewe unamwambia kwamba asajili sehemu zote

tatu, hiyo itakuwa ni ngumu. Yeye angesajili biashara yake kubwa, halafu yakabaki matawi, mnajua mkienda pale mnafanya hesabu yote kwa jumla. Kwa sababu ni lazima mtu kama yule awe na afisi yake, afisi ile inasajili maduka yake yote. Kwa hivyo, unajua mali iliyoko Mlandege, mali iliyoko jiti kubwa Magomeni na iliyopo Kwamtipura. Kwa hivyo, wakienda watu wanachukua kodi wanachukua pale pale afisini kwa kuchukua vitabu na kufanya hesabu. Lakini ukimwambia akasajili duka la jiti kubwa Magomeni, akasajili duka la Mlandege na akasajili duka la Kwamtipura. Kwa hivyo, kibiashara tunawarejesha nyuma.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, hili lifanyiwe kazi kwa lengo la kukuza biashara, lakini na wafanyabiashara nao watononoke, tusitizame upande mmoja. Kwa sababu kila mfanyabiashara ukimpa hali nzuri na yeye ndio anapata kwenda mbele.

Mhe. Spika, niongeze hapo hapo kwenye wafanyabiashara. Mhe. Spika, kuna adhabu nyingi wamewekewa wafanyabiashara wale ambao ni wakorofi. Lakini sijaona hapa tunzo ama ziada anayopewa mfanyabiashara mzuri, haimo humu. Lakini akichelewa adhabu, riba na kila kitu. Sasa hebu na tutizame kote kote, yule aliyekuwa mzuri mumpunguzie asilimia 5 pengine kwa mwaka au kwa mwezi, ndio watu wanapata kwenda mbele, sasa ikiwa unavuta kamba upande mmoja tu hiyo kamba itakaatika. Kwa hivyo, naomba na hili Mhe. Spika, tulitizame ili kuweza kutengeneza vizuri.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 15 bado ni kwenye huo huo usajili, kwenye kifungu cha 6 maombi ya usajili, kifungu kidogo cha (2)(a)(i) na (ii) naomba ninukuu halafu nitowe mawazo yangu. Hapa kinasema kwamba;-

Kifungu cha 6(2)

‘Maombi yoyote ya usajili yatalazimika kufuata masharti yafuatayo’:

Kifungu cha 6(2)(a)

‘Kuthibitisha kitambulisho’;

Kifungu cha 6(2)(a)(i)

‘Ikiwa ni mfanyabiashara, cheti cha jina la biashara ikijumuisha kitambulisho halali kilichotolewa kwa mwombaji wa ndani au mamlaka ya kitambulisho cha nchi;

Kifungu cha 6(2)(a)(ii)

‘Ikiwa ni ushirika, hati ya ushirika ikijumuisha kitambulisho halali kilichotolewa kwa muombaji wa ndani au mamlaka ya kitambulisho cha nchi;

Mhe. Spika, mimi inayonihangaisha ni hii nchi, mimi nimo humu Zanzibar ndio nchi yangu na nimeomba. Sasa naambiwa au kitambulisho cha nchi. Kitambulisho kipi cha nchi au kadi ya uraia. Kwa hivyo, nilitaka na hii nipewe ufafanuzi tu ili nifahamu. Maelezo yamekaa vizuri lakini mimi nikiyasoma sielewi imekusudiwa nini. Naomba hii kitambulisho cha nchi katika sehemu zote mbili, nambari (i) na (ii) nipewe ufafanuzi, kitambulisho cha nchi kipi cha uraia au *passport*, na mimi mtu ni mzaliwa wa hapa nataka nipate ufafanuzi, ili baadae nitakapokuja kuulizwa na mimi nipate kufafanua.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 16 kifungu cha 10 kuweka jina la biashara. Mhe. Spika, hii nashukuru kwamba huku nyuma wako wafanyabiashara walianza utaratibu huu, lakini imeonekana sasa hivi bora utiwe kwenye sheria ili watu wote wende kwa mfumo mmoja. Wapo wanaoandika mtu kwenye duka lake, pengine Mohamed Seif nambari fulani, wengine Ali Said. Wengine wameshafanya na wengine bado. Kwa hivyo, imetiwa kwenye sheria ili watu wote sasa hivi biashara zao waziweke kwenye ubao pale mbele na namba ili watu wajuwe, lakini inafanywa wasi wasi kwamba mji wetu hivi sasa kuna sheria mbali mbali zinazoongoza biashara pamoja na mji wetu.

Mfano, wako manispaa. Mji Mkongwe hivi karibuni yalibanduliwa mabango ya biashara. Je, katika sheria hii haigongani na sheria nyengine mfano Mji Mkongwe. Kwa hivyo, nilitaka na hili pia nipate jibu kwa sababu Mji Mkongwe nao matangazo wanayakubali lakini kwa aina yake. Sasa sijui mlishauriana baada ya sheria hii wataalamu wenu na watu wa Mji Mkongwe, kwa sababu sio sheria moja inamgonga mwenzake. Kwa hivyo, matangazo kuweka ni vizuri, lakini natanabahi hapa kwamba na Mji Mkongwe wanasheria zao za matangazo kama haya ya kuweka nje kwenye maduka. Nilitaka nipate ufafanuzi kama mlikaa pamoja mkashauriana na mkaweza kupata kitu cha pamoja, ndio mkaona mkitie kwenye sheria, kwa lengo la kuweka biashara yenu vizuri. Hiyo mimi siikatai.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 22, hapa panazungumziwa kifungu cha 27, “Kujifanya kuwa ofisa”. Naomba ninukuu halafu nitoe mchango wangu,

Kifungu cha 27 kinasema hivi:-

> "Mtu yeyote atakayejifananiza na afisa aliyeidhinishwa, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi cha fedha shilingi kisichopungua milioni tano na si zaidi ya shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au si zaidi ya miaka mitano au adhabu zote mbili".

Mhe. Spika, mimi mawazo yangu hapa ninaona adhabu imekuwa kali sana. Ningelishauri kwamba kosa lolote lile hasa kwenye utendaji wa kazi kuna makaripio. Labda ingeelezwa kwamba kutokana na kosa la awali atakaripiwa na kupewa onyo kali na kulinyimwa mshahara wa miezi miwili au miezi mitatu mathalani.

Lakini akirejea kosa tena ndio twende kwenye miaka mitano, shilingi milioni kumi. Pengine ni maskini ya Mungu ni njaa tu ilimuhangaisha. Sasa naomba na hili pia litazamwe kwa sababu adhabu imekuwa kubwa na kali mno. Mambo haya hayana mtu mmoja, tunaweza leo tukaitunga hapa bahati mbaya ikaweza mtu ikamrudia. Sasa naomba na hili kama uwezekano upo na wataalamu wapo kidogo tungelitazama tena ili tukapata kitu kinachoweza kikafaa pande zote mbili. Hiyo ninadhani itasaidia sana katika utekelezaji wa sheria yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 33, kifungu 64, kinasema kwamba, biashara baada ya kufilisika au kufariki. Naomba ninukuu na hapa halafu nitoe mchango wangu.

Kifungu cha 64 kinasema hivi:-

> "Endapo kwa sababu ya kifo au kufilisika maslahi ya malipo ya kodi yapo au yatachukuliwa na mtu mwengine masharti ya sheria hii yatatumika sawa sawa na mtu huyo".

Kwanza sikufahamu naona kama kuna kitu kime-mis au vipi, lakini nilivyoielewa ilivyokusudiwa kwamba, tuepushe mbali kafanywa kama mfanyabiashara kafa hakuwahi kulipa kodi, lakini hapo hapo unaambiwa kwamba kafilisika.

Mimi ninadhani tunachanganya vitu viwili tofauti. Kufilisika huwezi kufananisha na kufa. Kufilisika duka linakuwepo na mwenye biashara yupo, kama alikuwa na biashara ya shilingi milioni kumi, kaja mpaka shilingi milioni moja, huyo kafilisika lakini mwenyewe yuhai na duka lihai. Kusema mtu kufa, hayupo mtu lakini duka limebaki.

Sasa ninadhani tutizame hivi ni vitu viwili tofauti. Nilivyofahamu mimi ninadhani mtu akifa paachiwe tu huyo atakayekuja kurithi ndio atafanyiwa utaratibu. Lakini ukisema mtu aliyekufa au kufilisika, mtu ameshakufa unamchanganya na mtu aliyefilisika. Sasa ninadhani na hilo wataalamu mulitizame, mimi upande wangu nimeliona halikukaa vizuri, sijui kimaandishi lakini kimaana pia, huwezi mtu aliyekufa ukamlinganisha na mtu aliyefilisika, mmoja yuhai na mmoja tumeshamzika.

Sasa ninadhani na hilo Mhe. Spika, wataalamu kifungu hiki mukitazame kwa lengo la kutizama sheria yetu wananchi waweze kuipokea vizuri na kuifanyia kazi. Ninadhani na hilo likionekana linafaa basi ninaomba mulitazame ili tuweze kwenda uzuri yetu.

Mhe. Spika, ninadhani baada ya hayo machache nitoe fursa kwa wenzangu kwa haya niliyoyaona mimi kwa haraka haraka yamefahamika, na ninadhani Mhe. waziri na wataalamu wake watafanya hiyo kazi kwa sababu kodi lengo letu ni kupata mapato ya kuweza kusaidia nchi yetu, kusomesha, kujenga miundo mbinu, maji, umeme, hospitali na mambo mengine.

Sasa ninadhani hayo yakisimamiwa kwa uzuri na sheria ikafuatiliwa ninadhani dhamira na malengo yetu tutayafikia tunakokwenda.

Mhe. Spika, mwisho kabisa mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Ninakushukuru Mhe. Spika. (Makofi).

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Ninashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kidogo. Lakini Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni inatuelekeza tunapozungumza tukuelekee wewe na maneno tuyaelekeze kwako, lakini jana watu wa televisheni walisema hawanipati vizuri, sasa leo nitaelekea kwa Mhe. Mwanajuma, hayupo ili wenye televisheni wanipate vizuri. (*Kicheko*).

Mhe. Spika, Mswada huu umeandikwa kwa lugha ya kisheria, tena sheria yenyewe inayohusu mambo ya fedha. Sasa si rahisi ukausoma mara moja ukaweza ukaufahamu, lazima uupitie usome na mwengine utafahamu na mwengine hufahamu. Nini madhamuni yake?

Madhumuni yake Wizara ya Fedha na Uchumi wanatwambia "*this is the tool and we finish the job".* Ndio maana yake nilivyofahamu mimi, kwamba wanataka tuwape nyenzo, ili wao wamalize kazi ya kukusanya kodi. Nyenzo yenyewe kuwa tuzungumze, tuutetee, tuurekebishe na hatimaye tuupitishe.

Sasa niwaombe Waheshimiwa wajumbe wauzungumze…

Wajumbe: Zima simu!

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Sio simu yangu bwana! matatizo kule.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa wajumbe pamoja na kwamba ni mgumu lakini waupitie, maana mambo ya fedha kila mmoja anayajua, umuhimu wa kodi kila mmoja anafahamu. Sasa ni vizuri basi tuupitie, tuuchangie na hatimaye tuupitishe ili hiyo *tool* wanayotaka Wizara ya Fedha na Uchumi tuwape waweze kumaliza kazi.

Lakini Mhe. Spika, na mimi kidogo niruhusu kidogo nitoe dukuduku langu kabla sijaingia kwenye Mswada. Mhe. Spika, wakati ninapochangia mimi ama Mhe. Ali Denge Makame ama Mhe. Moh'd Komba Mkanga, Mawaziri hutujibu kiduchukiduchu, lakini anapochangia mfano Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Rashid Seif Suleiman au Mhe. Ame Mati Wadi hujibiwa kwa sana kwa sababu wale wanapiga buti sisi hatupigi buti.

Sasa ila hiyo, hivyo mawaziri wetu wajirekebishe, sisi tunazungumza kwa niaba ya watu maswali tunayoyauliza wakiyajibu wananchi wanapata kuelimika. Mimi leo nitakuwa na maswali mengi, kwa hivyo Mhe. Dr. Mwinyi Haji leo nisikilize upate unijibu.

Swali langu la kwanza Mhe. Spika, ni hii *tin number*, anayetakiwa kuwa na hii team number ni mfanyabiashara ama kila mtu? Kwa sababu humu ndani ya Baraza lako Mhe. Spika, kuna Wajumbe wameagizia gari na huko nje vile vile kuna watu ambao sio wafanyabiashara, lakini anapokwenda kuitoa gari apeleke *tin number* wakati yeye si mfanyabiashara. Sasa nilikuwa ninauliza hii *tin number* ni kwa ajili ya wafanyabiashara ama kila mtu anatakiwa awe nayo.

Kwa sababu kuna mtu anaagizia kitu kimoja kimoja tu labda akenda kulipa ushuru lazima awe na *tin number*. Nilikuwa nikizungumza na Mhe. Ali Suleiman Ali alisema na yeye vile vile ilipokuja gari yake katakiwa *tin number*, lakini yeye kwa kuwa ana biashara nyengine ya daladala, lakini yeye kumbe juzi kenda India kufanya biashara. Sasa yeye inamsaidia lakini kuna wengine haiwasaidii, akishatoa gari ndio imekwisha. Nilitaka kidogo hili suala Mhe. Waziri anisaidie Mhe. Spika.

La pili Mhe. Spika, anayetakiwa kulipa kodi ni mtu anayefanya biashara. Sasa swali langu la pili, Shirika la Umeme haidhuru ni shirika la serikali lakini linafanya biashara, linanunua umeme kutoka Kidatu ama Mamlaka ya Maji

inachimba maji inatuuzia sisi huku, zaidi ya ile *VAT*, kuna kodi nyengine yoyote au kuwa zinaingia katika mfuko wa Hazina hakuna kodi hapo. Ndio nikakwambia Mhe. Spika, leo nina maswali chungu nzima.

Jengine Mhe. Spika, na hili sio langu peke yangu na waheshimiwa wengi humu linawakera. Hii kodi inayoitwa *Income-tax*. Mhe. Spika, taasisi za muungano zote, Polisi, JWTZ, *BOT*, Uhamiaji na wengine ambao wanafanya kazi ndani ya Zanzibar, wanakatwa *Income-tax* lakini *income-tax* hiyo ninasikia Zanzibar haiji, wakati wanafanya kazi ndani ya Zanzibar. Ni kupoteza mapato na tunaambiwa kuwa kodi yote ni mali ya serikali, sio kama alivyosema Mhe. Rashid, kwa upande mmoja ninakubaliana naye kwamba kuna watu wanafikiri serikali kama dudu kubwa limekaa hivi, kila mmoja mwenye mrija wake aende akapachike, anayetia tumboni apate kuvuta lakini sio serikali ilivyo.

Kodi zote ni mali ya serikali. Sasa kwa kuwa kodi zote ni mali ya serikali kwa nini kodi hizi hatuzipati hapa Zanzibar. Ninafikiri sababu kubwa hatuzipati ni kwa sababu zinakusanywa na *TRA* na chombo hiki ni chombo cha muungano.

Nitatoa mfano Mhe. Spika, ilikuwa kodi ya saruji na kodi ya pombe inayokuja Zanzibar ilikuwa hailipwi. Lakini *ZRB* wamegombania mpaka kodi ile hivi sasa inalipwa *VAT* yake. Sasa kwa nini hii income-tax wasipewe *ZRB* ambao wameonesha ufanisi mzuri katika kukusanya kodi?

Jengine Mhe. Spika, nimeangalia kuna vifungu vingi hapa vimefutwa katika sheria ya *VAT*, stamp duty, kuna kama tano hivi. Kuna vipengele vingi vimefutwafutwa na kuna vyengine vimabakia. Sasa kwa kuwa hizi sheria zote na hii sheria kubwa iliyoletwa, zote zinazungumzia kukusanya kodi. Kwa nini zote zisiwe *centralized* pahali pamoja, ikawa sheria moja tu kubwa inazungumzia mambo yote ya kodi kuliko kuwepo visheria vidogo chungu nzima.

Mimi ninafikiri tungelivikusanya vyote hivi ikawa sheria moja tu na inasimamiwa na *One Stop Centre* nafikiri ingelileta ufanisi mkubwa zaidi, kuliko kuwa na visheria vidogo chungu nzima, inaweza vikatiwa kwenye hii sheria moja tu ikawa vinaonesha kila kitu. Ninafikiri Mhe. Waziri angeliangalia hilo ili kuleta ufanisi katika kukusanya kodi. Kuna kodi ya *stamp duty*, *VAT*, *petroleum levy*, kodi ya ardhi, zingeekwa kodi zote pahali pamoja, zikawa zinalipwa pahali pamoja. Ninafikiri ingeleta ufanisi mkubwa zaidi.

Jengine Mhe. Spika, ninachotaka kuzungumzia ni kuhusu usajili wa biashara. Usajili huu hawa wanaosajili hizi kampuni wana matatizo. Matatizo yenyewe yaliyokuwepo, unajua kuna choyo cha biashara. Mfano Mhe. Ali Suleiman kaanzisha kampuni kaweka jina lake anafanya biashara nzuri basi na mimi

ninaweza nikafanya nikaiga nikabadilisha jina kidogo basi mtu mwengine anafanya kampuni kama ile kaondoa “Z” katia “S”.

Sasa hivi kuna kampuni moja Uingereza inaitwa *Phillips*. Spelling yake ni *Philips*, wameondoa *l* moja tu. Kwa hivyo, unaweza kwenda dukani kwa mfano unatafuta pasi unaona *Philips* unadhani ya Uingereza kumbe vile China, lakini wameondoa *l* moja tu.

1. Sasa wanakubabaisha wewe unayekwenda kununua kwa kuwa wao wanataka kufanya biashara na wameona kwamba ile Kampuni ya *Phillips* ya Uingereza ilikuwa ikifanya biashara nzuri zaidi, kwa hivyo labda tukipenyeza hivi na sisi tutafanikiwa, kweli wamefanikiwa na wanauza kweli.

Mhe. Spika, sasa kuna ubabaishaji wa biashara kama hizi kwa majina haya na sijui sisi huku tunayaangalia vipi majina ya biashara hizi ambazo zinasajiliwa.

Mhe. Spika, kuna Kampuni moja hapa inaitwa Muzammil iko peke yake. Muzammil walileta viatu vya wanawake, yaani viatu vizuri kweli lakini chini vimeandikwa Muzammil tena yale maandishi yenyewe yamechongwa. Kwa hivyo, baada ya kufika hapa Masheikh wamekuja juu na kusema hii ni Aya ya *Quraan* wameitia kwenye viatu watu wanakanyaga ni dhambi tu. Kutokana na hali hiyo, ilibidi viatu avirudishe asiuze. Sasa matatizo ya kuweka majina mengi inakuja kama hivyo, kwa hivyo walishindwa kuviuza viatu kwa sababu Masheikh waliwabana kweli “*Yaa ayyuhalmuzammil*”.

Sasa matatizo hayo yanakuja kwenye kusajili hizi kampuni kwa kuweka majina mengine ukaona labda hili la *Quraan* niweke. Lakini baadaye linakuja kukuletea matatizo kama hilo, yaani viatu alivyoagiza karibu na Sikukuu vyote ilibidi virudishwe kwa ajili ya kuondolewa lile jina na hayo ni matatizo.

Mhe. Spika, jambo jengine na leo nimesema nina maswali tu. Kuna mawasiliano kati ya wanaotoa leseni na *ZRB*. Kwa kweli hakuna na ndio maana *ZRB* wanashindwa kukusanya kodi vizuri. Kwa mfano, Halmashauri za Wilaya zinatoa leseni za *bar*, kisheria ya *ZRB* kila *bar* inatakiwa ilipe shilingi 500,000/-. Sasa hakuna mawasiliano baina ya Halmashauri na *ZRB* na matokeo yake *bar* inauzwa kule na wala kodi hailipwi.

Vile vile Kamisheni ya Utalii kuna hoteli ambazo wamezipa leseni lakini hawana mawasiliano na *ZRB*, yaani *ZRB* hawajui kwamba kuna hoteli imepewa leseni na matokeo yake kodi haikusanywi. Mhe. Spika, jana nilizungumza hapa lakini kipengele hiki sikukisema.

Matokeo yake sasa kwa kuwa hakuna mawasiliano basi kodi hazikusanywi vizuri. Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri aliangalie. Kwa sababu bado mfumo wa kutoa leseni kwa Halmashauri za Wilaya, Kamisheni ya Utalii na hata Baraza la Manispaa ni wa kizamani, yaani sio wa kileo. Kwa sababu hawana *computer* kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na baadaye kupeleka kule kwamba hizi tumesajili kwa kutumia *flash*.

Kwa kweli mfumo wao ni wa kizamani, pamoja na mfumo huo lakini bado hawana mawasiliano na matokeo yake mapato mengi yanapotea wakati leseni zimetoka na huko wale wanaokusanya kodi hawana habari, sasa fedha nyingi zinapotea sehemu hizo.

Mhe. Spika, mawasiliano ni mazuri kwa sababu hata mtu anakwenda kukata leseni basi aelekezwe pamoja na kwamba mimi nimekupa lakini nenda *ZRB*. Kwa hivyo, baada ya kumpa maelekezo mazuri basi yule mtu anaweza kufahamu, lakini *ZRB* leo anafuata kwenye *bar* ambayo imeshafunguliwa miezi mitatu au minne kwa ajili ya kuikamata, wanasema kwamba sisi hatukuambiwa. Kwa sababu mawasiliano ni kitu kizuri sana.

Mhe. Spika, nitakupa hadithi moja ndogo tu, kuna jamaa walikusanyika wakamfuata mtu wakamwambia ee bwana ee tumekuja kwako tunataka mchango wako tujenge ukuta wa kuzungusha makaburi yetu, imekwisha. Akawaambia mmebaini maiti wanakimbia? Aaa maana yake watu wasije wakavamia, wengine wanakuja kuchukua mchanga tu. Basi mngenambia mapema kama hivyo, mimi nilifikiri maiti wanakimbia ndio maana mnataka kujenga ukuta. Maana kosa yale mawasiliano hukumueleza vizuri yule mtu.

Sasa kama hukumueleza vizuri ndio atakwambia mimi sikufahamishwa kwamba kuna kodi nyengine nikalipe. Hilo ndio tatizo ambalo tunalipata. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi mawasiliano kati ya taasisi zinazotoa leseni na *ZRB* ili makusanyo yaende vizuri.

Lakini jengine Mhe. Spika, walipa kodi ni wafanyabiashara na biashara ni biashara, wakati wowote biashara inaweza ikafeli ukala hasara. Unaweza ukafunga duka lako ukaja asubuhi limeingia moto, ni hasara. Ama umefunga duka lako au godown lako umekuja asubuhi wameingia wezi wameiba. Matokeo yake utajikuta yule mlipa kodi wako mzuri sasa ameshafilisika. Je, hawa tunawaangalia vipi. Si wafanyabiashara wengi wanaokata bima hasa kwa hapa kwetu, ni wachache sana wanaokata bima. Sasa watu kama hawa ambao ni walipa kodi wazuri je, sisi wakishaanguka tunawasaidia vipi.

Mhe. Spika, mtu akila hasara anachanganyikiwa. Katika miaka ya 70 nakumbuka kuna mwarabu mmoja alinunua gari la kufanyia biashara. Bahati mbaya gari lile bovu kila siku liko garage halendi, basi alikwenda kusali *nawaitu uswali fardha swalati l-ishaa arbaa al-hasara*, *Allah Akbar*. Kenda kuitaja hasara aliyopata kwenye gari kwenye sala, anachanganyikiwa mtu. Sasa lazima watu kama hawa walipa kodi ni vizuri tuwaangalie wakipata hasara. (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Spika, hivi sasa kutokana na uchumi wa dunia kuyumba, Marekani imetoa pesa chungu nzima kuwasaidia walipa kodi wake ili wasifilisike waweze kunyanyua uchumi wa nchi yao. Leo nimeona kwenye nipashe serikali ya Muungano nayo imetoa pesa chungu nzima kuwapa watu wa biashara ili waweze kulipa kodi. Sasa na sisi hapa sikuona kwenye mswada huu, hakuna pahala pakuona kwamba mfanyabiashara mlipa kodi mzuri akifilisika basi atasaidiwa vipi. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri aliangalie hilo.

Kwa sababu katika biashara kuna mambo mengi yanatokea. Kuna rafiki yangu mmoja kenda China kanunua madengrizi kalipa pesa kila kitu kaamini nitilieni kwenye kontena, kawapa watu wa kusafirisha kontena limekuja kontena mpaka hapa. Kenda kalipa *duty* kamaliza wamefungua kontena toa mzigo mna magunia, kenda mpaka Ubalozi wa China anahangaika mpaka leo karibu mwaka mzima hakuna kinachokwenda. Sasa wameshamfilisi huyu, sijui hata hizo pesa alizolipa huku tena kama karudishiwa.

Si huyo tu, kuna mwengine yeye kenda kanunua ma-*speaker* yale makubwa makubwa huko huko China, kanunua *speaker complete* pamoja na jumba lake.Limekuja kontena kalipa kila kitu, kwenda kulitoa mna majumba matupu *speaker* hamna. Hizo ni hasara za kibiashara, sasa watu kama hawa tunawaangalia vipi. Lazima tuwe na kitu cha kuwaangalia ili tuwawezeshe na wao waweze kulipa kodi vizuri.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 (b) kimeandikwa mtu anayekusudia kufanya biashara zaidi ya moja atalazimika kusajiliwa kwa kila biashara. Lakini mimi ningeliomba kiongezwe kifungu kingine kwa sababu wafanyabiashara wetu wana udanganyifu mkubwa. Siku hizi kuna *photocopy* za rangi, kinachofanyika mtu ana duka mfano Malindi kalikatia leseni, ana duka jengine Mlandege, jengine Magomeni anatoa *photocopy* ile anatia kioo anakwenda kubandika pale. Ukenda wewe unakuta *photocopy* rangi kijani ile leseni yao vile vile, kumbe ni *photocopy* leseni amekatia duka moja tu. Sasa huo ni udanganyifu ndani ya biashara.

Mhe. Spika, mimi ningelipendekeza kiongezwe kifungu mtu anayekusudia kufanya biashara zaidi ya duka moja atalazimika kusajiliwa kwa kila duka. Nafikiri hii itasaidia kwa sababu sasa hivi udanganyifu sasa hivi ni mkubwa.

Mhe.Spika, katika nchi hii ukenda Manispaa watu waliokata leseni hawazidi mia tisa, kweli kuna maduka mia tisa mji huu na kila chochoro lipo duka na sasa hivi kila anayejenga nyumba anatia na mlango wa duka. Nafikiri katika nchi yenye maduka mengi baada ya Uingereza na India basi hapa kwetu Zanzibar tunachukua nafasi ya tatu. Mhe. Spika, hayo ndio matatizo tuliyokuwa nayo, na ndio maana nikasema kwenye leseni kuwa na mawasiliano na hawa watu wa *ZRB*, kama kutakuwa hakuna mawasiliano ndio matatizo hayeshi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina mchango mkubwa kwani mswada wenyewe huu ni mgumu wengi wetu unatushinda kuutafsiri lakini tena tunadodosa angalau tumpa Mhe. Waziri *points* za kuweza kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo mimi naunga mkono hoja hii na naamini Mhe. Waziri atanijibu vizuri hatonidharau kama wanavyofanya wengine. Nashukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi niunge mkono mswada huu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani mimi natanguliza kauli ya kusema kuwa kwa niaba yao tunaunga mkono mswada huu wa mambo ya kodi. Pia nawaomba wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwamba tuuchangie mswada huu na baadae tuunge mkono ili sheria hii ifanye kazi ili kodi iweze kukusanywa chini ya sheria ambayo sisi wenyewe tumeichangia vilivyo.

Mhe. Spika, hii nafasi tumepewa na Mhe. Waziri kwenye mswada huu, lakini kabla sijenda mbele niseme mambo ya jumla. Sisi ambao tunawakilisha wananchi na sisi ndio tunao kitumia chombo hiki kulalamikia mang'uniko ya wananchi hasa yakiwa masuala ya kodi. Napenda niwasihi na niwaombe Wajumbe wenzangu hii nafasi tuitumie ili tusiwache mwanya kwa Serikali wananchi wakaja kulalamika kutoa kodi, na sisi wakatuingiza humo humo wakati hapa ndipo penye nafasi yetu ya kuuboresha mswada huu ili mambo yawe mazuri kwa wananchi wetu.

Mhe.Spika, kodi kama ilivyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe ndio uti wa mgongo na ndio kianzio cha fedha hizo ambazo tunajivunia kupata mahitaji yetu ya kila siku. Tunasomeshwa kwenye vijarida, televisheni, magazeti, wanasiasa kwamba pesa hazitengenezwi kwa mitambo tu ila ni juhudi za wananchi wazalishe mahitaji yao lakini sehemu kubwa ni kulipa kodi.

Mhe.Spika, kodi twende katika tawala hizi zetu za sasa na hata zilizopita nyuma kulikuwa na watu wa kukusanya kodi.Kwa hivyo, Serikali kuweka mipango ya kukusanya kodi hili sio jambo geni kabisa.

Mhe. Spika, utaratibu wa kulipa kodi kwa mwananchi umeanza tangu asili naweza kusema tokea mababu zetu kwa Serikali zote zilizopita. Kwa hivyo, kila wakati kuna utaratibu wake tu mahitaji yanaongezeka kwa wingi.

Mhe. Spika, mbali ya mswada huu kazi kubwa ili itaweza kwenda sambamba na yaliyomo katika mswada huu ni taaluma hasa kwa walipa kodi. Wizara ya Fedha, Bodi ya Mapato inajitahidi kutumia vyombo vyetu vya habari, lakini taaluma yenyewe kwenye vyombo vya habari inakuwa ni ya muda mfupi na bado haijakuwa ya kutosha kwa kiwango ambacho wananchi kila mmoja awe anafahamu umuhimu wa kulipa kodi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri huu mswada tunachangia, nina hakika utapitishwa, lakini jambo muhimu kabisa ahakikishe elimu kwa walipa kodi ni kitu cha msingi kabisa na kinawekewa mikakati ya kuwa kila mtu apate elimu kuwa inastahiki kulipa kodi kwa viwango ambavyo vitakuwa vinawekwa.

Mhe. Spika, itakuwa ni makosa kuchukua hatua mbali mbali za adhabu zilizowekwa humu kwa watakaoshindwa kulipa kodi au wanaokataa. Mimi naona sababu kubwa ni kutofahamu juu ya hizi taaluma, nafikiri wakiwa na taaluma nina hakika watu wote watakuwa wepesi kulipa kodi kwa sababu wanahitaji. Kwanza wakishafahamishwa hii kodi mnayolipa ni fedha zenu na zinatumika kwa maslahi yetu, barabara mnayopita ndio fedha zinazotoka huko, walimu wanasema mishahara midogo waongezwe ili walimu wapate nafasi nzuri yakuweza kusomesha watoto wetu ili taaluma iendelee na iwe ya kiwango cha juu. Mhe. Spika, mwalimu bila ya maslahi yakutosha mwalimu hatakuwa na mazingira mazuri yakuweza kusomesha. Kwa hivyo, ni kutokana na fedha ambazo zinatokana kwa njia ya kodi, serikali inapata kuweza kulipa mishahara.

Mhe. Spika, nije katika mswada wenyewe kuanzia ukurasa wa 12-13 humu mna maneno ambayo Mhe. Waziri ningemuomba pia anisaidie. Kwanza kuna neno “afisa aliyeruhusiwa”.Maana yake ni afisa anayefanyakazi chini ya mamlaka ya Kamishna kwa madhumuni ya Sheria hii au sheria nyengine ya kodi. Lakini kodi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nafikiri haitokani kwenye Boti ya Mapato tu, zimetajwa hapa taasisi mbali mbali ambazo zinakusanya kodi. Mhe. Spika, je, tafsiri hii haitawahusisha huko na ikiwa hawahusishi ina maana hawashughuliki na masuala ya kulipa kodi kwa sababu tunajua baadae kodi hizi zote kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaingia kwenye Bodi ya Mapato.

Mhe. Spika, katika ukurasa huo huo kwenye kifungu cha 3 kuna neno leseni ya biashara. Leseni ya biashara inajumuisha malipo, gharama, ushuru, ada, faini na adhabu mimi hapa sijafahamu ningemuomba Mhe. Waziri akija kutoa majumuisho anifahamishe.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4(1) cha thamani ya kodi. Je, huyu mwenye kulipa hii thamani yake ataijua vipi? Kwa bidhaa tumeona imeelezwa kama itategemea wingi lakini huduma pia zinatozwa kodi pamoja na mambo ya vifaa. Kwa mfano, kama mtu ana ghala anakodisha watu kuweka vifaa na anapata pesa nyingi je, mtu wa aina hii anaingia upande gani? Mhe. Spika, hapa ningemuomba Mhe. Waziri pia anisaidie.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 15 kifungu cha 6 maombi ya usajili yatafanywa kwa Kamishna. Hapa ningetaka kujua hivi sasa leseni zote zitakuwa kwa Kamisheni ya Bodi ya Mapato. Nafikiri kama itakuwa hivyo basi kazi itakuwa rahisi zaidi, lakini kama sio hivyo basi mimi kipengele hiki sijakifahamu vizuri. Mhe. Spika, katika uratatibu huu mpya wa kodi na humu tumeambiwa kodi, ada, ushuru zote zinaingia sasa hivi Mhe. Waziri anatwambia leseni zote tukachukue huko mpaka za kukata makaa, kupigia tanu, kukata miti. Kwa hivyo, sasa hivi leseni itakuwa katika Bodi ya Mapato au bado zitakuwa katika mamlaka ziliopo na kwa misingi ipi ili ziweze kufanana na sheria hii ambayo tunaipitisha. Kwa sababu sisi tunatakiwa kuwa walimu wa wananchi juu ya hao walipa kodi.

Mhe. Spika, mambo hayo kama hatujayafahamu yanakuwa yana matatizo. Namshukuru sana Mhe. Waziri kabla ya kuleta mswada huu pamoja na pesa chafu alitupa taaluma, lakini taaluma ile ilikuwa ni ndogo sana. Haya masuala niliyouliza mimi ni kwamba tungepata muda wa kutosha huu mswada baada ya kusomwa na Mhe. Waziri na maoni ya kamati pamoja na waziri kivuli akatia baraka zake basi tungepiga makofi tukenda zetu.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 19/10/2009 saa 3:00 asubuhi)